

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 24 Juni, 2011

(Mkutano Ulianiza Saa Tatuhu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 111

Malipo ya Likizo za Watumishi

MHE. PAULINE P. GEKUL aliuliza:-

Ni haki ya Mtumishi kulipwa likizo yake ya mwaka hata kama muda wa likizo hiyo unaangukia muda wake wa kustaafu:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Watumishi ambao wamenyimwa likizo zao kwa kisingizio kuwa muda wao wa kustaafu umefika na kunyimwa kulipwa likizo zao.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni H. I ya Kanuni za Kudumu (Standing Orders) likizo ni haki ya mtumishi. Endapo mwajiri ataona kuwa hawezu kumruhusu mtumishi kuchukua likizo yake, analazimika kumlipa mshahara wa mwezi mmoja mtumishi huyo. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni H.5 (a) ya Kanuni hizi, mtumishi hulipiwa nauli ya likizo kila baada ya miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, kutokana na miongozo niliyoitaja, ni makosa kutomlipa mtumishi stahili yake ya likizo kabla ya kustaafu.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa katika majibu ya msingi ya Waziri amesema kwamba ni haki ya watumishi wa Umma kulipwa likizo zao pale wanapostaafu.

(a) Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati mwafaka wa kulipa likizo za wastaafu hao ambao wamestaafu lakini hawakulipwa likizo zao?

(b) Kwa kuwa mtumishi anapostaafu anahitaji kurudi katika eneo ambalo ametoka, na kwa kuwa katika shule za msingi katika Halmashauri ya mji wa Babati walimu wapatao watano (5) hawakuweza kulipwa likizo zao walipostaafu tangu mwaka jana mwezi wa kwanza mpaka leo, lakini pia walimu hao hawakuweza kupewa fedha za kusafirishia mizigo yao.

Je, Serikali haioni kwamba imewatesa walimu hao kwa muda wa mwaka mmoja na nusu mpaka sasa hawapewi fedha za kusafirishia mizigo yao makwao na wakati huo huo hawajalipwa likizo.

Je, Serikali inasema nini kuhusu wastaafu hao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOAA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, hapa tunazungumzia sheria hata kama mtu amekaa miaka mitano au mingapi, sheria ikitisima kwamba ni haki yake alipwe na kama hakulipwa hatuwezi kukaa tuna-*debate* hapa, *debate* ya sheria iliishamalizika.

Kwa hiyo hapa kama Mheshimiwa Mbunge anafikiri kwamba kuna watumishi waliondoka bila kulipwa kwa misingi hii ya sheria niliyoitaja hapa atuletee mara moja tutamwona Mheshimiwa Hawa Ghasia na kuzungumza naye na kumwambia hawa walipwe haki yao. Hatuwezi ku-*debate* hapa habari hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge uwe na amani moyoni mwako, wewe katuletee na huyo unayesema kwamba alistaafu hapo akaenda bila kulipwa tuelewane kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka ni-*quotation* kitu kimoja. Haki inayozungumzwa hapa ni haki ya mshahara kwa sababu usije ukasema kwamba nipe mshahara halafu

useme nipatie pia na nauli yangu ya kwenda Muleba, akikulipa mshahara ndiyo habari imeishia hapo kwa maana ya mshahara aliokulipa.

Kwa hiyo, mimi nataka nitahadharishe tu, lakini sisi tuko tayari kusikia hilo tutazungumza nao. Nimeita watu wangu wa *human resources*, tumezungumza na bwana Paraga amenieleza kwamba utaratibu ndiyo huo, lakini mimi niko tayari kumsikiliza tuasaidiane.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Manispaa ya Kigoma Ujiji kuna walimu wengi sana ambao wamekuwa wanaenda likizo hawajapata stahili zao ni zaidi ya miaka miwili, mitatu.

Pamoja na kwamba amesema hilo ni suala la sheria, lakini sheria isiyotekelawa maana yake ni nini sasa? Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kuhusu jambo hili.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, mimi hapa nazungumzia matukio na sheria kwa maana ya nchi nzima. Mheshimiwa Serukamba anasema kwamba kuna watu ambao hawakupewa haki yao. Mimi nimekwenda Morogoro pale nika- *head delegation* pale na nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ambayo ili-review madai ya watumishi wote ukiacha hata na walimu wanaozungumzwa hapa. Tukasema tufanye mahesabu tuangalie kila kitu kinachodaiwa pale, baadaye tukaambiwa kwamba tupeleke madai yale kwa *CAG's Office* aangalie na ahakiki aseme anaonaje kuhusu hayo madai. Taarifa ya CAG ikatoka ikasema kwamba hawa haki zao ni hizi, hawa haki zao ni hizi.

Mheshimiwa Spika, hapa tuna-deal na nchi nzima, inawezekana kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Serukamba kwamba katika hali hiyo bado kuna walioponyoka pale wakawa hawakulipwa haki zao. Mimi namuomba atuletee majina ya wale walimu anaowasema hapa sisi kama Serikali tutashughulikia jambo hilo.

Na. 112

Matokeo Mabaya ya Kidato cha Nne

MHE. VINCENT J. NYERERE aliuliza:-

Matokeo ya mtihani wa kidato cha Nne mwaka 2010 hayakuwa mazuri na yameacha vijana wengi mitaani na vijijini, vijana ambao ni tegemeo la nguvu kazi ya Taifa lakini wamebaki bila elimu wala matarajio yoyote.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya vijana hao wengi waliobaki mitaani kutokana na kufeli katika mitihani yao.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vicent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya mtihani wa kidato cha Nne mwaka 2010 hayakuwa mazuri na vijana wengi walishindwa mtihani huo. Kufuatia hali hiyo na kwa kuzingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Seriakli za Mitaa(TAMISEMI) tumefanya utafiti ili kubaini sababu za ufaulu duni, na nini kifanyike kwa wanafunzi walioshindwa mtihani huo.

Mheshimiwa Spika, kazi hii ya utafiti wa ufaulu duni imekamilika na Serikali itatoa tamko juu ya hilo katika mukutano huu wa Nne wa Bunge lako Tukufu. Aidha, wakati tunasubiri tamko hilo la Serikali, namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wawe na subira.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mabaya ya kukatisha tamaa ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mojawapo ya majibu ya tafiti itakuwa ni ukosefu wa walimu, vifaa vya kufundishia na maabara na si kosa la wazazi na wanafunzi bali ni kosa la Serikali.

(a) Je, Serikali haioni sasa ni muda mwafaka wa kuhakikisha watoto hao wanarudi shulen i ili wasome na wafanye mitihani na washinde ili wasiharibikiwe na maisha hapo baadae?

(b) Je, Serikali haioni sasa ni muda mwafaka wa kufundisha stadi za kazi katika shule za sekondari kwa vitendo ili watoto wanaoshindwa kuingia kidato cha tano waweze kwenda katika soko la ajira moja kwa moja? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vicent Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, moja ni kuhusu sababu za ufaulu duni wa Kidato cha Nne. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli michango yake ni mingi na hatuwezi tukawachukulia wanafunzi wale kwamba wao wenyewe tu peke yao ndiyo walikuwa wana makosa kwa ufaulu huu duni.

mSerikali imefanya utafiti imegundua, lakini kwa lile ambalo Mheshimiwa Mbunge amelipendekeza halitakuwa rahisi kulitekeleza kwa nchi nzima, kwa maana ya kuwarudisha wanafunzi wale wa kidato cha nne wote shuleni katika shule zetu hizi kwa sababu sisi sote tunafahamu kwamba katika shule zetu za Sekondari bado tuna mapungufu ambayo Serikali inahangaika kuweza kuyaweka vizuri ili tuweze kupata elimu bora.

Mheshimiwa Spika, tuna uhaba wa madarasa na vitendeakazi. Sasa hivi kuna vijana tayari ni *Form Four* pamoja na kwamba kuna mapungufu kule madarasani, utakapowaleta tena wengine waingie humo humo kwenye *Form Four* ile bila shaka ni kwamba uwezo hautakuwepo wa kuwahudumia nao kwa lengo la kuweza kufanya mtihani kama wanafunzi wenzao wanaosoma *full time*. Kwa hiyo, hilo bahati mbaya hatutaweza kumudu kulifanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la pili kwamba Serikali ibadilishe mitaala ili iwe na mafunzo ya vitendo ili kumwezesha mwanafunzi awe na uwezo mkubwa zaidi anapomaliza shule. Hilo tutalizingatia, tumeanza kulifanyiakazi na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunalifanyiakazi vizuri zaidi. (*Makofî*)

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona, naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Wizara imetoa mwongozo kwa maswali katika shule za msingi kujibowi kwa njia ya *multiple choice* au kwa kutikii.

Je, Serikali haioni kwamba kwa kuendelea kufanya hivyo tunatengeneza watoto ambao wanafaulu kwa njia ya kubuni kwa kuwa watakuwa wanatiki tu kwa *ku-guess* hali ambayo itaendeleza watoto kufeli kama ilivyojitokeza katika matokeo ya mtihani wa mwaka huu?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agness Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, swali hili ni jipya na Mheshimiwa Mbunge hajasema moja kwa moja kwamba ni somo gani ambalo limefanyiwa utafiti kwamba lina majibu ya *multiple choice*.

SPIKA: Kweli swali ni jipya sana, eeh Mheshimiwa Susan Lyimo swali jingine.

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa ni ukweli ulio wazi kwamba matokeo hayo na mengine yatakayokuja yanakuwa mabaya kutokana na kutokuwepo kwa walimu wa kutosha katika shule hizo. Serikali inalitambua hilo, kwa kuwa pamoja na kwamba walimu wamekuwa wakimaliza masomo yao na kupelekwa katika shule hizo, lakini inaonekana wazi kwamba walimu hao hawaendi kutokana na mazingira mabovu.

Je, Serikali inasema nini kuhusu hilo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyo sema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba tume iliyokuwa imeshirkiana na Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI imefanya utafiti wa mazingira ya mitihani ya kidato cha nne iliyofanyika mwaka jana katika takribani Halmashauri 22, shule 132 katika mikoa 11 yaani ile mikoa ambayo ni kanda za kielimu.

Kwa hiyo, tutegeme Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, atakapokuja na tamko hapa tutalijadili kwa pamoja na kwa sababu Waheshimiwa Wabunge ndiyo mliotupa ushauri kwamba kutokana na matokeo mabaya haya basi ni vizuri Wizara ikaunda tume ifanye utafiti kwa mazingira hayo. Kwa hiyo hayo yote pamoja na maabara, walimu na mazingira yote yaliyojitokeza tusubiri utafiti huo umeishakamilika utakuja na mambo yote hapa na tutakuja kuyajadili.

Na. 113

Benki ya Wanawake Kufungua Tawi Zanzibar

MHE. SAID MUSSA ZUBEIR aliuliza:-

Ruzuku ya bilioni nne (4) ilitolewa na Rais ili kusaidia uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania na Benki hiyo imeshafunguliwa Jijini Dar es Salaam na kwamba uko uwezekano wa kuongeza bilioni mbili katika mwaka huu wa fedha:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kufungua Benki hii Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzanika na kuna wanawake wengi wajasiriamali?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mbunge wa Fuoni kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali imewezesha uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania. Aidha, benki hiyo yenye makao yake Makuu Jijini Dar es Salaam, inalo tawi moja tu lililopo katika mtaa wa Mkwepu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika mkutano wa Pili wa Bunge hili la Kumi, swali Namba 4, lililoulizwa na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, tarehe 8 Februari, 2011 ni kuwa, mipango ya baadaye ya Benki ya Wanawake Tanzania ni kufungua matawi mengine mikoani kwa awamu kadri mtaji wake unavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kumfahamisha Mheshimiwa Said Mussa Zubeir kuwa mchakato wa kufungua tawi la Benki huko Zanzibar umeanza na tayari uongozi wa

Benki umeshatembelea Zanzibar kwa madhumuni ya kupata jengo la benki kufanya shughuli zake kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi Zanzibar.

MHE. SAID MUSSA ZUBEIR: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake yanayoleta matumaini. Kwa kuwa tayari zilishatoka fedha za mwanzo kwa mwaka uliopita na Zanzibar haikufaidika na hivi sasa tuna matarajio ya kuongezwa nyingine.

(i) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akalithibitishia Bunge hili kwamba mchakato huu ambao umeanza tangu kipindi hicho mpaka leo, kutakuwa na matumaini mazuri ya kwamba zitakapotoka fedha za mara ya pili Zanzibar nayo itafaidika?

(ii) Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Muungano na Rais Kikwete ni Rais wa Muungano na ndiye aliyetoa fungu hilo na kuna matumaini ya kutoka nyingine tukimaliza bajeti hii ambazo zitakuwa ni sh bilioni 2.

Je, haoni kwamba kuna ulazima wa kuhakikisha kwamba angalau nusu ya hizi shilingi bilioni 2 zitakazotoka basi zinaelekea Zanzibar ili kuweza kuwasaidia akina mama kule Zanzibar?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinatolewa kwa Benki ya Wanawake wa Tanzania ambayo ni *Institution*. Kwa hiyo, tutakapofungua tawi Zanzibar ina maana na Zanzibar itanufaika. Lakini hakuna *financial institution* ya Benki ya Wanawake Zanzibar Kwa hiyo, tukifungua *branch automatically* Zanzibar itafaidika.

Mheshimiwa Spika, lakini nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ndiyo maana katika kuhakikisha kwamba tunauenzi Muungano na kwa sababu katika *international affairs* masuala ya kuwawezesha wanawake kiuchumi ni ya Muungano, tunawasilisha pamoja ripoti ndiyo maana badala ya kufungua tawi la benki katika mkoa wowote tumeamua tunaenda Zanzibar ili kuuenzi Muungano. Nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli sh bilioni 2 zimeishakuwa *allocated* katika Bajeti, Inshallah mambo yakiwa mazuri atatuona Zanzibar. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Watu wamevaa vilemba leo mnapendeza kweli, haya Mheshimiwa uliyesimama. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Naomba nimuulize Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo hili sio Zanzibar tu, wanawake wengi wa vijijini hawana taaluma wala ujasiriamali wa kufungua akaunti za benki vijijini na katika matawi mbalimbali.

Je, Benki hii ya Wanawake itahakikishwaje na Serikali kama inawezeshwa na ifike kwenye vijiji mbalimbali kufungua akaunti na matawi ili wanawake wengi wajasiriamali wafaidike?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Spika, sifa yetu kubwa ya Benki ya Wanawake wa Tanzania ukifananishwa na Benki nyingine ni ile *component* ya kutoa mafunzo kwa wajasiriamali Wanawake kabla hatujatoa mikopo. Ukifananisha na Benki nyingine wanatoa mikopo lakini hawatoi mafunzo.

Ni kweli tuna nia ya kufika vijijini lakini kwa kuanzia ndio maana tunafungua vitu tunaita vituo vya biashara, sio Matawi. Tunawafuata Wanawake walipo katika vijiji, tunawafundisha elimu ya ujasiriamali, tunawaambia ni jinsi gani unaweza ukafungua akaunti kabla hujapata mkopo. Kwa hiyo, ndio lengo letu kufikia Wanawake kama tulivyodhamiria.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Na. 114

Madhara ya Maji ya Mito Tigite

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE aliuliza:-

Uchafuzi wa maji ya Mto Tigite uliosababishwa na sumu ya mabaki ya taka za Mgodi wa Dhahabu wa *North Mara*, Nyamongo – Wilayani Tarime licha ya Tume ya Bunge kwenda kufanya uchunguzi na kuona ukweli wa jambo hilo ambalo lisababisha madhara makubwa kwa wananchi na hata mifugo yao lakini hakuna hatua zozote zaidi zilizochukuliwa:-

- (a) Je, kwa nini Serikali haijachukua hatua yoyote hadi sasa ya kuwalipa fidia wananchi walioathirika na maji hayo?
- (b) Je, ni hatua gani za makusudi zimechukuliwa na Serikali na wamiliki wa Mgodi wa *North Mara* za kudhibiti hali hiyo isitokee tena?
- (c) Je, wamiliki wa Mgodi wa *North Mara* wanafanya nini katika hali ya kuwapatia wananchi maji safi na salama ili wasiendelee kutumia maji ya mto huo ambayo sio salama?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, mwezi Mei mwaka 2009 Serikali ilipokea taarifa ya uchafuzi wa Mto Tigite kutokana na kuvuja kwa maji yenye tindikali toka Mgodi wa *North Mara*. Baada ya Serikali kuthibitisha juu ya tukio hilo hatua kadhaa zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ili kubaini athari za kiafaya kwa binadamu na mifugo zilizotokana na matumizi ya maji ya Mto Tigite. Tathmini hiyo haikuweza kuthibitisha bayana idadi ya watu na mifugo iliyopata athari za moja kwa moja kutokana na kutumia maji yenye tindikali kutoka Mgodini.

(b)Mheshimiwa Spika, ili kuzuia hali ya kuvuja kwa majitaka yenye kemikali kutokea tena, tarehe 1 Julai, 2009 Serikali ilitoa Amri ya Zuio (*Protection Order*) kwa Menejimenti ya Mgodi iliyotengua kibali cha kumwaga maji yanayotoka Mgodini kwenda kwenye Mto Tigite. Menejimenti imeanza mchakato wa kujenga mtambo wa kusafisha maji (*Water Treatment Plant*) yatokanayo na shughuli za uzalishaji Mgodini. Ofisi ya Bonde la Ziwa Victoria na Mgodi wanaendelea na Programu ya kupima ubora wa maji kwenye maeneo yaliyochaguliwa kila mwezi ikiwa ni hatua ya kudhibiti uchafuzi kwenye mto.

(c) Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya mgodi inashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kuchangia shughuli za Maendeleo ya Wilaya na kutoa huduma kwa jamii kwa mujibu wa mikataba ya uchimbaji wa madini. Kijiji cha Nyamongo kinapata huduma ya majisafi na salama kutoka katika skimu iliyojengwa na mgodi inayochukua maji kutoka Mto Mara. Ninaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ishirikiane na Menejimenti ya Mgodi ili kutafuta fedha za kutekeleza miradi ya kuchimba visima, kujenga mabwawa na malambo kama ilivyoainishwa kwenye tathmini ya vyanzo vya maji iliyofanywa na Wizara yangu katika vijiji tisa vinavyozunguka Mgodi.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo kwa kweli hayakidhi haja ya swali husika. Lakini naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Baraza la Mazingira ya Taifa (*NEMC*) lilituma wataalamu kwenda katika Mgodi wa *North Mara* Nyamongo kwa kufanya uchunguzi na wakachukua *sample* ya maji ya Mto Tigite na wakaahidi kwamba wangetoa matokeo ya uchunguzi baada ya mwaka mmoja. Lakini mpaka sasa hivi umeshapita mwaka mmoja na zaidi lakini hakuna matokeo yoyote ya uchunguzi yalishatolewa. Je, ni lini Baraza hili litatoa matokeo hayo.

Moja ya ahadi ambazo Mgodi na wawekezaji wengine waliahidi katika Wilaya ya Tarime ni kwamba watasaidia sana upatikanaji wa maji katika vijiji vya Kerende, Nyenkulu, Kewanja, Nyangoto, Matongo, na Kunguru Nyamwaga. Lakini hadi sasa utekelezaji wake ni *zero*. Je, Serikali inasema nini kuhusu ahadi hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwenye sehemu (a) swali lake lilitaka kujua Serikali itawalipa fidia kiasi gani na kwenye jibu langu nimesema kwamba kwa sababu hatujakua na tathmini inayoonyesha idadi ya watu ni wangapi na ni kiasi gani ile sumu imeingia kwa watu wale. Kwa hiyo, ni vigumu sana kuweza kujua kiasi gani cha fidia unaweza ukawapa watu na mifugo walioathirika na sumu ile.

Lakini hatua ambazo zimechukuliwa ni kwamba ile *protection order* imetolewa na kuhakikisha kwamba maji yale hayawezi kuvuja tena, yale mabwawa yametengenezewa *liners*. Kwa hiyo mwanzoni yalikuwa hayana *liners*. Kwa hiyo kule kuvuja tena hakupo.

Mheshimiwa Spika, (b) mpaka sasa hivi vijiji vinavyozunguka mgodi ule tayari vimeshachimbwa visima 8 na Serikali na pia wale watu wa mgodi wanatoa huduma ya maji safi katika baadhi ya vijijini ambavyo ni makubaliano ambayo waliyatoa wakati wanaingia kwenye eneo lile.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuzingatia kwamba Sheria ya Mazingira inazitaka Kampuni wakiwemo wachimbaji wa madini kufanya *enviromental impact assessment* kabla ya kuanza shughuli za uchimbaji. Je, tunaweza tukaletewa katika Bunge hili *enviromental impact assessment* iliyofanyika katika mgodi huo wa Nyamongo kabla ya kuanza uchimbaji wenywewe?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabla mgodi haujaanza ni lazima huwa inafanyika hiyo inayoitwa *enviromental impact assessment*. Na *impact assessment* hiyo ilifanywa na ni lazima ukifanye mara kwa mara ni ile *environmental audit* ambayo huwa inafanyika, kwa hiyo *data* hizo akitaka tutazileta.

Na. 115

Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Mbwasa

MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Makutupora wameibua mradi wa ujenzi wa Bwawa la Mbwasa kwenye kijiji cha Mbwasa kwa ajili ya kukidhi mahitaji maji binadamu na mifugo, mradi ambao wananchi wanautekeleza kwa nguvu zao wakisaidiwa na wafadhili:-

- (a) Je, Serikali inautambua mradi huo?
- (b) Kama Serikali inautambua. Je, iko tayari kuutengea fedha katika mwaka wa fedha ujao ili kuweza kuukamilisha mradi huo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. John Zefania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa bwawa la Mbwasa ulioibuliwa na wananchi wa Kata ya Makutupora unaendana na malengo ya Serikali ya Mpango wa Miaka 5 ya mwaka 2011/2012 mpaka 2015/16 unaolenga kujenga Mabwawa ya kuvuna maji kwa ajili ya kilimo cha Umwagiliaji katika mikoa kame hususan Dodoma, Singida, Tabora na Shinyanga.

Kwa kutambua hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imekwishauingiza mradi huo katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ya Manyoni (*DADPs*).

Katika mwaka wa 2011/2012 Halmashauri ya Wilaya imetenga shilingi milioni 25 kupitia “*Capital Development Grant*” na Mfuko wa *Tanzania/Japan Food Aid Counterpart Fund* tayari umetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya mradi huo. Hatua inayofuata ni kuuombea mradi huo fedha za ujenzi kutoka katika Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) kupitia Mifuko ya Maendeleo ya Umwagiliaji ya *DIDF* na *NIDF*.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoahidi tarehe 16 Juni, 2011 nilipotembelewa Ofisini kwangu na ujumbe toka Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ulioongozwa na Mhe. Capt. John Zefania Chiligati, (Mb.), Serikali itanza kutumia fedha zilizokwishaplikana kutekeleza mradi wa ujenzi wa bwawa la Mbwasa katika mwaka wa 2011/2012. Bwawa hilo linalokadiriwa kugharimu shilingi bilioni 1.2 litakapokamilika, litawanaufaisha wakulima katika skimu za umwagiliaji za Chikuyu (170 ha), Mtiwe (165 ha), Lisilile (150 ha) na Ngaiti ambazo hivi sasa zinalimwa mara moja tu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, nashinda kujizuia kumpongeza sana Mheshimiwa Chiligati kwa juhudni kubwa alizofanya kuibua mradi huu na juhudni anazozifanya kuendelea kuwaaletea maendeleo endelevu na hasa katika kilimo cha umwagiliaji maji mashambani wananchi wa Manyoni Mashariki.

MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa majibu ya kutia moyo aliyyoyatoa. Hata hivyo nina suala dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwamba ili mradi huu uanze kutekelezwa unahitajika ufanyiwe upembuzi yakinifu utakaogharimu karibu shilingi milioni 50 mpaka 70. Ni kweli kwamba Mfuko wa Pamoja wa Tanzania na Japan wametupatia shilingi milioni 200 tunashukuru.

Lakini wamesema hizo zisifanye kazi ya upembuzi yakinifu ziende kujenga mradi moja kwa moja. Kwa vile Halmashauri haina fedha hizi Mheshimiwa Naibu Waziri

atakubali kwamba atatuletea shilingi hizo za upembuzi yakinifu haraka haraka ili mradi uanze?

NAIBU WAZIRI WA MAJI:Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwanza niwashukuru *Tanzania/Japan Food Aid Counterpart Fund* kwa mchango wao wa shilingi milioni 200 na Halmashauri kwa kuchangia shilingi milioni 25. Sasa kwa sababu wafadhili hawa wameshatuonyesha kwa kuchangia shilingi milioni 200 huu upembuzi yakinifu ambao utahusisha hiyo *technical investigations* utafanywa na Serikali na fedha hizo zitatolewa kwa sababu tayari wafadhili wameshaweka fedha zao na sisi Serikali lazima tuonyeshe kwamba tuna nia ya kujenga. Kwa hiyo, fedha hizo zitatoka Serikalini.

MHE DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, kwa kwa mradi huu ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais alipokuwa kwenye Kampeni Chikuyu mwaka jana. Na kwa kuwa kwa juhudzi za Mbunge wananchi wamejitolea nguvu zao na Halmashauri imeunga mkono. Je, Serikali haiioni kwamba mradi huu una kila sababu ya kipaumbele ili uweze kutekelezeka haraka kuondoa kero ya wananchi na kuinua kilimo cha wananchi wa Chikuyu na Wilaya ya Manyoni kwa ujumla?

NAIBU WAZIRI WA MAJI:Mheshimiwa Spika, niongezee tena kusema kwamba ahadi yetu iko pale pale. Kwa kweli Mheshimiwa Rais alikwishaahidi na tumesema bwawa lile likikamilika hekta zitakazomwagiliwa ni 2,000 na zitaongezea kwa zile ambazo sasa hivi zinamwagiliwa mara moja tu. Kwa hiyo, nataka nisisitize tu kwamba tutatoa kipaumbele ndio maana nimesema katika msimu huu unaokuja nina hakika kabisa fedha za Serikali zitatengwa tumalize hiyo *technical investigations* na tuingie katika hatua ya pili ya ujenzi wa bwawa hilo.

Namwomba Mheshimiwa Dada yangu Diana Chilolo awe na amani kabisa mradi huu utatekelezeka. (*Makofii*)

Na. 116

Dawa Kutoka MSD

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Baadhi ya zahanati na Vituo vya Afya katika Jimbo la Manyovu, hazijaandikishwa hivyo hazipati dawa kutoka *MSD*:-

- (a) Je, Serikalli inasemaje juu ya Vituo vya Afya ambavyo havipati dawa za Serikali lakini vinastahili?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha hali hiyo ili wananchi wahudumiwe kwa kiwango kinachostahili?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kasulu ambayo Jimbo la Manyovu ni sehemu mojawapo ina zahanati 54 na vituo vya afya 6 vya Serikali, Zahanati na vituo vya afya hivyo, huwekewa fedha Bohari ya Dawa (*Medical Stores Depratment (MSD)*), ili kuviwezesha kununua dawa na vifaa tiba kulingana na mahitaji yake na mgao wa fedha. Vituo hivyo, vimefunguliwa akaunti Bohari ya Dawa na vinatakiwa kuagiza mahitaji yake kila baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Wizara ina taarifa ya zahanati moja iliyoko katika kijiji cha Mwanza ambacho zahanati hiyo ni mpya na itaanza kupata mgao wa dawa kutoka *MSD* kuanzia mwezi Julai, 2011. Naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri yake kuwasilisha Wizarani orodha ya vituo vya tiba yaani zahanati au vituo vya afya vingine kama viro ambavyo havipati dawa ili tuweze kufanya utaratibu wa kuviwekeea fedha za dawa *MSD*.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, kwanza nipongeze majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Nilikuwa nauliza maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni kiasi gani cha dawa ambacho zahanati inaweza kuagiza kwa mara moja?

Pili, kwa kuwa zahanati zetu zinatakiwa kuagiza kila baada ya miezi mitano (3) na muda mwingine wanaagiza wanakuta dawa zile hazipo *MSD*. Na kwa kuwa Kigoma ni mbali unakuta kwamba kila baada ya miezi 3 mpaka dawa zifike vituo vyetu havina dawa. Je, unaweza ukaruhusu Mkoa wa Kigoma ukawa unaagiza kila baada ya miezi mitano (5)? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba hivi vituo vya afya au zahanati wao wanaagiza dawa kila baada ya miezi 3 na idadi ya dawa inategemea mahitaji husika ya hicho kituo.

Swali la pili, swali lake nimeliona kama ombi nitaliangalia lakini tumejitayarisha *MSD* tumeongeza zoni kwamba tulikuwa na zoni 9 na tuna mpango wa kuongeza zoni na nafikiri mojawapo ya zoni itakuwa mko wa Kigoma tujenge bohari pale ili tuwasogezee huduma karibu zaidi. (*Makofî*)

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa MSD wanapeleka dawa kwenye zahanati na kwenye ziara yetu ya CHADEMA Operesheni Sangara imefika kwenye kituo cha Kasanga. Jimbo la Kalambo na nikashuhudia mwenyewe dawa zilizopelekwa na *MSD* pale ni maboksi karibu 10 yote ni kondomu na nilivyomwuliza Nesi akasema hawajaagiza hivyo. Je, Waziri anasema nini kuhusu *MSD* wanapeleka dawa kwenye zahanati ambazo hazijaagizwa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, hii ya leo kali.

Mheshimiwa Spika, ndio maana nikasema hii ya leo kali. Taarifa hizi kwa kweli zitakuwa za kusikitisha kama wameagiza dawa kwa mahitaji yao halafu wakaletewa kondomu tu lakini nafikiri hii pengine ni mojawapo ya mahitaji yao.

Lakini kilichotokea inawezekana wakati wanaagiza *MSD* walikuwa hawana dawa hiyo kwa wakati ule. Kwa hiyo, kilichokuwepo ndicho walicholetewa na ndicho hicho walichoagiza. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 117

Huduma ya Matibabu Kwa Wazee

MHE. MARGARET A. MKANGA aliuliza:-

Sera ya Wazee imeelekeza kuwapatia wazee matibabu bure lakini utekelezaji wa suala hilo umekuwa haueleweki na pia una urasimu mkubwa mahali pengi nchini:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa uhakika wa kuondoa kero na adha hii wanayopata wazee katika suala zima la matibabu yao?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magret Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Sera ya Wazee pamoja na Sera ya Afya kwa pamoja zinaelekeza makundi maalum wakiwemo wazee kupatiwa huduma za afya bila malipo. Aidha, ni kweli kwamba katika baadhi ya maeneo kumekuwa na usumbufu kwa wazee hao wakati wanapohitaji huduma hizo kwa sababu ya kigezo cha uwezo wa kiuchumi kama kilivyobainishwa kwenye Sera ya Afya.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia suala hili na kuondoa usumbufu na kero wanazozipata wananchi, Serikali kuitia Wizara ya Afya na ustawi wa jamii, ilipitia mwongozo wa uchangiaji wa huduma za afya mwaka 2009/2010 ambapo mapendekezo ya namna ya kuboresha huduma za afya, hasa kwa makundi maalum yaliyotolewa. Miiongi mwa mapendekezo yaliyotolewa katika mwongozo huo ni pamoja na kutoa huduma za afya bila malipo kwa wazee wote bila kujali kigezo cha uwezo kama sera ya

afya ya mwaka 2007 inavyoelekeza. Mwongozo huu kwa sasa unapitiwa na mamlaka nyingine za Serikali kwa ajili ya kuanza kutumika rasmi. Mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kupitia mwongozo huo yatatumika pia, kudurusu Sera ya Afya ya 2007.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuadhimisha Siku ya Wazee Mkoani Dodoma tarehe 1 Oktoba, 2009, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maagizo kwa watendaji wa Hospitali kutenga dirisha maalum kwa ajili ya kuwahudumia wazee ili kupunguza kero na usumbufu wanaoupata pindi wanapohitaji huduma za tiba. Hadi sasa Mikoa yote ya Tanzania Bara na katika baadhi ya Halmashauri tayari wamekwishaanza kutekeleza maagizo haya. Aidha, madirisha ya Bima ya Afya yanatumika kutoa huduma kwa wazee katika hospitali za Mkoa na Wilaya. Utekelezaji unatofautiana kulingana na upatikanaji wa fedha kwa kila Halmashauri. Wizara itaendelea kufuutilia na kuwahimiza watendaji mbalimbali kuhakikisha wanafuata maagizo na miongozo iliyopo kwa lengo la kupunguza kero na adha kwa wazee wanaohitaji tiba.

MHE. MARGARET A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri kiasi ya Mheshimiwa Waziri na kwamba amekiri utekelezaji unatofautiana kutegemeana na kutopatikana fedha. Lakini kuna kitu kingine. Je, Serikali inasema nini kwa watendaji ambao wanajitetea kwamba hatuwezi kutekeleza suala hili kwa sababu hatujapata maelekezo kimaandishi kutoka juu?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mkanga kwamba kama imetokea mmepata taarifa mtumishi huyu kwamba amepewa maelekezo kwa sera hizi ambazo tunesema tutaanza kuzitekeleza baada ya wadau wengine kuitia, mimi naomba unipe taarifa tuweze kuishughulikia ipasavyo. Wakati wengine nilikuwa naongea na wenzangu kwamba tumepewa majumuku makubwa ya kuhakikisha kwamba tunatoa huduma bora za afya za watanzania. Kwa hiyo lazima tuwajibike, kwa wale ambao hawawajibiki, maana hii inatoka ni suala la mtumishi mwenyewe binafsi, hawa Waheshimiwa Wabunge nawahakikishia tutawashughulikia. Wale ambao hawawapi haki zao hawa wazee huduma hizi ambazo kwenye sera tumezielekeza.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimwulize Mheshimiwa Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sera ya wazee inasema kuwapatia wazee matibabu bure. Lakini je, ni kwa ajili ya magonjwa ya aina fulani tu? mbona wanapotakiwa kufanyiwa upasuaji hutakiwa kutoa fedha jambo ambalo wazee wengi maisha yao ni duni na hawana uwezo wa kutoa fedha? Mheshimiwa Waziri anasemaje?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, sera hii haina ubaguzi ugonjwa gani. Ni magonjwa yote hawa wazee wanatakiwa watibiwe bure. Kwa hiyo, kama imetokea inawezekana kwa mazingira pengine hakuna dawa, lakini kama dawa mzee amelipishwa anatakiwa ile dawa kwa sababu haikuwepo kwenye kituo kile anatakiwa zile hela zirejeshwe. Hali kadhalika kama hii huduma ya opareshi imetokea ni makosa ya kiutendaji naomba taarifa mtuletee tutazishughulikia. (*Makofi*)

Huduma ya Mawasiliano ya Simu – Bungu

MHE. STEPHEN H. NGONYANI aliuliza:-

Tarafa ya Bungu ina shughuli nyingi za kiuchumi, kijamii na kibiashara na ina wananchi wengi lakini hakuna mawasiliano, hasa ya simu za mikononi:-

Je, ni lini maeneo hayo yatapatiwa huduma ya mawasiliano kwa kutaja maalum ambapo zoezi hilo litafanyika?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Stephen Ngonyani (a.k.a Profesa Maji Marefu), Mbunge wa Korogwe Vijiji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa sekta ya mawasiliano nchini umekuwa ukienda sambamba na kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi, kijamii na kibiashara katika maeneo mbalimbali nchini. Ni dhahiri kwamba ukuaji wa sekta hii umeweza kushuhudia mafanikio kadhaa ikiwemo kuendelea kushuka kwa gharama za huduma ya mawasiliano ya simu katika maeneo mbalimbali nchini.

Hata hivyo, ukuaji wa sekta ya mawasiliano katika baadhi ya maeneo nchini unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile idadi na kipato cha wananchi katika maeneo mbalimbali nchini kutowania na gharama kubwa za kuwekeza na kuendesha mitambo ya mawasiliano mbalimbali pamoja na uhaba wa miundombinu ya barabara na nishati ya kutosha yenye gharama nafuu kwa ajili ya kuendesha mitambo ya huduma za mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutambua changamoto zinazokabili ukuaji wa sekta ya mawasiliano, Serikali inashirikiana na makamapuni ya Simu nchini kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ili kuhakikisha kuwa ifikapo mwishoni mwa mwaka 2013 zaidi ya asilimia tisini (90%) ya Watanzania wote wawe wamefikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu ikiwemo Tarafa ya Bungu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge, wananchi wa Tarafa ya Bungu ambaa hivi karibuni wameshuhudia kampuni ya Airtel ikiweka na kuchambua mnara uliokuwepo ili uweze kuhudumia watu wengi zaidi pamoja watanzania wote kwa ujumla waweze kuwa na wavumilivu wakati juhudhi mbalimbali zikiendelea kufanyika ili kuondoa upungufu wa huduma za mawasiliano katika baadhi ya maeneo nchini. Vilevile napenda kuwashimiza wananchi wawe tayari kutoa ushirikiano wa kutosha kwa taasisi na

kampuni mbalimbali zenyе malengo ya kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo yao.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, asante sana. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri nakupokea simu zangu ahsante sana. Kwa kuwa tatizo la Tarafa ya Bungu linafanana kabisa na Kata ya Kizala pamoja na Kata ya Mkaramwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kuhakikisha sehemu hizo zinafanyiwa?

Je, kazi hiyo itaanza lini?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swalı langu la msingi Kizala na Mkaramwa ni maeneo yaliyoko katika Wilaya ya Korogwe. Kampuni ya *Airtel* ilipokuwa ikifanya utafiti na kuhakikisha kwamba ina uhamisha mnara uliopo katika Tarafa ya Bungu ili uweze kuhudumia watu wengi zaidi. Vilevile imepitia maeneo ya Kata ya Kizala na Mkaramwa ili kuhakikisha kwamba kata hizi vilevile zinafikiwa na mawasiliano. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ifikapo mwensi wa tisa kazi hii itakuwa imekamilika.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kuna tetesi kwamba minara ya simu inatoa mionzi ambayo ni hatari kwa afya za binadamu.

Je, Serikali inasemaje kuhusu jambo hilo? (*Makofī*)

SPIKA: Kwa hiyo, kuomba omba hapa ni hatari. Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, mionzi itokayo katika minara ya simu haina madhara. Kwa kisayansi kuna mionzi inayotofautiana. Kuna *Gamma-ray*, kwa wale waliosoma ni ile ambayo inahatarisha. Lakini mionzi hii ni ya mawasiliano ambayo *frequency* zake ni kidogo sana na hazina madhara sana ukiwa katika eneo fulani. Ila kama mtu atapanda na kukaa karibu na ule mnara kule juu kwa muda mrefu hapo ndipo inaweza ikasababisha madhara.

SPIKA: Kwa hiyo, tupo salama. Tunaendelea na swalı lingine la Mheshimiwa Said Juma Nkumba.

Na. 119

Tatizo la Mawasiliano ya Simu za Mkononi – Kiwere

MHE. SAID JUMA NKUMBA aliuliza:-

Wananchi wa Kata za Kipiri, Kitunda na Kiloli katika Tarafa ya Kiwere wana tatizo kubwa la mawasiliano ya simu za mkononi.

Je, Serikali ina mipango gani ya kuhakikisha maeneo yaliyotajwa yanapatiwa huduma hiyo ili kurahisisha mawasiliano yao kwa kuwa wako mbali na Makao Makuu ya Wilaya ya Sikonge.

NAIBU WAZIRI NA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kumekuwa na matatizo ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini zikiwemo Kata za Kipiri, Kitunda na Kiloli katika Taarifa ya Kiwere. (*Makofii*)

Napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali kuitia Wizara yangu tayari imekwishafanya upembuzi yakinifu kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ambapo maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge ni mionganini mwa maeneo zaidi ya mia mbili (200) yaliyoainishwa na Mfuko katika awamu ya kwanza kwa ajili ya kufikishwa huduma za mawasiliano, hivyo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa maeneo husika upatikanaji wa huduma za uhakika za mawasiliano katika kipindi kifupi kijacho.

Aidha, maeneo ya Kata za Kipiri, Kitunda na Kiloli yapo katika mpango wa kufanyiwa tathimini yakinifu na kampuni ya mawasiliano ya *Airtel* katika mwaka huu ili kuweza kufikisha mtandao wa mawasiliano ya simu za mkononi na hivyo na basi kusaidia wananchi wa maeneo hayo kuwa na mawasiliano.

MHE. SAID JUMA NKUMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru pamoja na majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa hapa. Nina maswali madogo ya nyongeza mawili.

Kwanza, kwa kuwa kazi ya tathmini yakinifu imeshafanyika katika maeneo yote matatu lakini eneo la kwanza la Kitunda ndilo ambalo kazi kwa kweli naiona inafanyika kwa sababu watu wa *Airtel* wameshafika pale mara mbili mara tatu hivi. Maeneo mengine haya bado. Sasa Waziri atakuwa tayari kusaidia ili msukumo wa uhakika ufanyike wa uhakika zaidi ili na maeneo yale mengine yaweze kufanyiwa upembuzi yakinifu kwa haraka zaidi?

Lakini la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri hapa ametoa ahadi kwamba muda si mrefu mwaka ujao wa fedha kazi hii itakuwa imekamilika na wananchi wanapata huduma hii, kazi hii itakuwa imekamilika na wananchi wanapata huduma hii ya mawasiliano katika Tarafa nzima ya Kiwere.

Sasa kwa sababu wananchi wangu wengine wanasikiliza redio, wengine hawaangalii luninga, wengine watakuwa na kazi zao binafsi, utakuwa tayari kuniruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri nikaitishe Mkutano wa hadhara niwaambie hii ahadi ili muda utakapokuwa umekamilika niweze kuwa pamoja na wewe kuhakikisha kwamba mambo haya yamekamilika ipasavyo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu la msingi maeneo haya yameshafanyiwa utafiti wa awali na maeneo haya si tu kwamba yatapata huduma hivi karibuni, Serikali yetu ni makini, ina mambo ambayo ina uhakika nayo.

Nimhakikishie tu kwamba katika kipindi ambacho nimemwahidi wananchi wa Kata alizozisema watapata mawasiliano na nimwombe aende akijidai kabisa akaitishe mkutano na kuwaeleza wananchi wa Jimbo lake. (*Makofi*)

MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza. Kwa kuwa hali ya Tarafa ya Bungu katika Jimbo la Korogwe Vijiji na na Tarafa ya Kiwere katika Jimbo la Sikonge, inafafanana kabisa na hali ya Tarafa ya Ndagaru katika Jimbo la Magu ambayo haijawahi kuona umeme toka Tanzania ipate uhuru.

Kampuni za Simu za *Airtel* na *Vodacom* zilikuja zikapita zikafanya *survey* na zikaainisha maeneo ya kuweka minara, nimefuatilia mpaka nikafika mahali nimechoka.

Mheshimiwa Waziri utanisaidia ili watu wa Ndaguru nao wafaidi matunda ya uhuru kwa kupata walau mawasiliano kwa kuzingatia kwamba hawana umeme tangu uhuru?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukieleza hapa mipango ya Serikali na kama alivyojibu kwa ufasaha kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ina mipango mingi mizuri mmoja wapo ni hii dhamira ya kusambaza umeme vijiji. Tumeanzisha Wakala wa Nishati Vijiji mahususi kwa ajili ya kushughulikia eneo hilo ili kuongeza kasi hiyo na tunavyoongea ninafahamu Mheshimiwa Dkt. Limbu na Mheshimiwa Ndasa, Mbunge wa Sumve wana miradi yao kama walivyo Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo mengine tunashughulikia kuititia utaratibu huo wa Wakala wa Nishati Vijiji.

Na. 120

Shirika la Ndege la ATC

MHE. MARIA I. HEWA aliuliza:-

Shirika la Ndege ATC linaonekana kusuasua sana kwa muda mrefu: Je, kwa nini hali hiyo iko hivyo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ndege ATC tangu lilipoanzishwa, kwa muda mwingi halikuwa na Menejimenti nzuri na hivyo kujikuta likiendeshwa bila tija. Pamoja na kuupo kwa usimamizi mbovu mwanzoni, maamuzi ya msingi kama vile nauzi ilibidi yaidhinishwe na Serikali, hivyo basi kuchelewesha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali isiyoridhisha ya uendeshaji wa Shirika, Serikali ilibidi kubinafsisha Shirika la Ndege, Mwezi Novemba, 2002, kwa kuuza asilimia 49 ya hisa zake kwa Shirika la Ndege la Afrika Kusini (SAA) na kuunda Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL). Hata hivyo, utendaji bado uliendelea kuwa wa kusuasua, kwani mwekezaji naye hakuwa mbunifu katika kuiendesha kampuni kwa ufanisi. Badala yake aliipunguzia kampuni hata ule uwezo iliyokuwa nao ATC wa matengenezo ya ndege na ukusanyaji wa mapato yake kupitia IATA na yote haya yakawa yanafanywa na SAA.

Kutokana na hali hiyo, ubia kati ya ATCL na SAA ulisitishwa mwezi Agosti, 2006 na ilipofika Februari, 2007, kampuni ikakabidhiwa kwa Bodi na Menejimenti ya Watanzania kuisimamia na kuiendesha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, huduma za ATCL ziliendelea kudorora kutokana na utendaji mbovu wa Bodi na Menejimenti ya Kampuni na hivyo kampuni kuendelea kusuasua hadi kushindwa kutoa huduma kabisa tangu tarehe 10 Februari, 2011.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniruhusu niulize maswali mafupi ya nyongeza.

- (a) Kwa vile Serikali inakiri kwamba Shirika hili limesuasua, je, wana maandalizi yepi sasa ya kuweza kulifufua tena ili Shirika hili liwe hai?
- (b) Baada ya kusuasua hivyo na SAA likabebwa na Wazalendo nao ndiyo wamelimaliza kabisa; je, Serikali imechukua hatua gani ili kitendo hiki kisije kikarudiwa tena? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, baada ya Shirika la Ndege kushindwa kutoa huduma kabisa tangu tarehe 10 Februari, 2011, tunachofanya sasa kurudisha huduma hizo kufuatia sababu ambazo zilifanya Shirika lisitoe huduma hizo ikiwa ni kupeleka ndege kwenye matengenezo ambazo hazijarudi, Serikali imelipia ndege ambayo iko *South Africa* ili irudi. Ndege hiyo iko katika matengenezo ya mwisho na itakapofika mwisho wa mwezi Julai, ndege hiyo itakuwa ipo hapa nchini ili huduma

zirudi tena. Pia Serikali inapanga kupeleka ndege ya pili ya *Dash Aid* kwenye matengenezo

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo kwenye wakati wa kutafuta Menejimenti mpya ya kuendesha Shirika hilo sambamba na Bodi mpya ya kuendesha Shirika hilo. Tutakachofanya ni kuwapatia hizo ndege mbili za kuanzia na kuwapatia mtaji (*working capital*) ya kuendeshea ndege hizo, pamoja na kubadilisha mfumo mzima uliokuwa unaendelea hapa kwa kuwa Shirika ni lazima lilipiwe gharama za uendeshaji wa Serikali ikiwemo mishahara, utengenezaji wa ndege kama hivi ambavyo tumesema, zikiwemo bima za ndege, Shirika lipewe vitendea kazi na lipewe mitaji ya kujiendeshea.

Mheshimiwa Spika, wakati tunafanya hivi, sambamba na hiyo, bado tupo katika harakati za kutafuta wabia wa uhakika watakothibitika ili tuingie nao pamoja katika kuendesha Shirika hilo la Ndege.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda pia umekwisha. Kwanza, ninayo matangazo ya wageni waliopo hapa Bungeni. Tunao Wakuu wa Mikoa 17 kama tulivyo eleza jana na Makatibu Tawala wa Mikoa 21, wapo kwa ajili ya kusikiliza Hotuba ya Waziri Mkuu. Hawa Wakati wote watacaa katika nafasi ya *Speaker's Gallery*, ndiyo hao waliopo hapo, nisingependa kumtaja mmoja mmoja lakini kama mnawajua Wakuu wenu wa Mikoa, kawasalimieni mkitoka hapa.

Tunao wanafunzi 40 wa Shule ya Msingi ya Mwongozo iliyopo Mwananyamala, Jimbo la Kinondoni, wakiongozwa na Mwalimu wao anaitwa Herry Shuma, ninaomba wasimame kama wapo ndani.

MBUNGE FULANI: Ni Walimu.

SPIKA: Aah ni Walimu, ahsanteni sana Walimu. Tunawashukuru mmekuja kutuangalia. Tunao pia Wanafunzi kumi na mbili na Walimu watatu wa *Mama Clementina Foundation Kilimanjaro Academy* kutoka Moshi; wako wapi? Ahsante tunafurahi kuwaoneni, someni kwa bidii.

Tunao Wanafunzi hamsini na Walimu kumi wa Shule ya Msingi Bunge kutoka Dar es Salaam na wao wasimame pale walipo, ahsante sana, karibuni. Hii ni shule ambayo iko karibu na Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Mheshimiwa Danhi Makanga, Mkuu wa Wilaya ya Kibondo na alikuwa Mbunge wa zamani; karibu sana. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo ya kazi; Katibu wa Kamati ya Waheshimiwa Wabunge wa CCM, aninaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati, Siku ya Jumamosi, tarehe 25, saa nane mchana, katika Ukumbi Namba 118, Jengo la Utawala; hivyo, Wajumbe wa Kamati hiyo ya Uongozi wahudhurie kikao hiki.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa Wabunge wa CCM, aninaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati, Tarehe 26, saa nane mchana katika Ukumbi wa Msekwa. Wajumbe wote wa Kamati hiyo, wanaombwa wahudhurie bila kukosa. Kamati ya Uongozi ni tarehe 25, saa nane na wote ni tarehe 26 saa nane.

Waheshimiwa Wabunge, ninapenda kuwatangazia kwamba, kesho tarehe 25, Siku ya Jumamosi, kutakuwa na Semina ya Masuala ya Uongozi, itakayotolewa na *Uongozi Institute* katika Ukumbi wa Msekwa, kuanzia saa nne asubuhi. Mtakumbuka kwamba, hii *Institute* imezinduliwa hivi karibuni, kwa hiyo, kutakuwa na semina kuhusu mambo ya Uongozi; Wabunge wote mnakaribishwa saa nne asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa.

Siku ya Jumapili pia tarehe 26, kutakuwa na semina kuhusu Sekta ya Nishati na Madini katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa nne na nusu asubuhi. Kwa hiyo, Siku ya Jumapili ni semina kuhusu Sekta ya Nishati na madini, saa nne na nusu asubuhi na kesho Jumamosi kuna semina ya Mambo ya Uongozi. Ninaomba Wabunge mhudhurie hizo semina ni sehemu ya masomo ambayo inafaa myapate.

Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Fedha, imewasilisha masahihisho kwenye Kitabu cha Tatu cha *Estimates of Public Expenditure, Supply Vote Regional*, tuninaomba tuzigawe kwa Wabunge wote. Kuanzia tarehe 29 mtavitumia vitabu hivi, vipo vile vyta Wizara, vipo vyta Maendeleo na hii *Volume III*; muwe navyo hapa ndani muweke kwenye viti vyenu, kwa sababu tutavitumia sana. Siyo vizuri unakaa hapa unasema ndiyo wakati hukijui unachokisema.

Waheshimiwa Wabunge, tutavitumia vitabu hivi kwa kipindi chote, kwa hiyo, muwe navyo hapa.

Waheshimiwa Wabunge, ninapenda pia kutangaza kwamba, ile tafrija tuliyotangaza ya Balozi wa Canada, ninaomba Waheshimiwa Wabunge mjitahidi kuja, tutaifanyia VETA, kwa hiyo ni mlango wa nyuma hapa mnatembea tu kwa miguu. Saa mbili kasorobo usiku baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge, mnakaribishwa kwenda kule. Kwa misingi hiyo hiyo, Wakuu wa Mikoa na Ma-RAS mliopo, ninaomba pia mshiriki katika Siku hiyo ya Taifa ya Canada, mnakaribishwa kwa sababu mpo ninaomba mhudhurie kama nafasi itawaruhusu.

Waheshimiwa Wabunge, ukiangalia hizi karatasi zote hapa sijui ngapi nilizonazo, kila mtu aninaomba nimsaidie kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu, huu siyo utaratibu. Utaratibu wetu, tumeshabandika majina pale, kwa hiyo, Mwenyekiti ye yeyote anayekaa hapa atakapomchukua mtu wa 130 akamuweka kuwa wa pili, tutazua mtifaruku ndani ya Bunge hili. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, mkubali kwamba, kama mlichelewa kuomba ndiyo umechelewa na mimi ningependa kuwashawishi kama kweli mnataka ninyi wote mwongee, basi tupunguze muda iwe dakika kumi, kwa sababu kwa dakika kumi na tano kwa siku tatu ...

(Hapa Wabunge fulani walipiga kelele)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mimi sijawaomba mseme, ninataka kuwaambia kwamba, ninaomba tufuate utaratibu, orodha hii itafuatwa hivi hivi, kwa sababu tukibadilisha hapa itakuwa tatizo. Kweli wengine mnasafari, ndiyo hivyo kama unasafiri wewe nenda tu hutazungumza, umependa kusafiri hutaweza kuzungumza. Kwa hiyo, ninaomba kabisa hii orodha ifuatwe kama ilivyo wala msimwandikie Mwenyekiti awapendelee hataweza kufanya hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba sana hili lizingatiwe.

Waheshimiwa Wabunge, jambo la pili, ninadhani tulikosea wakati tunaanza shughuli ya kuchangia, tulikosea kuwaambia ni lini uninaomba kuchangia, kuna wengine hapa waliomba hata kabla Hotuba ya Bajeti haijasomwa tayari waliomba kwa Waziri Mkuu. Utaratibu wetu ni kwamba, kwa mfano, tutakapokuja Wizara inayofuata watawasilisha Randama siku moja kabla ya kusoma hotuba, wakiwasilisha ile Randama ndiyo mnaanza kuomba kuchangia.

Ombeni kwa fomu, msiombe kwa barua, mkiomba kwa fomu tunajua nani alianza na nani anafuatia. Ninawaombeni sana mwombe kwa fomu kwa Katibu na mninaomba siku moja kabla, siyo siku tano kabla, watapoteza zile karatasi kwa sababu hatuna utaratibu wa *computerisation*.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba muwe wavumilivu na wale walioomba tutafuata utaratibu huo, kama una dharura bahati mbaya itabidi uende tu, ukifikiwa bahati yako, usipofikiwa bahati mbaya.

Kwa kila siku asubuhi tunakuwa na wachangiaji 17 na jioni wachangiaji 10, kwa hiyo, kwa siku moja tunakuwa wachangiaji 27 tu. Asubuhi ya leo watakaoanza kuchangia ni Mhehimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mheshimiwa Ismail Rage, Mheshimiwa Ally Juma Haji na wengine tutaendelea kuwataja baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, nina wageni ofisini, kwa hiyo, ninamwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, anipokee.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester M. Mabumba) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu kwa hatua inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Ofisi ya Waziri Mkuu
na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Tunaendelea na majadiliano ya Hotuba ya Waziri Mkuu, kama tulivyotangaziwa hivi punde, tutaanza na Mheshimiwa Edward Lowassa.

MHE. EDWARD N. LOWASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia asubuhi hii. Kwanza na mimi nimpongeze Spika, kwa kuchaguliwa na Bunge hili kuwa Spika wetu; ninampongeza sana. Pili, ninaomba nimpongeze Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa na kuthibitishwa kwa kishindo na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ninawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri, kwa heshima mliyopewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, mlioshinda katika viti vyenu; hongereni sana; ninawatachia kheri na kuwaombea kipindi cha miaka mitano na vinavyofuata mchaguliwe vilevile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuwashukuru Wananchi wa Monduli, kwa mara ya nne kwa kunipa heshima kubwa ya kuja katika Bunge hili. Nilipita kwa asilimia 94, tukawa wane; wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Assumpter Mshama, Jimbo la Nkenge; nampongeza sana; Mheshimiwa Shabiby, Jimbo la Gairo, alikuwa wa pili; na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Jimbo la Kilindi, alikuwa wa tatu. Ninawashukuru sana, kwa sababu hata Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Monduli walimpa asilimia 90. Ninawashukuru sana kwa heshima waliyonipa, ninapenda kuwaahidi kwamba, nitawapa utumishi uliotukuka, ndiyo shukrani yangu kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Jimbo langu lilipata njaa kubwa sana, mifugo ilikufa na hakuna kilichoota. Rais aliahidi kwamba, hakuna Mtanzania atakayekufa kwa njaa, nimesimama kuishukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali yote, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Ninawashukuru na kuwapongeza kwa dhati kwa jinsi walivyoshughulikia maafa yale, hakuna Mtanzania aliyekufa kwa njaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika kuwaambia kwamba, mwaka huu tena njaa inaendelea, hakuna mvua hata tone moja, ninawaomba kama walivyokuwa makini na mahiri mwaka jana na mwaka huu vilevile wawe makini na mahiri. Niombe la pili kwamba, pengine ni vizuri Serikali ikatusaidia kupima tabianchi, nini kinatokea katika mazingira yale, inawezekana mvua hazitakuja tena ili kama ni kuhama Wananchi wahame. Serikali isikae kimya tu, iangalie *beyond this*, ni nini maana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaipongeza Hotuba nzuri sana na majedwali yale ni mazuri sana. Nisameheni mimi ninaona kama Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa kubwa mno, Muundo ule ni mkubwa sana; kuna Maafa, Uratibu, Bunge, sasa Uwekezaji na Uwezeshaji iko pale na TAMISEMI iko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ndiyo kila kitu katika nchi hii, hospitali zote ziko pale, shule zote za msingi zipo pale, shule zote za sekondari zipo pale, ni dubwasha moja kubwa sana. Mimi ninawashauri watafakari, kama kuendelea na muundo

huo kutampa nafasi Waziri Mkuu, kufanya kazi zake za *coordination* na usimamizi kwa makini zaidi kama watapunguza Wizara hiyo wakaifanya ikawa *separate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema ni vizuri ikawa yenyewe kwa sababu ilivyo, inakuwa na urasimu mkubwa sana wa kufanya maamuzi. Monduli tulipata tatizo la maji, tukakatiwa umeme kwa wiki tatu, kulifanya jalada lihame kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu pale lishughulikie maji yetu, imetuchukua wiki tatu. Muundo ule haufai, ninapendekeza utazamwe upya ili Muundo huu wa TAMISEMI uachiwe ufanye kazi zake vizuri zaidi na uwajibike kwa watu vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile kwa suala la maji Monduli, hatuwezi kulipia gharama ya maji yale, tuninaomba kama wanavyofanyiwa Handeni, Maswa, Chalinze, Makondeko na Monduli, iwe katika orodha hiyo ili waweze kushughulikia suala la maji, inapopata bili za maji ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili ni miaka 50 ya Uhuru wa Nchi yetu. Miaka 50 ya Uhuru wa Nchi yetu ni Historia ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yake. Miaka 50 hii ni miaka ya Uongozi wa CCM, chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Chini ya Mzee Ali Hassan Mwinyi, chini ya Mzee Benjamin William Mkapa na Chini ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Yamefanyika mengi ambayo siyo vizuri yakabezwa. (*Makofi*)

Kwanza, ninawashukuru sana *TBC*, kwa vipindi wanavyotoa kutukumbusha historia ile; ni vizuri sana, ninawapongeza. Ingefaa kama taasisi zingine za nchi hii zingefanya hivyo, kutukumbusha historia hii; ni historia ya maana sana. Wapo watu wanaothubutu kubeza historia hii, tusiwakubalie. Nitaeleza sababu za kutowakubalia. (*Makofi*)

Kwanza, imekuwa miaka kumi ya Uhuru wa Nchi yetu, Mwalimu alisema: "Akija mtu jeuri na fedhuli akikuuliza Tanzania mna nini mjibu kwa uungwana tuna amani." Nchi hii ina amani, dunia inajua na Watanzania wanajua. Katika jukwaa la amani ndiyo maana tumeshikiri katika Ukombozi wa Bara la Afrika, Watanzania wanajua na dunia inajua. Kwa amani hii, ndiyo maana tulijenga Reli ya TAZARA kwa kuthubutu kati ya Tanzania na Zambia; Watanzania wanajua na dunia inajua. Ndiyo maana tumejenga Shule za Msingi asilimia 95 ya Watanzania wanakwenda shulen; Tanzania inajua na Dunia inajua. Tumejenga Shule za Sekondari kwa kila Kata ya Tanzania; Watanzania wanajua na Dunia inajua. Tumevuta maji ya *Lake Victoria* kutoka Mtera mpaka Shinyanga na yanaweza kwenda Nziga mpaka Tabora; Watanzania wanajua na Dunia inajua. Tumejenga kilomita za lami nyingi karibu sehemu kubwa ya nchi yetu, Watanzania wanajua na Dunia inajua. Tumejenga Chuo Kikuu Bora Kikubwa *Sub Saharan Africa, UDOM*, Watanzania wanajua na Dunia. (*Makofi*)

Mheshiimwa Mwenyekiti, unawezaje kuidhoofisha leo historia hii; na unawezaje kukiondoa Chama cha Mapinduzi katika historia hii? Tuna uchumi unaokua kwa asilimia saba, mzuri kuliko nchi nyingi Duniani; Watanzania wanajua na Dunia inajua. Huu ni

ushindi mkubwa kwa Chama cha Mapinduzi. Kinara na Waasisi wa mambo hayo ni Chama cha Mapinduzi, wala tusiogope ni historia nzuri sana. (*Makofi*)

Ninawaomba, kama walivyothubutu Viongozi waliotutangulia na sisi tuendelee kuthubutu, ndiyo heshima ya Chama cha Mapinduzi. Eneo moja ninawaomba tuthubutu kujenga upya Reli ya Kati kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma na Mwanza. Wala tusiogope, tukinuia tunaweza, tuijenge Reli hiyo ili ifungue nchi yetu upande wa Magharibi. Tuna biashara kubwa sana, *transit trade*, ambayo tukiisimamia vizuri kwa kujenga Reli ya Kati mpya, tutafanya vizuri sana katika uchumi wetu; tusiogope. (*Makofi*)

Tujenge upya Bandari ya Mtwara, tujenge upya Bandari ya Tanga, tujenge upya kwa ku-modernize Bandari ya Dar es Salaam, tunaweza. Viongozi waliotutangulia walithubutu na sisi tuthubutu tunaweza. (*Makofi*)

Ndugu zangu, nitauliza fedha zitatoka wapi? Fedha tunazo; *UDOM* hapa tumejenga kwa hela zetu karibu trilioni moja; tutakosa hela za kujenga reli? Vilevile katika *Private Sector Partnership* tunaweza tukaitangaza Reli hii tukapata watu wa kuja kujenga. (*Makofi*)

Tumepata *gas* nyingi sana kule Mtwara, huenda tukawa watu wa pili duniani kwa kuwa na *gas* nyingi. Tunaweza kutumia *gas* hiyo kwa kukopa. *Gas reserve* tukakopa tukapata fedha za kujenga reli hiyo na tukajenga bandari zote tatu; lazima tufanye sasa. (*Makofi*)

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mambo haya makubwa yametupa heshima Duniani na yametupa mshikamano na amani katika nchi yetu. Lazima tuendelee kujenga matumaini hayo. Uchumi wetu unakua kwa asilimia saba; ni vizuri sana. Lazima tufikishe mahali uchumi ule utafsirike vijijini, watu waone matumbo yao yamekuwa bora. Njia pekee ya kutafsiri mambo haya ni kama uchumi unafanya vizuri, tusiogope kukopa. Wale wanaofatilia Siasa za Kimataifa, Jumatatu iliyopita Wamarekani walianza *debate*, *Republicans*, juu ya uchaguzi wao. Hoja moja wanayoizungumza ni ajira, ni uchumi, lakini wakaja na jambo jipya kwamba, lazima kiwango cha kukopa Serikali, lile Deni la Taifa liongezwe. Kama Marekani anaongeza Deni la Taifa; sisi Watanzania ni nani tusiongeze Deni la Taifa? Tuongeze Deni la Taifa ili tuweze kukidhi mahitaji ya sasa. Mimi ninasema nchi yetu ni nzuri, tunaweza kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kurudia kusema, Chama cha Mapinduzi na Serikali yake, kimefanya kazi nzuri sana. Kimefanya kazi hii kwa kuthubutu, tuendelee kuthubutu. Kuna ugonjwa unaoingia wa kuogopa kutoa maamuzi, tutoe maamuzi. Heri ukosee kwenye kutoa maamuzi kuliko kutotoa maamuzi. Toeni maamuzi, achani kuogopa, tumepewa nchi fanyeni maamuzi. Heri uhukumiwe kwa kutoa uamuzi kuliko kwa kutotoa uamuzi, toeni maamuzi. Ninasema tukinuia na kuamua, tunaweza kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ninakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii, nikushukuru sana kwa kuniruhusu kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza, ninaomba nichukue nafasi hii, kukipongeza sana Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Samahani, Waheshimiwa Wabunge, ninaomba utulivu ndani ya Bunge.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Ninaomba nkipongeza sana Chama cha Mapinduzi kwa kuzingatia na kuhakikisha kinatekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa maslahi ya Watanzania wote bila kujali itikadi za vyama, dini, ukabila wala kitu kingine chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimkumbuke babu yangu mmoja, siku moja alinieleza kitu, huyu babu yangu alikuwa ni mtu mtaratibu sana. Alikuwa kila jioni lazima awe na kibuyu chake cha pombe kwa ajili ya kujiliwaza. Kuna siku moja wakati tunacheza mpira tukakisukuma kibuyu cha pombe tukamwaga pombe, siku hiyo ndipo tulipogundua yule babu kumbe ukimwingilia katika mambo yake ni mkali kuliko hata nyuki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niiambie Serikali ifanane na yule babu yangu, iwe makini na itakapoingiliwa katika mipango ya kuwasaidia Watanzania kujikomboa na umaskini walionao Serikali iwe makini, iwe kali na iamue kusimamia mambo hayo kwa uthabiti mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia ninafanana na yule babu yangu, leo wewe ukiniambia kwamba hakuna maendeleo kwenye Jimbo la Peramiho, nitakukasirikia kwa nguvu zangu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni nani ambaye alikuwa hajui katika miaka mingi toka tumepata Uhuru, Serikali ilikuwa haijajenga daraja la kuunganisha nchi ya Msumbiji na Mkoa wa Ruvuma kupitia Kijiji cha Mkenda? Daraja lile leo limejengwa na baada ya kujengwa Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wananzaika sana na biashara nje ya mpaka wa Mkoa kwa kupitia daraja hilo. Hivi ni nani haoni katika Jimbo la Peramiho barabara kupitia Mradi wa MCC inajengwa kutoka Songea, Peramiho kwenda Mbanga kwa kiwango cha lami na Wananchi wote wameshalipwa fidia zao? Hayo siyo maendeleo makubwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni nani haoni katika Jimbo la Peramiho kwa takriban miaka 20 kulikuwa na sekondari tatu tu, leo lina shule za sekondari 26, zile tatu zilizoanza mwanzo; sekondari mbili sasa hivi ni kidato cha nne na cha tano; nani halioni hilo suala na akasema kwamba hakuna maendeleo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni nani asiyeona kwamba sasa Hospitali ya Peramiho inapandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa na kuwasaidia Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na Jimbo zima la Peramiho, kuondokana na kero ya kusafiri kwenda kutibiwa Muhimbili katika magonjwa makubwa wakaendelea kutibiwa pale katika Mkoa wa Ruvuma kupitia hospitali hii? Nani atabeza kwamba siyo maendeleo makubwa katika Jimbo la Peramiho? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ninaomba kusema katika mambo ambayo ni ya ukweli lazima tukubali. Leo hii kuna mradi mkubwa sana wa umeme wa gridi kutoka Makambako kwenda Mkoa wa Ruvuma, umeme ule utavifaidisha vijiji vyote vilivyoko barabara kuu kuanzia Wino, Mahanje, Madaba, Gumbilo mpaka kufika Mji wa Songea. Umeme ule umeshafika katika Mji Mdogo wa Peramiho. Nani halioni hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwa kweli mtu akimwaga pombe yangu kwa kusema katika Jimbo la Peramiho hakuna maendeleo tutagombana. Nani asiyeona mafanikio makubwa ya ruzuku ya pembejeo ambayo imewakomboa wakulima wangu wakubwa katika Jimbo la Peramiho? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Peramiho ndilo linaloongoza kwa kilimo cha mahindi, mazao yote ya chakula ukisema *big four* katika Mkoa wa Ruvuma, Peramiho tunaongoza. Serikali imetuletea pembejeo za kutosha na ninaomba niiombe iongeze pembejeo hizo, ihakikishe magunia safari hii yanafika kwa wakati na ihakikishe fedha za kununua mahindi zinapatikana kwa haraka. Ninawaambia Serikali yangu kwa kazi hiyo mliyofanya hakika Wananchi wa Jimbo la Peramiho wanawashukuru na wanaomba mwendeleze moyo huo. Nani leo atakuja amwage pombe yangu ili Wananchi wangu wasipate pembejeo tena, wasipate magunia na wasinunuliwe mazao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikwambie kwamba, hayo yote ni mafanikio makubwa. Tunazo nafasi za kujifunza ili tuweze kwenda mbele zaidi. Hakuna mtu anayevaa suruali miguu miwili kwa wakati mmoja, hayupo. Lazima uanze kuyashughulikia matatizo kwa namna yake kwa upande mmoja na uingilie yale yaliyobakia. Ninaamini bado zipo kero nyngi kwa Watanzania, lakini ni lazima tukubali yaliyotekeliza ni msingi mzuri wa kutupeleka mbele tunakokwenda. (*Makofi*)

Mimi ninajua tunapata shida sana ya kukamilisha miradi ya barabara vijijini, kwa mfano, zile barabara zangu kwenye vijiji kama vile vya kule Muhukulu, Mawezo na Ifinga, Halmashauri haina uwezo. Sasa Serikali ikishazigundua barabara za namna hiyo, kwa kuwa tumetekeliza yale yaliyopita ni nafasi nzuri ya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kujipanga na kuyatekeleza hayo ambayo yamebakia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo sisi wote tunajua ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili. Asilimia 70 ya Watanzania wapo vijijini, hakuna asiyelijua hili. Kwa kuwa asilimia kubwa ya wakulima wapo vijijini, ninadhani ni nafasi tu nyngine nzuri sana kupitia Serikali za Mitaa, lakini kupitia mipango mizuri na mpango ulioainishwa na Serikali yetu kuhakikisha kwamba, maendeleo sasa yanawafikia Wananchi kule vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Edward Lowassa, amezungumza kitu kikubwa sana hapa, uchumi wetu unakua na amesema uchumi huu kama utaendelea kukua, Serikali itusaidie unapokua ujihusishe na hali halisi ya maendeleo ya kipato kwa Wananchi wa chini, ambao ni walalahoi walioko vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kushauri kwenye Serikali yetu ukiacha kuhangainia uendelezaji wa viwanda na uwekezaji katika mambo mengine makubwa, yupo mtaalam mmoja amesema siyo neno sana kuangalia Sekta ya Viwanda kama ni Sekta Kiongozi. Ukianza na viwanda vidogo vidogo utawasaidia walalahoi wengi kuinuka kiuchumi. Ninasema hivyo kwa kuwa viwanda vingi vikubwa sasa hivi vinajikita katika kutengeneza bidhaa ambazo Wazungu wanasesma ni *luxury*. Bidhaa ambazo ni *luxury* haziwezi kusaidia kuchochea maendeleo ya kipato ya Wananchi wa chini. Ukiwekeza katika kilimo kwa bidhaa zinazotokana na kilimo, hakika ninakwambia huu umaskini wa kipato utaondoka tu. (*Makofi*)

Sasa hayo ni mambo ambayo yamezungumzwa kwenye mpango na mimi niseme kwamba ni nafasi kubwa kwa Serikali yetu kuhakikisha inaangalia umuhimu wa vipaumbele hivyo ili kusaidia kuwakomboa Wananchi wetu kule vijiji. Tuwasaidie kwa nguvu zetu zote, tuwasaidie kwa moyo wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijamaliza kuzungumzia eneo hilo, ninaomba niseme ni kweli lipo tatizo la kimsingi kabisa. Kila mwaka Serikali yetu imekuwa ikipokea fedha nyingi na kuzipeleka katika kuleta maendeleo kule vijiji. Ukiachilia mbali Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, ninadhani lipo tatizo kwa mfano, mwaka huu tutapeleka shilingi zisizopungua bilioni 7.8 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwenye Serikali za Mitaa. Miradi hii inatakiwa sasa tutazame fedha zinazokwenda Wananchi wanazikamata kwenye vidole na kuangalia maendeleo yao yanabadilika, hapo kuna tatizo la msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siri, lipo tatizo la ugonjwa wa kujituma kwa nguvu na kusimamia maendeleo haya ipasavyo kwa watendaji na watumishi ingawa siyo wote, lakini wengi katika Serikali yetu. Ninaomba tukubali wote sasa ni Watanzania, tuumie jamani na maendeleo ya nchi yetu. Haipati picha fedha nyingi zinazoletwa na Serikali kwa maendeleo ya Watanzania halafu Watanzania bado waendelee kulalamika hawana maendeleo; ni sawa na kuweka mfuko wa kusagia unga, mahindi yanapoingia mfuko unatuna lakini unga ukishashuka mfuko unabaki hauna kitu tena. Kwa hiyo, lazima tuliangalie hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kuishukuru sana Serikali kwa kukubali sasa Madaba itaingizwa kwenye mchakato na kupatiwa kuwa Mji Mdogo. Ninaishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha na kujenga Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea pale Peramiho. Niombe kwa Serikali sasa hivi kumekuwa na zoezi la kufunga vituo vya afya na hospitali zisizokidhi. Madhara yanayopatikana ni makubwa, ingawa nia njema ya Serikali ipo ya kuhakikisha vituo vile vinafanya kazi bora.

Kwa zile hospitali na vituo vinavyosimamiwa na Serikali, hebu tujiulize; tumeviwezesha vikawa katika hali nzuri? Ninamwomba Waziri wa Afya kupitia TAMISEMI anisaidie kufungua Kituo cha Afya Madaba, ni kituo kinachohudumia karibu vijiji 20, akinamama wajawazito leo wanapata shida kubwa sana, fedha na uwezo wa Halmashauri kikitengeneza kituo kile kiwe katika hali inayotakiwa uwezo ni mdogo. Ninaomba Serikali ilitazame hilo. Leo kama kuna akinamama watataka kujifungua, siwezi kuelewa itakuwaje. Itakuwa ni hatari kubwa. Sasa kama wajibu wetu ni sisi Serikali kuhakikisha mazingira yanakuwa safi, inakuwaje mpaka tunavifunga vituo hivyo? Siku zote tulikuwa wapi kuvitazama ubora wake na kuhakikisha vinaendelea kuwa viro katika hali salama? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Waziri wa Afya kupitia TAMISEMI, ninaona ananisikia, toka juzi tunajadiliana suala hili, ninamshukuru ameanza kunipa ushirikiano. Hakika kituo kile kisipofunguliwa, maafa makubwa yatatokea. Ninaomba sana Serikali inisikie katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninawashukuru sana Wananchi wangu wa Jimbo la Peramiko, Miradi ya Umwagiliaji kama nilivyoeleza kwenye ziara, wala sina haja ya kusema hapa, tumeshapata shilingi milioni 600 kazi imeanza.

Tuna fedha nyingi zisizopungua shilingi bilioni tatu kutoka Mradi wa Bonde la Mto Ruvuma kwa maana ya ushirikiano wa Tanzania na Msumbiji kule Namatui miradi itaendelea, tunazo fedha ambazo zitaendelea kuletwa kwa ajili ya kununua mahindi kwenye Vituo vya *SGR*, tunaiomba Serikali ituongezee matrekta, magunia, mifuko ya kukuzia mbolea kutoka moja kuwa miwili tuwalishe na Wananchi wa Monduli kule anakolalamika Mheshimiwa Edward Lowassa, uwezo wa kulima tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali yangu, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ninaomba niwataje ambao watachangia; Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Augustino Mrema, Mheshimiwa Ismail Aden Rage na Mheshimiwa Ali Juma Haji wajiandae. Tunaanza na Mheshimiwa Godfrey Zambi.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu, ambayo iliwasilishwa hapa Bungeni jana. Kwanza, ninaomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kwa hotuba zao nzuri ambazo walizitoa jana jioni; ninawapongezeni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kuchangia na suala linalohusu maslahi ya Madiwani, lakini pia na Wenyeviti wa Vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani kwa sehemu kubwa, wanafanya kazi zinazofanana na kazi za Wabunge, kinachotofautisha ni ukubwa wa maeneo, lakini jambo

linalosikitisha na hili ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alisikilize sana na Mheshimiwa George Mkuchika pia alisikilize sana na pale watakapokuwa wanatoa majibu, watoe majibu ya kuridhisha ili Waheshimiwa Madiniwani katika nchi yote, waweze kusikiliza Serikali inasema nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani wanafanya kazi kubwa sana katika nchi hii, katika maeneo ya Kata, wao ndiyo wanaowakilisha Serikali kwa sehemu kubwa sana, wao ndiyo wanaosimamia Kamati za Maendeleo za Kata na shughuli zote za maendeleo zinazofanywa katika Kata hizo zinasimamiwa na Waheshimiwa Madiwani. Kinachosikitisha ni kipato ambacho Madiwani wanapata kutokana na kazi yao kubwa na ngumu ambayo wanaifanya katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Madiniwani 4,517 katika nchi hii, kwa hiyo, hapa ninapendekeza kwa Madiwani hawa tuache kuwalipa kitu kinachoitwa posho, tuwalipe mishahara na hili ndilo limeanza kuzungumzwa sana hapa. Suala la posho limeanza kupigwa kelele katika Bunge hili kwamba, posho hazistahili, kwa hiyo, tukiendelea kuwalipa kitu kinachoitwa posho Wabunge na wao wanasiaka kwamba, sasa Bunge linapiga vita posho, hawa Madiwani watasononeka sana. (*Makofi*)

Ninaomba tuwalipe Madiwani mishahara na nina sababu ya kusema hivyo, kama nilivyosema wanafanya kazi kubwa sana katika nchi hii na nimefanya hesabu ndogo tu na hili Mhehimiwa Luhaga Mpina alishalisema hapo awali, ninaomba niliseme kwa msisitizo huu. Hawa Madiwani 4,517 waliopo, kama Serikali itaamua kulipa shilingi laki tano kwa mwezi kama mshahara, maana yake tutakuwa tunawalipa shilingi bilioni 2.2 kwa mwezi na kwa maana hiyo kwa mwaka tutawalipa shilingi bilioni 27, jambo ambalo ninaamini lipo ndani ya uwezo wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali inakusanya takriban kwenye shilingi bilioni 500 kwa mwezi, hatuwezi kushindwa kutenga shilingi bilioni 27 za kuwalipa madeni kama mishahara kwa mwaka mmoja, haiwezekani. Kwa nchi ambayo iko *serious*, haiwezekani. Leo hatupo Madiwani wameendelea na vikao katika nchi nzima, kwa ajili ya kujadili maendeleo katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ifikirie kuwalipa Madiwani mishahara na siyo posho kama ilivyo sasa na posho zenyewe zinazoitwa posho shilingi 120,000, hatuwatendei haki Madiwani. (*Makofi*)

Ninaomba tuwatendee haki kwa sababu wanafanya kazi sambamba kabisa na sisi Wabunge na ninaomba Wabunge wenzangu wote katika hili tuwaunge mkono Madiwani wenzetu, kwa sababu na sisi pia ni Madiwani ili waweze kufanya kazi vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo suala la Wenyeviti wa Serikali za Vijiji; katika ngazi ya vijiji, Wenyeviti ndiyo wanaosimamia maendeleo kwa ujumla. Kinachosikitisha *VEOs* ambao ndiyo watendaji katika vijiji wanalipwa mishahara, Wenyeviti mpaka leo hawalipwi kitu. Serikali inazungumza kwamba, tunawalipa posho, lakini unapotenga asilimia 20 ya mapato ya Halmashauri kwamba yaende kule kijijini

ndipo umlipe Mwenyekiti, hatuwatendei haki, kwa sababu kuna vijiji vingine ambavyo havipati hata senti tano, kwa maana hiyo hawa Wenyeviti wataendelea kutokupata kitu.

Ninaomba Serikali pia ifikirie kutenga fedha kidogo kwa ajili ya Wenyeviti na hapa nimejaribu kufanya hesabu kidogo; tuna vijiji karibu 11,817 katika nchi hii vilivyosajiliwa na kwa taarifa ambayo Waziri Mkuu alitwambia jana. Sasa ninafikiri hata ukiwatengea posho ya shilingi 60,000 tu kwa mwezi, maana yake kwa mwaka mmoja watakuwa wanalipwa kama shilingi bilioni nane. Sasa ukijumlisha hizi shilingi bilioni 27 na shilingi bilioni nane ambazo Wabunge watapewa, utapata shilingi bilioni 35.6 kwa mwaka mzima. Hatuwezi kushindwa kulipa tena Wenyeviti posho ya shilingi 60,000 kwa mwezi ili wasimamie vizuri shughuli za maendeleo katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala ambalo Wabunge wote ninaamini tumekuwa tunapigiwa kelele sana tunapokwenda kwenye ziara katika maeneo mbalimbali, wanasma wafikiriwe kulipwa chochote kuliko utaratibu wa sasa ambao Serikali ikipita na Mheshimwa Aggrey Mwanri akipita anasema, Serikali mna uwezo kabisa; lakini posho zipo wapi huko vijijini ambapo tunaambiwa tuwalipe hawa? Ninaomba sana hizi hoja Serikali izitolee maamuzi.

Suala la pili ni la mbolea ruzuku, ambayo ina ruzuku ya Serikali. Hili limekuwa ni tatizo lingine katika nchi hii. Utaratibu unaotumika leo kwa mbolea wa ruzuku katika nchi siyo mzuri. Mbozi ni eneo ambalo linalima sana, Mkoa wa Mbeya ni mkoa ambao unazalisha sana kwa maana ya mahindi na mazao mengine, lakini ninazungumzia mbolea ya ruzuku. Kwanza, mbolea ya ruzuku imetawaliwa na wizi mkubwa, mbolea hiyo ya vocha imetawaliwa na wizi mkubwa sana na mimi ninaomba nitoe mfano. Mwaka 2008/2009 kwa Wilaya ya Mbozi zaidi ya vocha za thamani ya shilingi milioni mia mbili zilipotea, ninaamini Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na *RAS* wangu, wanasiliza na wanayajua haya maana tumeyazungumza sana katika Vikao vya Mkoa.

Mbolea imeibiwa zaidi ya shilingi milioni 200, watu wamekamatwa wamepelekwa Mahakamani, wameshinda, wamerudishwa kazini hakuna hatua nyingine zinazochukuliwa. Tunapokwenda vijijini, Wananchi wanasma Serikali inabariki wizi kwa sababu watu wamekamatwa, wamepelekwa Mahakamani, wameachiwa, Serikali imeendelea kuwaweka kazini na kila mwaka wameendelea na wizi wa vocha hizi ambazo zinatolewa na Serikali. Hatuwezi kupiga hatua za maendeleo kama Serikali itaendelea kuwalea watu ambao wanaiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwenye kampeni niliwahi kusema sitampigia makofi mtu ambaye anawahujumu wakulima, mtu mwizi sitampigia makofi, afadhali kura hizo nizikose kuliko kumpigia makofi mwizi. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iliangalie hili na ichukue hatua madhubuti kwa wale wote ambao watakuwa wanajaribu kuhujumu zoezi la mbolea. Mbolea hizi pia zinatugawa huko vijijini; kuna Wananchi wanaopata na wanaokosa. Wanaokosa wanasma ninyi Serikali ya CCM endeleeni na hao hao ambao mnawapa mbolea. Mbolea hii inatugawa na kwa sababu inakuja chache, hatuwezi kuwapa Wananchi wote, inatugawa sana. (*Makofi*)

Ninaomba Serikali iangalie namna ya kuondoa tatizo na hilo ni tatizo kubwa hasa katika Mfumo wa leo wa Vyama Vingi vya Siasa, maana ndiyo hapo wametokea watu wengine wakinyimwa mfuko wa mbolea wanakimbilia Chama cha Upinzani, wameona Serikali ya Chama cha Mapinduzi haiwafai. Ninaomba tuangalie namna ya kufanya Wananchi wengi waweze kuwa na amani na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Zipo pia mbegu na dawa, tumeendelea kupata mbegu feki na dawa zingine ambazo siyo nzuri sana. Wananchi wanunua, lakini wanapokwenda kuzipanda, mbegu nyingine hazioti na dawa nyingine hazifanyi kazi; ninaomba Serikali ijaribu kuangalia hili na kulismamia vizuri zaidi. Zimeanza pia kupita *propaganda* kwa mbegu zile ambazo zinazalishwa na kituo chetu cha kilimo pale Uyole. Kuna mbegu *UH 6303* na *UH 615*, wapo wafanyabiashara ambao wameanza kuzipiga vita mbegu hizi kwamba, hazifai. Ninaomba niseme hizi ni *propaganda*, mbegu hizi hizi ndizo Mheshimiwa Kofi Annan alipotembelea Mbeya alikwenda kuzikagua *Yura* na alikagua mashamba ambayo mbegu hizi wamepanda wakulima na zimeota vizuri sana. Ninaomba nithibitishe, mimi ninalima kidogo, nilipanda mbegu *UH 6,303* imeota vizuri kuliko mbegu zingine zozote ambazo zinajaribu sasa kuletwa kwenye soko kwamba, zinafanya kazi vizuri, jambo ambalo siyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie jambo lingine linalohusu kahawa. Kumeanza kuwa na biashara ya kununua kahawa ya maganda. Kinachosikitisha, bei zinazotolewa kwenye kahawa hii au kahawa ya matunda ni ndogo sana, ninaomba Serikali iwasimamie wakulima ili waweze kufaidika na kilimo chao. Ninaomba niseme tarehe 21 Januari, 2010 milikwenda kwenye Mkutano wa Wadau wa Kahawa pale Moshi, tulijadili mambo mengi ikiwa ni pamoja na ununzi wa kahawa ya matunda na kahawa nyingine iliyokamilika. Sasa kinachotokea, wapo wafanyabiashara ambao wanataka wanunue kahawa ya cheli au kahawa ya matunda kwa shilingi 500 kwa kilo, tukiruhusu hilo huu utakuwa ni wizi wa mchana na mkulima huyu hatafaidika hata kidogo. Ninaomba nieleweke hapa, hoja hapa siyo kuwepo au kutokuwepo kwa biashara ya cheli, suala hapa ni mkulima huyu anaafaidika namna gani ambapo usiku na mchana anawaza namna ya kuendesha maisha yake katika hali ngumu iliyopo leo.

Kwa hiyo, ninaomba Serikali ilisimamie hili, wasiwepo wafanyabiashara wachache ambao watakwenda kwa mkulima kununua kahawa kwa shilingi 500, ile cheli, halafu watakapouza kilo moja wao wauze kwa shilingi 7,000, 8,000, wakati mkulima huyu anaendelea kuteseka sana, hili halitakuwa jambo sahihi sana. Ninaomba niipongeze Serikali ya Mkoa kwa kuliangalia jambo hili na kulismamia, ninaomba Mkuu wa Mkoa na Viongozi wenzako, msikatishwe tamaa katika hili, ninaomba mlisimamie vizuri ili wakulima wetu waweze kufaidika vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumze jambo la matuta na hili ninalizungumza mbele ya Waziri Mkuu, kwa sababu ya umuhimu wake. Kule Mbozi kuna Kijiji cha Ihanda na Kijiji cha Luanda, maeneo haya ni hatari sana kwa maisha ya watu na ninaomba Wananchi wa Mbozi wanielewe kwamba, ninasimama vizuri sana kuwatetea katika hili. Vimekuwa vinatokea vifo vingi sana maeneo ya Ihanda na eneo la Luanda, vinavyosababishwa na magari ambayo yanakwenda kwa *speed* sana. Miezi

michache iliyopita, eneo la Ihanda limeendelea kuwa sehemu hatari sana na Wananchi wameendelea kufa sana. Vilevile baada ya Wananchi kuona wanagongwa sana, siku moja waliamua kulizuia gari moja lililosababisha kifo cha Mwananchi pale, wakalichoma moto na barabara ilifungwa kwa karibu saa tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumekuwa tukilizungumza kwenye Vikao vya Barabara vya Mkoa (*Road Board*), tumeomba maeneo hayo yawekewe matuta; mpaka leo Serikali inapata kigugumizi cha kuweka matuta. Ninasikitika sana maeneo mengine yanawekwa matuta na barabara zinaendelea kujengwa. Ninaomba pale ambapo Wananchi wanagongwa mara kwa mara, matuta yawekwe, lakini hayawekwi. Hili ni jambo ambalo wakati mwininge tunalazimika sasa kutoa shilingi kwenye Bajeti ya Serikali, pamoja na kwamba Bajeti zitapita, lakini tuoneshe *concern* kwamba, tunaumia kwa sababu Wananchi wetu wanaendelea kupoteza maisha yao na baada ya kuzungumza hapa hoja itakapojibwa, Wananchi wa Ihanda na Luanda wasikie kwamba, wanatendewa haki kwa maana ya kwamba, Serikali itakuwa inaweka matuta katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaomba nizungumzie suala la kutoa ajira kwenye Halmashauri zetu. Ninaomba Mamlaka ya Ajira zirudishwe kwenye Halmashauri, tusitegemee ku-*centralise* ajira wakati tuna *D by D*, tuna ugatuaji wa madaraka kwenda Vijijini, Wilayani, leo tuna-*centralise* ajira zifanyike Dar es Salaam; ajira za madereva, wahudumu, *VEOs* na *WEOs*. Jambo hili haliwezi kukubalika, tunaomba Halmashauri zirudishiwe madaraka ili ajira ziweze kufanyika katika Halmashauri zetu na leo ninavyosema, kule Mbozi ninaamini maeneo mengine nchini, yamekwama kuwa na Watendaji wa Vijiji kwa sababu ya *bureaucracy* iliyopo mpaka uajiriwe huko Dar es Salaam, jambo hili haliwezi kukubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme Serikali iliahidi kuboresha Kituo cha Polisi Mbozi pale Vwawa, Kituo hiki kilijengwa miaka ya 1960 na mwaka 2007 nilisema hapa Bungeni kwamba, tunaomba kijengwe upya. Serikali iliahidi, mpaka leo hakuna kinachoendelea, ninaomba hilo lifanyike. Mwisho, ninaomba Hospitali ya Vwawa, Hospitali ya Wilaya, ambayo pia Serikali iliahidi kuijenga upya, iijenge upya na tuliamiwi zimetengwa shilingi bilioni tatu na tukaelezwa hakuna maendeleo yoyote yanayoruhusiwa kufanywa kwa maana ya ukarabati wa majengo ambayo leo mengine yamechakaa, lakini Wizara imesema yasikarabatiwe kwa sababu kuna ukarabati mkubwa unaokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hilo lifanyike na baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Kwanza, ninamshukuru sana Waziri Mkuu, kwa hotuba yake ya Bajeti; Hotuba ni nzuri na Bajeti ni nzuri. Pili, ninampongeza sana Rais, kwa kumteua Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara mbili mfululizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimevutiwa sana na maneno ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ukurasa wa 64; Mheshimiwa Waziri Mkuu anazungumzia juu ya amani, haya maneno ya hekima, busara ni vizuri kwa manufaa ya Tanzania nikayanukuu: “Tunatimiza miaka 50 ya Uhuru tukiwa tumejijengea misingi imara ya amani na utulivu na sote tumeona manufaa yake. Hata hivyo, kuna dalili ya baadhi yetu kutaka kuanza kubomoa misingi hiyo. Ninaamini tunaweza kudai haki zetu bila kusababisha uvunjifu wa amani au vurugu ya aina yoyote.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuwaambia wanasiwa wa pande zote katika suala hili la amani, sote ni wadau; tusipofanya hivyo tutaivuruga nchi yetu sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukataka kufikia malengo yetu ya kisiasa au tukataka kuibadili Serikali iliyopo madarakani, lakini tutumie hoja, tufanye hivyo kwa amani, tusishabikie sana uchochezi, vurugu na hasa maandamano. Ninasema maandamano, kwa sababu tangu yamefanyika yameishia kupindua Serikali zilizoko madarakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili gazeti nililonalo hapa siyo la *TLP* ni gazeti makini la Mwananchi la Alhamisi, tarehe 9 Juni, 2010. Linaunga mkono maneno hayo na linatutahadharisha, linazungumzia habari ya Misri kwa kubadiliki Serikali ya Misri kwa vurugu, maandamano na uchochezi wamepata faida gani. Wenyele wanasema biashara ya utalii nchini Misri imeshakua kufuatia mabadiliko ya kisiasi nchini, baada ya aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Hussein Mubarak, kuondolewa na Wananchi. Makampuni kadhaa ya Biashara ya Utalii yameonesha kuwa, hali ni mbaya na mengine yamewapunguza wafanyakazi wakati wafanyabiashara wengine wanafikiria kufunga biashara zao. Watalii wengi wanaogopa kutembelea Misri baada ya machafuko ya karibuni. Maofisa wa Misri wanaonya kwamba, nchi hiyo inaweza kukabiliwa na mgogoro mkubwa wa kiuchumi. Kwa upande wake, Jenerali Nasser, Mjumbe wa Baraza Kuu la Kijamii linalotawala kwa sasa nchi ya Misri, aliyambia katika mkutano wa kiuchumi Mjini Cairo kwamba, uwekezaji kutoka nje umesimama. Kuhusu kiwango cha umaskini toka kuibuka kwa vurugu zilizomwondoa Rais Mubarak madarakani, inasemekana kuwa kimeongezeka na kufikia asilimia 50.

John Stakafon, ameonya kuwa, kuendelea kuzorota kwa uchumi katika Taifa lile, itakuwa maafa makubwa kwa nchi. Sekta ya Utalii Nchini Misri, ambayo ilikuwa inachangia pato na ajira, sasa imepoteza wastani wa dola bilioni moja kila mwezi kutokana na watalii wengi kuahirisha safari zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tahadhari ninayotaka kusema hapa, kama mdau wa nchi hii, kama mdau wa amani, vitendo vyetu tunavyofanya tusije kuharibu nchi yetu wenyele. Leo Misri haitawaliki, hakukaliki, hakuna biashara, uchumi umezorota, watalii hawafiki, umaskini umeongezeka, je, ndicho tunachokitaka hapa Tanzania? (*Makofi*)

Ndugu zangu, kule Madagascar, maandamano yalianza hivi hivi, kuna huyu kijana DJ anayeitwa Andry Rajoelina, akahamasisha watu kum-discredit Rais, kui-discredit Serikali ni ya wezi, majambazi; sawa, wakafanikiwa kwenda Ikulu wakamwondosha Rais Marc Ravalomanana aliyechaguliwa Kikatiba na Kisheria. Leo ile nchi haitawaliki, hakukaliki, hakuna amani kule Madagascar; ndiyo tunachotaka huku Tanzania? (*Makofi*)

Leo Libya hakukaliki, yalianza maandamano ya amani, uwongo uwongo, leo Marekani wamevamia nchi ile, Ufaransa wamevamia nchi ile, Uingereza wamevamia nchi ile. Kuna vita. Ndicho tunachotaka Tanzania? Ndugu zangu Tunisia mambo ni hayo hayo, ndiyo sababu nikasema haya maandamano tunayoendekeza tunayofundisha vijana, lengo lake kote ambako yamepitia ni kuiondoa Serikali iliyochaguliwa na wananchi kwenye madaraka. (*Makofi*)

Kenya baada ya uchaguzi, watu hawakuridhika na uchaguzi, maandamano yale yaliua watu 1,000. Watu wamekuwa wakimbizi katika nchi yao mpaka leo hawajajengewa vile vibanda, wala ajira walizoahidiwa wazipate wale vijana waliokufa, wale wajane. Ndugu zangu mwisho wa siku baada ya machafuko, Mwai Kibaki anakaa upande mmoja wa meza. Rafiki yangu Raila anakaa upande mwingine, wanaambizana wewe utakuwa Rais, mimi Waziri Mkuu, biashara imekwisha pale. (*Makofi*)

Wale ndio maana wakauawa. Wako wapi leo? Haki zao ni nini? Kwa hiyo, nataka nikuunge mkono Waziri Mkuu kwa hili la amani halina Chama Tawala wala Vyama vya Upinzani. Hatuwezi kuvuruga nchi yetu tukaharibu nchi hii. Kwa sababu hawa vijana wasiokuwa na ajira tunaowadekeza, tunaowalelea kuwapeleka barabarani, niliwhali kusema hapa, jamani tuwapeleke vijana wetu kwenda kupiga kura. Ndiyo namna ya kuiondoa Serikali iliyoko madarakani kikatiba. (*Makofi*)

Narudia tena, tulijiandikisha watu milioni 20 mwaka jana, waliopiga kura milioni nane, na milioni 12 hawakupiga kura. Lakini ukiwaambia waandamane wanakwenda kuandamana. Mimi nataka niwatahadharishe Watanzania, haya mazoezi mnayofanya ya kuandamana, angalieni Madagascar, angalieni Misri, angilieni Tunisia na Libya. Je, ndicho mnachokitaka kije Tanzania? Je, hatuwezi kubadili Serikali yetu kama hatutaki kwa hoja, kwa kupiga kura tukaenda kwenye vituo? Mimi wala siamini kama maandamano yanaweza kumweka mtu madarakani. Leo kule Misri anayetawala siyo wale walioandamana na vyama vyao.

Jeshi limejitokeza, limechukua madaraka, jeshi ndilo linatawala sasa. Kwa hiyo, ninachotaka kusema, narudia tena mwaka 1995 mimi nilipata kura 1,800,000, asilimia 28. Hakuna mpinzani anayeweza kufikia kiwango changu, bado mimi nang'ara hapa. (*Makofi*)

Tukiangalia kura nilizopata mwaka jana, mbona ziko chini ya zile za Augustino Lyatonga Mrema? Nyie Serikali, Waziri Mkuu, nakuomba, mimi nilikuwa Naibu Waziri Mkuu, mdogo wako.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mrema, ongea na Mwenyekiti.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Haya. Ndugu Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu. Maana mimi nilikuwa mdogo wake Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Ndani, niliweza kuwa mdau wa kutetea amani hii. Mbona zile haki zangu hamnipi? (*Kicheko/Makofi*)

Wewe ukiacha kazi utapewa asilimia 80 ya mafao yako ya mshahara wako, nipeni basi hata asilimia 20. Mnasema hiki cheo changu hakikuwa kwenye Katiba, Rais ndiye anaanzisha cheo. Hata Mawaziri wetu wanaanzishwa kwa *decree* ya Rais. Ilikuwaje cheo ambacho Mwalimu Nyerere alianzisha, akasimamia akakaa pale Dkt. Salum Ahmed Salum, Naibu Waziri Mkkuu wa pili Agustino Lyatonga Mrema. Juzi mlikuwa mnaptisha posho za Majenerali, mnasema hapa mkipunguza posho za Magenerali hapakaliki. Kwa hiyo, ya Mrema mkimnyima ndiyo mnaona ndiyo sawa sawa? Msije mkaona simba amenyeshewa mkafikiri nyani. Nyie mmenifundisha mambo mengi, najua vitu vingi. Sasa kwa nini haki hamnipi? Sasa naomba Serikali hii na hasa Waziri Mkkuu ili niendelee kutetea mambo mengi ya nchi hii, naomba haki yangu mnipe. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kuhusu mishahara ya Walimu. Mheshimiwa Mkuchika amezungumza kwenye ukurasa wa 18 kuhusu madeni ya walimu. Taarifa zinaonyesha kwamba wamelipwa mpaka mwaka 2008. Hebu fikiria mwalimu maskini mpaka 2008 walimu wanadai mishahara, wanadai posho zao, wanadai likizo tangu mwaka 2008 hajawalipwa. Mimi kule Moshi Vijijini walimu wangu wanadai shilingi milioni 67. Chonde chonde nakuomba fedha zile kama watapatiwa wale walimu nitashukuru sana.

Wako walimu vijana ambao wameingia kwenye ajira kuanzia Januari mpaka leo, wanadai jumla ya shilingi milioni 390, hawajapewa. Wako shule wanafundisha, hawajapewa, wanahangaika, wakifika pale kwenye Ofisi ya Mkurugenzi hawapewi. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkkuu ndani ya siku mbili, tatu utakavyokuwa una-*wind up* hii bajeti yako, uniambie kama wale vijana wangu 130 wale walimu ambao wako pale kuanzia Januari mpaka sasa hivi kama hizo pesa wamepata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kule kule ni njaa. Tuliomba tani 17,333.7 kuanzia Juni mwaka huu mpaka Juni mwaka utakaokuja. Lakini mpaka sasa hivi Serikali imetuonyesha kwamba wataanza kutupatia tani 1,184. Tani 118 zitolewe bure kwa ajili ya wazee, walemvu, vijana na yatima na kadhalika. Tani 1,065 za mahindi ziuzwe kwa wananchi kwa shilingi 50 kwa kilo. Lakini tatizo ni kwamba yale mahindi kutoka Arusha hayajaja kwa sababu tu Serikali imetuma shilingi milioni 33.7. Kumbe wale watu wanaobeba mahindi wanataka shilingi milioni 52. Chonde chonde naomba hizo fedha zitoke, mahindi yale yaje.

Halafu na ile biashara inayofanyika pale Himo, watu wana njaa, huku kuna malori ya mahindi yanakwenda Kenya. Waziri Lukuvi alikwenda mpaka pale. Malori ni mengi, hayapiti kwenye barabara rasmi zinazojulikana, wanapita kwenye vichochoro, madaraja yangu yamevunjwa. Naomba Serikali ieleze sera yake ni nini sasa hivi? Kwa sababu

wananchi wa Vunjo hawanielewi. Huku wana njaa, wanaona malori ya mahindi yanaelekea Kenya. Kwa nini ile biashara tusifanyie pale Himo, watu wa Kenya wenye njaa wakaja kununulia pale? Kwa nini tuwapelekee huko mipakani kwa kutumia njia za panya, vichochoro, kama mahindi yale yana bei huko Sudan ya Kusini au kule Somalia, basi waje kununulia pale Himo kusudi tuweze kupata ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa sababu kuna njaa, kuna miradi ya umwagiliaji. Serikali imefanya vizuri kupeleka fedha kule Kahe ya Mashariki kwa ajili ya umwagiliaji wa maji. Mmeleta fedha nyingi sana ambazo sina hakika, ndiyo sababu nilikuwa nataka nimwombe Waziri Mkuu kama ataweza kunitumia mtu kwenda kucheki, fedha alizotuma mwaka 2007/2008 shilingi milioni 60, mwaka 2008/2009 shilingi milioni 210 na mwaka 2010/2011 shilingi milioni 250. Ni fedha nyingi, lakini: Je, tuna hakika kwamba fedha hizi zimefanya kazi yake inavyotakiwa kule Kahe? Kwa nini watu wana njaa wakati walitakiwa wawe na maji na Serikali imetumia fedha nyingi sana?

Lakini linguine, hata upande wa Kahe Mashariki, Serikali imetuma fedha nyingi sana. Mwaka 2008/2009 Serikali imetuma shilingi milioni 155. Mwaka 2010/2011 shilingi milioni 200, mwaka 2011/2012 shilingi milioni 250. Ni fedha nyingi sana zinakwenda kwenye umwagiliaji. Siwezi kuilaumu Serikali kwamba haiangalii Jimbo lile, lakini bado watu wana njaa, hayo maji yako wapi? Kwa hiyo, naomba timu ya kwenda kule Kahe Mashariki na Kahe Magharibi.

Halafu nina mambo mengine madogo. KINAPA imenipa fedha shilingi milioni 20 kwa ajili ya kujenga tanki la maji pale Ashira. Nimeoiomba Serikali shilingi milioni 10 tu ku-*supliment* shilingi milioni 20. Serikali tunashindwa jamani! KINAPA imetoa shilingi milioni 20. Sasa naomba shilingi milioni 10 tu. Mimi nimekwishachangia shilingi milioni tatu. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu mchango wako, na wewe unisaidie ili tanki lile tulimalize.

Halafu ule mradi ambao Mheshimiwa Rais aliahidi wa maji ya kunywa Himo, shilingi milioni 150 wananchi wamehangai, wamechimba mitaro, wamelaza mabomba, lakini bado mradi ule haujakamiliika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, muda wako umekwisha.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Kwa misingi hiyo, naunga mkono hoja hii nzuri, itasaidia sana wananchi wa Vunjo. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Naomba niwataje watakaochangia tena. Tuna Mheshimiwa Aden Rage, Mheshimiwa Juma Haji na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa ajiandae. Tunaanza na Mheshimiwa Rage.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nami nawashukuru wananchi wa Manispaa ya Tabora kwa kunichagua kwa kishindo baada ya kutafuta nafasi hii ya Ubunge kwa kipindi kirefu sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, ningependa kuchukua nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi Mkao wa Tabora kwa kuhakikisha majimbo yote kwa Mkao mzima yamechukuliwa na Chama cha Mapinduzi. Tunataka kuwaambia wenzetu wa upande wa upinzani watu wa Tabora hatudanganyiki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Tabora ina matatizo makubwa sana ya maji. Uwezo wa *TUWASA* ni kuzalisha maji sasa hivi lita 9,500,000 kwa siku tu. Matumizi ya maji kwa siku moja katika Manispaa ya Tabora ni lita milioni 24. Tuna upungufu wa takribani 15,500,000. Kama unavyoolewa, Manispaa ya Tabora ni *semi arid*, huwezi kupata maji chini ya ardhi. Maji ambayo yako juu ya ardhi, tuna mabwawa mawili, bwawa la Igombe na bwawa la Kazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Bwawa la Igombe limekauka. Lilikuwa lina uwezo wa kutoa lita milioni mbili za maji kila siku. Lakini sasa halitoi maji zaidi ya miezi sita mpaka sasa. Wananchi wa Tabora wanapata taabu sana. Kwa hiyo, tunaomba hatua za dharura ziwekwe ili kuwezesha *TUWASA* waongeze uzalishaji wa maji kutoka katika Bwawa la Igombe angalau waweze kuzalisha maji lita milioni 15 itaweza kupunguza matatizo kwa wananchi.

Sasa natoa ushauri kwa Serikali, *TUWASA* wanadai pesa karibu shilingi milioni 411 katika Wizara ya Ulinzi na Polisi. Tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie ili pesa hizo tupate tununue pampu mbili tuweze kuzalisha maji na wananchi wa Tabora waweze kuwa na uhakika wa kupata maji angalau kwa kipindi hiki mpaka mwaka 2013 au 2014, mradi kabambe wa maji kutoka *Lake Victoria* ambao ningependa kuwapongeza Serikali nimeona kwenye bajeti wametenga pesa kwa ajili ya kuvuta maji kutoka Kahama mpaka Tabora. Lakini hatuwezi kuyapata maji hayo mapema, kuyapata itakuwa mwaka 2013 au 2014. Kwa hiyo, naomba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iiangalie hili kwa makini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora tuna hospitali moja inaitwa Kitete, ndio hospitali ya Mkao. Hospitali hii imejengwa mwaka 1906, wakati huo ilijengwa kama *military barracks* (Kambi ya Jeshi). Lakini wakati wa vita, wanajeshi wa Kiingereza wakawa wanatumia vile vile kama hospitali ya wanajeshi wanaopata majeraha, baadaye wananchi wa Tabora na wenyewe wakaanza kutibiwa pale na hatimaye baada ya uhuru ndio imekuwa hospitali yetu kuu ya Tabora. Sasa fikiria majengo ya mwaka 1906 na leo ni mwaka 2011, ni miaka mingapi? Kuna ukarabati ambao unaendelea kila siku, lakini ukarabati huu bado shida imekuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nasikitika katika bajeti ya mwaka 2009/2010, hospitali ile ilitengewa shilingi milioni 600; Mwaka 2010/2011 hospitali ile ikatengewa shilingi milioni 290 kwa ajili ya ukarabat; mwaka huu tumetengewa shilingi milioni 94. Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu iiangalie kwa makini pesa hizi zilizotengwa, hazitoshi hata kidogo, kwani hali ya jengo ya *Theatre* haliridhishi hata kidogo; *X-Ray Department* hairidhishi hata kidogo; Wodi ya wagonjwa ya watu wa akili siyo nzuri hata kidogo; *Ward* ya majeruhi pia na yenyewe ina matatizo na *MCH Clinic* nayo ni tatizo

kubwa. Kwa hiyo, tusipoweza kuangalia tutasaidiaje, na *solution* ni kujenga hospitali mpya ya kisasa ili wananchi wa Tabora na wenyewe waweze kuokoka katika sehemu hii ya afya.

Ndugu Mwenyekiti, sasa hivi angalau tuna *dispensary* takribani 16. Tuna upungufu wa *dispensary* tisa. Nina imani kabisa kwamba TAMISEMI watafanya kila linalowezekana, vijiji vingine au Kata nyingine ambazo hazina *dispensary*, basi na wenyewe waweze kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora sijui kwa nini kila inapofika Novemba na Desemba ndege hazitui katika uwanja wetu. Kila mwaka ikifika kuanzia Novemba na Desemba za biashara ndege hazitui. Kwa hiyo, kuanzia Novemba mwaka jana mpaka leo mwezi wa sita ATC haijkwenda Tabora wala *Precision*. Kwa hiyo, tunaomba tafadhali sana mtuangalie na ningependa vile vile kuipongeza Serikali, nimeona wametenga shilingi bilioni 16 kwa ajili ya kukarabati au kujenga uwanja upya wa Tabora katika kiwango cha lami. Nadhani ni wakati muafaka sasa Ofisi ya Waziri Mkuu ikaihimiza Wizara ya Uchukuzi ihakikishe kwa sababu ninalewa wamekwishatangaza na tenda hivi sasa mkandarasi aweze kufika pale, wananchi wa Tabora tusiendelee kupata taabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora tuna matatizo makubwa ya usafiri. Usafiri ambao wananchi wa Tabora walikuwa wanautegemea siku zote ni usafiri wa reli. Usafiri wa barabara, barabara zetu za kwenda Tabora na katika Mikoa mitatu tu iliyobaki ambayo haijaunganishwa kwa kiwango cha lami, Tabora ni mojawapo. Lakini napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, Naibu Waziri wa Ujenzi, alikuja Tabora kutembelea pale na alitembelea kuhakikisha kwamba barabara ya Manyoni - Tabora, Tabora - Nzega na Tabora - Urambo wanapata kiwango cha lami. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Ujenzi ihakikishe hasa kwa kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu ahadi ambayo Mheshimiwa Rais alitoa kwamba kabla ya mwaka 2015 Tabora wataweza kwenda kwa lami mpaka Tabora. Nina imani kabisa ahadi ambayo ilitolewa na matumaini ambayo nimeyaona sasa hivi, makandarasi watano wako pale wanafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vile vile kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu, Manispaa ya Tabora tulikuwa *allocated* walimu wa Shule za Sekondari 138. Waliofika pale Tabora walifika 114. Walimu 12 walipochukua pesa yao wakaingia mitini, hawakurudi tena. Lakini mpaka sasa tuna walimu 102. Jambo hili kwa kweli ni la furaha na wananchi wa Manispaa yangu wameniomba niishukuru Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa tuna matatizo makubwa katika shule zetu za msingi. Tuna upungufu wa madawati takribani tunahitaji madawati yasiyopungua 11,000. Nina imani kabisa kwamba TAMISEMI wataangalia uwezekano wa kutusaidia kuweza kupata nafuu katika madawati. Katika Shule za Sekondari, mpaka sasa tumejitahidi tuna upungufu kidogo wa takribani madawati 2,870. Kwa hiyo, tuna imani kabisa kwamba TAMISEMI wataweka mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba vijana wa Tabora wanapata sehemu nzuri ya kusomea. Ninafahamu kuna mpango kabambe wa ADB wa kujenga maabara katika Shule zote za Sekondari. Nimefarijika leo nilipomsikia Waziri,

Kapteni Mkuchika, akiongea kwenye *Television* kwamba wataanza na maabara 500, nina imani kwamba basi Tabora Manispaa, haitasahaaulika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora zao ambalo ninapenda kujikita kwenye kilimo sasa, zao ambalo tunajivunia na tunalitegemea ni zao la tumbaku. Lakini tunaomba Serikali isituchanganye. Wizara ya Kilimo inahimiza tulime tumbaku kwa nguvu zote na tumelima. Wizara ya Biashara na Viwanda, inatafuta masoko, Wizara ya Afya inaanza kupiga vita zao la tumbaku, tusilime tumbaku. Sasa inataka tufanye nini? Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aangalie tatizo hili, kwa sababu kuna Azimio lililopitishwa na *Head of States* kule Addis Ababa, katika kikao chao cha 18, nchi za kiafrika zinazolima tumbaku ni lazima wataendelea kulima tumbaku kulinda *interest* za nchi zao. Kwa hiyo, kikubwa ambacho tunaiomba Serikali, iangalie bei ya tumbaku, mwaka huu tumepata bei kidogo, siyo nzuri, lakini mwaka jana tulipata bei nzuri. Tuna imani kwamba Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba tunapata bei nzuri katika mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazungumzaji waliotangulia...(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, tunakushukuru sana.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuunga hoja 100 kwa 100. (*Makofi*)

MHE. ALI JUMA HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema leo hii, kusimama katika Bunge lako hili Tukufu na kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kutoa pongozi kwa chama change Tukufu, Chama cha Mapinduzi kwa kunithea mimi kuwa mgombea kwa tiketi ya chama hicho katika Jimbo hili la Chaani. Nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Chaani kwa kunichagua kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu uliopita na kuweza kunirejesha tena kwa kipindi cha pili katika Bunge hili Tukufu. Nawapongeza sana kwa imani waliyonionyesha na mimi ninawaahidi tutaendeleza kasi kuliko ile ya kipindi changu cha kwanza, kipindi kilichopita. Ninawaomba wawe na subira, wanisubiri nirudi, tukaanze kazi zetu za kuhudumia Jimbo letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mwizi wa fadhila, niishukuru sana familia yangu kwa uvumilivu mkubwa walionionesha na hususan dereva wangu, ndugu yangu, kwa kazi kubwa aliyokuwa anaifanya wakati wa uchaguzi wangu na hadi hivi sasa. Ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hotuba zao hizi walizoziasilisha mbele

yetu na leo tunazichangia hapa. Kwa kweli ni hotuba nzuri zenyenye kuleta matumaini na hasa kama zitasimamiwa vizuri katika utekelezaji wa shughuli zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kila penye uzuri hapana dosari. Zinakuwepo dosari. Mimi nizungumzie suala la Wizara ya Afya. Tumekuwa tukishuhudia sana bajeti ya Wizara ya Afya, inapanda kidogo kidogo inashuka, inapanda, inashuka, haina mustakabali ule wa kuendelea kupanda kwake hadi tukafikia lile azimio tulilolisaini la Abuja, mwaka 2001. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia haya kwa kutoa takwimu za bajeti ya Wizara ya Afya na tuone jinsi bajeti yake inavyotengwa. Mwaka 2008/2009 tulikaribia kufikia lengo lile la Abuja, tulifikia asilimia 13.7, mwaka 2009/2010 tukashuka tukafikia asilimia 11.3, mwaka 2010/2011 tumeshuka zaidi tumefikia 9%, mwaka huu tunaojadili hapa tunategemea kufikia asilimia 10. Hii inaumiza sana na inashangaza sana, na sijui kama tutafikia hii asilimia 15 ya Azimio la Abuja, kwa sababu, huu uwekaji wa bajeti ya kupanda na kushuka, kwa kweli inavunja moyo, na kwa nchi yetu kama hii sasa hivi, wakati wowote tunasherehekea miaka 50 ya uhuru, hadi leo hatujafikia hata asilimia 14 ya Azimio la Abuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili lifikapo mwaka 2015 inatakiwa nchi zote hizi zilizosaini ikiwemo nchi yetu ya Tanzania, ziwe zimeshafikia hiyo asilimia 15 ya Wizara ya Afya. Sasa hatujui kwa miaka hii mitatu iliyobakia kama tutaweza kufikia. Tunaomba Mungu tufikie. Itakuwa ni aibu kama hatukufikia, wakati leo hii tuona tunashindwa na nchi ndogo kama ya Rwanda, ambayo hivi sasa imeshafikia asilimia 18.3, nchi ambayo imekumbwa na misukosuko mikubwa ya kiuchumi, ya kisiasa, ya kijamii na hata tumeshuhudia wakimbizi wao tulikuwa tunawahifadhi sisi nchi ambayo ina amani kabisa. Lakini wametushinda, wao wameshakiuka hili Azimio kwa kufikia asilimia 18. Mimi ninaiomba Serikali tujitahidi sana tufikie angalao asilimia 14.5. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *MSD*. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, tumekuwa tukishuhudia kila mwaka *MSD* ina deni lisilofutika, halishuki, ila kupanda tu. Mwaka jana walikuwa na deni la shilingi bilioni 36, lakini bajeti tunayoipitisha hapa hadi mwaka huu wana deni la shilingi bilioni 46. Deni hili siyo kwamba *MSD* labda wanajingiza kwa utashi tu, hili linatokana na dawa ambazo hasa sisi tunaletewa za misaada, wanailipia pale bandarini, ukodishaji wa maghala. Kwa kweli, hili deni linaleta usumbufu mkubwa kwa Idara yetu hii ya *MSD*. Sasa mimi ningeiomba Serikali, ama kuwapatia fedha *MSD* kuondoa deni hili au walibebi wao Hazina kule na liondoke kule *MSD*. Dawa zile ziwe zinalipiwa na Serikali Kuu, moja kwa moja, vinginevyo tutakuwa tunaitwisha mzigo uliokuwa hauna mpango wowote. Ama kwa hatua nyingine, basi Serikali itangaze rasmi kulifuta deni hili kupitia Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunatembelea *MSD* kule, tulikutana nao wakatueleza baadhi ya matatizo yao. Moja ya tatizo walilotueleza ambalo leo ndiyo mahali pake na mimi kulieleza hapa, ni kwamba hizi Halmshauri zetu wakati mwingine

zinachelewa kupeleka mahitaji yao kule kwa wakati muafaka. Wanachelewa sana kiasi ambacho *MSD* na wao wanashindwa kupanga mipango yao vizuri.

Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuchika, azihimize hizi Halmashauri zipeleke mahitaji kwa wakati ili na wao *MSD* wafanye *order* zao kwa wakati na wananchi wetu dawa ziwafikie kwa wakati. Vinginevyo itakuwa inalaumiwa *MSD*, kumbe ni makosa ya upande mwingine. Hii ni sawasawa na makosa yale ya mchunga ng'ombe, anamtandika bakora ng'ombe wa nyuma kumbe mwenye kuchelewesha ni ng'ombe wa mbele, ndivyo inavyofanywa *MSD* sasa. Inalaumiwa *MSD* kumbe na makosa ya Halmashauri, yapo! Kwa hiyo, naiomba Serikali kuitia Wizara hii, iwahimize sana Halmashauri kupeleka mahitaji yao kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la udhibiti wa dawa. *MSD* hii hii, tuliangalia utaratibu mzima wa wanavyosafirisha madawa. Kwa kweli sisi tuliuona utaratibu ni mzuri sana kuanzia pale Bohari Kuu mpaka kufika Wilayani huko kwenye Vituo vya Afya. Lakini leo utashangaa dawa zile zikishafika kwenye Vituo vya Afya unazikuta zinauzwa katika maduka ya dawa binafsi. Ushahidi upo, kwa sababu juzi nimeangalia kwenye TV, nimeona Kituo cha Afya, nafikiri Wilayani Nzega, kimefungwa. Moja katika makosa yalichofungiwa ni kwamba mwenye kituo kile ni mdhamini wa dawa za Serikali na ni mfanyakazi wa Serikali pia. Kwa hivyo, hii ni dhahiri kwamba bado udhibiti dawa ni mdogo na tunaiomba Serikali ijitahidi sana kudhibiti dawa ili hizi dawa ziwafikie wananchi wetu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona wakati unakwenda mbio, nzungumzie hasa kuhusu uchafu wa Jiji la Dar es Salaam. Kwa kweli, Dar es Salaam, Jiji lile hasa sehemu za Kariakoo ni chafu mno! Tunaiomba Manispaa pale iwjajibike vizuri, uchafu wenyewe ni wa hatari. Mimi siku moja nilikuta maji kwa wingi yanatiririka, lakini naangalia juu jua ni kali sana. Nikafikiria kuna mvua, lakini kijua kikali, kuja kuangalia ni maji ya makaro ya nyumba mbalimbali. Jioni yake, sehemu zile zile watu wametandika mabango na maroba wanapanga biashara, nyanya, matango, maparachichi, watu wanununa kwa wingi. Ni hatari kwa afya za wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naomba liangaliwe sana katika Jiji lile na hasa sehemu ya Kariakoo. Msongamano wa magari katika zile barabara za ndani ni mbaya sana. Kwa kweli sasa hivi *parking* kubwa za magari ziko kule ndani. Mimi namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa makusudi nampelekea ombi hili, siku moja afanye ziara ya makusudi kupita mle ndani, siyo vibaya. Rais wa Zanzibar kule kila mwezi wa Ramadhani, hupita madukani, masokoni, haidhuru bei za vyakula haziteremki wala bishara za nguo, lakini wananchi wakiona tu anapita, basi wana tamaa. Kwa hiyo, na sisi tunamwomba Waziri Mkuu, hebu siku moja apitie burebure aone msongamano wa zile barabara zetu kule za ndani. Kwa kweli, hii hali inatisha na ni mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kengele ya kwanza imeshanililia, nimalizie kwa kuwashukuru sana wananchi wangu kwa kurejea tena na kuipongeza Serikali yetu. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Kwa kuwa kwa kipindi hiki ni mara ya kwanza kuchangia katika Bunge hili, kwanza nawashukuru wananchi wa Jimbo la Chwaka kwa kunirejesha tena kuwa Mbunge wa Jimbo hilo kwa kipindi cha nne. Naamini kwamba hawanirejeshi kwa sura, lakini kwa utendaji. Kwa hiyo, nategemea kwamba tutakuwa pamoja katika kufanikisha maendeleo ya Jimbo la Chwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitaingia sana katika Muungano na kitabu hiki kwa kweli, Waziri amebana. Amevana, sielewi sababu yenewe ni nini! Nasema Muungano wetu unatokana na nchi mbili. Muungano wetu unatokana na nchi mbili na wako viongozi walioasisi Muungano huu, lakini bado kuna sintofahamu au kutofahamiana ndani ya Muungano huu. Nasema hivyo kwa sababu, unajua ukitoka Zanzibar, kuna mtandao unasema umeondoka Mkoa wenye ofa mara mbili. Mimi nashangaa sana, hapa hatujaelewana! Sisi tumeunganisha nchi na mtandao huo mara moja tunataka uzime maelezo yako unayopelekea ujumbe. Unajielewa mtandao huu na unajifahamu vizuri! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilikuwepo vitabu hapa kila tukitoka vitabu hivi, katika miaka mitano, sita, nyuma mpaka kumi, tulikuwa Zanzibar, tunaorodheshwa kama Mkaoa. Suala hili mwiko! Baada ya kusema kipindi kilichopita, ikaandikwa Mkao wa kaskazini. Kwa hiyo, suala hili kwa kweli linatusononesha, hatuwezi kusema kwamba, aah, ng'ombe huyu tunapeleka huku kwa kupata kuku, hatuwezi. Hatuwezi kabisa, na hili ninalisemea kwa nguvu zote, sisi tumeungana nchi, tumeunganisha nchi mbili ndiyo ikaunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ikiwa kuna wachache, na hii yote kutoptaka na taaluma, na nilishangaa wakati mmoja alipokuja Rais, katika mzozo wetu tuliokuwanao hapa, alikuja kuhutubia Rais; toka nikae Bunge hili kipindi cha miaka 16, akihutubia Rais, tunatoa maelezo na ikiwa kuchangia tunachangia katika Bunge hili. Baada ya kukaa Rais, kutoa maelezo yake, baada ya mzozo uliotokea, akatamka rasmi kwamba Zanzibar ni nchi tukiwa ndani ya nchi yetu hivi, ikiwa tuko nje ndiyo tunasema Tanzania, tunawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini basi, lililojitokeza nikamwuliza Spika pale, nikainuka, nikamwuliza kuna tatizo gani hata kitabu hiki kipindi hiki hakikutoka? Nikajibiwa, kitatoka, tusubiri. Tukakaa kwa muda, nikasimama, nikauliza tena, nikajibiwa kwamba Ikulu, ndio yenyenye mamlaka. Mimi nilihesabu hivi, na akili yangu ilinijia kwamba ile kuzungumza kwamba Zanzibar ni nchi, halikupendeza! Ndivyo nilivyohesabu mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihesabu hivyo na akili yangu ilinijia hivyo, kwamba lile la kuzungumza kwamba Zanzibar ni nchi, halikupendwa. Ndivyo nilivyohesabu, kwa sababu mara zote hapa vitabu tunatoa na vitabu ni kumbukumbu. Hawa watoto wetu tunawapeleka wapi? Hali hii mnatuanzishia mzozo wenzeni, kwa sababu vitabu ndivyo vyenye kusomwa na vitabu angalia vitabu hivi, sehemu za mikoa nyuma tunakotoka vyote vinaambatanishwa, Zanzibar imebananishwa na Kilimanjaro, Mtwara, Arusha,

Lindi na kadhalika. Leo kwa mtoto, kizazi kinachokuja atakuja fahamu nini? Lipi atakuja kulielewa? Hili ni kosa tunalofanya wakubwa. Kaeni tufahamiane kwamba Zanzibar kuhesabu kama Mkoa, sisi hatutaki! Sisi hatutaki! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mwaka 2005/2010 wakati huo wa Mheshimiwa Ali Mohamed Shein, kuna hoja tisa zilijadiliwa. Katika hoja tisa hoja mbili ndiyo zilizopata maamuzi, hoja saba hazijapata maamuzi nazo ni kero za Muungano. Tunataka kujua na huku mnasema mnawaelimisha wananchi. Mimi sioni kama wananchi wanaelimishwa juu ya Muungano, ni kuleta mgogoro, hatimaye kwa kizazi kinachofuatia. Hata hili Bunge tukatazama, wengi hawakuwepo wakati wa mapinduzi. Kwa sababu mapinduzi mimi niliyosoma Darasa la Saba, haya angalia hali ya wajumbe wa hapa kama kweli wakati huo hata fahamu zipo na hapa kuna sababu nyingi wanasema kwamba tunawaelimisha wananchi, bado hawajaelimishwa. Tutaka usalama wa nchi hii, Muungano wetu uzidi kudumu uwe imara tufahamiane. Tuna haki ya watoto wetu, vijana kuwaelimisha na kuwapa taaluma juu ya Muungano. Tukifanya hivyo tutafika mahali pazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba vikao vya mafahamiano vya undugu, vya urafiki vimefanyika 75, lakini haya: Je, ya Muungano yamefanyika mara ngapi? Haya ndiyo yanayotesa wananchi. Haya ndiyo yenye matatizo! Leo tunafanya vikao vya urafiki mwema Wizara na Wizara, tunasema jamani mtutatulie toka tuliokuwa tunaufahamu, toka wakati huo tunaitwa Makao Makuu tunafahamu sisi umri wetu, basi tunataka mafamahamiano yawe mazuri, ili kuhakikisha mambo haya yanafanikiwa na yale yenye matatizo tuhakikishe kwamba yanaondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine, tunasema juu ya mapato. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 hapa nakumbuka liliuja suala kuhusu mambo ya gesi na mimi ni mmoja nikauliza swali hili kwa Naibu Waziri pale, akajibu swali hili tukataka Zanzibar kujua tumefikia wapi, jibu sikupata, nikaambiwa fedha zitapelekwa Hazina. Lakini hata kama zinapelekwa Hazina, ilikuwa tujue kipato cha Zanzibar ni kiasi gani? Ipelekwe huko huko kwa sababu kweli tumeungana, mafuta yanatoka huko huko, lakini tunakwenda *idle*, hatujui suala hili ni kosa. Tulete mafahamiano tujue kiasi gani tunachopata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar ina Serikali yake. Tunasema Zanzibar ina Serikali yake, ina watumishi wake, mambo 22, ni mengi kwa Muungano. Lazima mengine tuyatoe, Zanzibar inajitegemea na inaendesha nchi yake. (*Makofi*)

La mwisho, muda hapana, kuna 4.5 inaonyesha nyinyi miaka yote hii 4.5 ndiyo mliyoiwekea kuipa Zanzibar kwa sababu hata kwa upande wa *PADEP* tulipata dola milioni 54 za Kimarekani, lakini Zanzibar mkaipa 4.5. Nasema hili tuwasilishe muundo huu uondoke.

La mwisho, niliuliza swali kuhusu JKT na JKU, mkasema kwamba hatutazami kwamba huyu anatoka Zanzibar, huyu anatoka Tanzania Bara, hili hatukubali mko milioni 40, tuko milioni 1.5 ushirika huo mgumu, tunataka nafasi za Zanzibar zieleweke. Hatuwezi kuchanganyika na watu milioni 40. Uganda ilishauriwa Muungano huu ikakataa, Kenya ilikataa na Baba alisema Makao Makuu pale mnahakikisha ujavisilu mlifanya kwa kuungana na nchi kubwa kama hii, tutahakikisha kwamba hatutakumezeni, hivyo linakwenda viper?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa chombo kimoja cha Muungano kinaegamia upande mmoja, tutafika wapi? Kizazi chetu kinachokuja kitafika wapi? Kizazi chetu kinachokuja tunajua mbele nani atakuwa mtawala? Tunasema nafasi Zanzibar zieleweke, tuje kwamba haki za wananchi wa Zanzibar. Leo mnafanya mbinu, mnasema nafasi zitataka JKU na JKT, leo mnachukua mnapeleka JKT, wale kule JKU Zanzibar wote mtawaweza kweli? Mbona wenzetu mnakwenda kinyume? Hapa nilijibiwa swali niliuliza, wenzetu mnatuendea kinyume, tunasema wakati agizo linatoka kwa JKT na JKU, JKT iko Tanzania Bara, JKU kwa Zanzibar leo mnapanga mipango wote mwalete JKT, maana yake nini? Mbona mnatufanya hivi jamani? Hebu tufike mahali tuelewane, kuna tatizo gani, kisiwa kile?

Mimi nasema *wallah, wallah*, kama siyo Muungano, kisiwa kile nasema sisi tungekuwa mbali. Mimi nakwambieni, msitudanganye hapa, hata nchi hii tuseme misaada iliyopo kama sisi tungejitegemea unafikiri tungekuwa wapi? Nchi zote zitakwenda viper? Sisi tulikuwa na bendera yetu kimataifa, tuache mambo haya, hatuwezi kuitupa nchi! Leo sisi nchi mkasema tunaipoteza, hatukubali suala hili! Sisi ndiyo wa kusema wenyе umri huu, hamna humu wa kusema kwa sababu hao waliobaki wote hawakufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafahamu majumba ya michenzani, yale mimi nimejenga niko shule, najitolea. Yale majumba ya michenzani, niko shule najitolea, nainua tofauli, napeleka juu. Sasa hapa, hapana! Kizazi kiliopo sasa hakielewi hayo! Sisi ndiyo tunaoelewa na sisi kama hatutasema hapa, atasema nani? Nani atakwenda kusema hajui, hana historia yoyote? Nasema, jamani Muungano una maana sana. Mimi nasema hivi, nilishazaa Bara, sifichi na kama Muungano, mimi ndiye niliyefanya Muungano kwa sababu kizazi hiki hakiondoki, milele itakwenda *generation* na *generation*. (*Makofi*)

Lakini tuelewe kwamba nchi aliyetawala leo siye atakayetawala kesho. Tunawaona wenzetu Sudan, tunawaona wenzetu na nchi nyingine, mko milioni 40 tuko milioni 1.5 hakuna hata utaratibu wa kuingia katika nchi, hakuna. Lazima tutafute taratibu. China tunayo hapo, Hong Kong, huingii Hong Kong kama huna utaratibu maalum, na ndiyo leo tunapata majambazi, tunauliwa sisi, imani ile hatukuizoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulikuwa tunalala nje, gari unaweka nje, honda unaweka nje, juzi kakamatwa jamaa pale na bangi, anatoka huku huku! Tunakwenda wapi? Tunasema tunataka Muungano, tuna nia nzuri, udumu Muungano Mungu na atujalie, lakini matatizo myaondoe. Waziri unanisikia, japokuwa unazungumza, Waziri

nataka kuhakikisha kwamba haya tunayoyasema sasa tusije kuzungumza tena, tuzungumze mengine ya kuendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono kutokana na matatizo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru kwa kuokoa muda wetu. Naomba niwataje watakaoongea tena hapa, tuna Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Deo Filikunjombé, Mheshimiwa Abdul Mwalombwa, Mheshimiwa Asaa Hamad na Mheshimiwa Simbachawene, wajiandae. Sasa tutaanza na Mheshimiwa Said Amour Arfi.

MHE. SAID A. A RFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami niweze kuchangia hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake na fadhila zake nyingi juu yangu. Kadhalika, kwa sababu ndiyo mara yangu ya kwanza kuzungumza ndani ya ukumbi huu kwa kipindi hiki, nawashukuru sana ndugu zangu wapendwa wangu wakazi na wananchi wa Jimbo la Mpanda Mjini kwa imani kubwa waliyokuwa nayo juu yangu na kunirudisha kwa kipindi kingine cha pili. Ninawaahidi kuwatumikia kwa uadilifu mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Mpanda ni miongoni mwa Halmashauri nyingi katika nchi yetu. uwezo wa Halmashauri hii ni mdogo sana ni asilimia nne tu ya mapato yote ambayo Halmashauri inaweza kuchangia. Ni Halmashauri ambayo haiwezi kuijidesha, ni Halmashauri ambayo inategemea sana mchango mkubwa wa Serikali Kuu kwa maana ya asilimia 96. Lakini inasikitisha, inasikitisha kama jinsi dereva wa taxi aliposimama kwenye Kituo cha Mafuta akaona gari tanki la mafuta limepakia lita 12,000 na lenyewe limesimama kwenye Kituo cha Mafuta akajiuliza, gari hili lina lita 12,000 na bado limesimama kwenye Kituo cha Mafuta, linatafuta mafuta na wakati lina mafuta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hukuweka mafuta kwenye tanki la chini, gari haiwezi kupeleka yale mafuta. Kama Serikali Kuu pamoja na fedha zote walizokuwa nazo hawatazipeleka kwenye Halmashauri hakuna maendeleo hata kidogo. Nasema hivyo kwa sababu katika makisio ya bajeti iliyopita, Halmashauri yangu ya Mji wa Mpanda ilikuwa makadirio yake ni kupata Sh. 1,809,801,855/= lakini mpaka tarehe nilipolazimika kuahirisha, nisihudhurie vikao vya Kamati Dar es Salaam nisubiri kikao cha *finance* ili niweze kujua tumefikia wapi katika mapokezi ya fedha? Inasikitisha sana.

Katika makadirio hayo, shilingi trilioni 1,800 mpaka mwezi Mei. Halmashauri ya Mji wa Mpanda ilikuwa imepokea kama shilingi milioni 859 na kidogo, sawa sawa na asilimia 48 ya makadirio yote. Kwa maana hiyo, hata yale malengo na mikakati ya miradi ya maendeleo haikuweza kukamilika, na hali hii siyo kwa Halmashauri ya Mpanda peke yake ni kila mahali, kila Wizara imepata fedha pungufu ya makadirio yaliyokuwa yameidhinishwa na Bunge. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu huo wa fedha unaathiri sana miradi mingi ya maendeleo, kwa mfano, makadirio ambayo tulikuwa tunahitaji katika Halmashauri ya mji

wa Mpanda kutoka kwenye Mfuko wa Barabara tu (*Road Fund*), ni shilingi milioni 322. Tumeletewa shilingi milioni 32, matokeo yake ni nini? Tutakuwa tunazungumza tarakimu ambazo zitawapa matumaini makubwa sana Watanzania, tunazungumzia bajeti ya shilingi trillioni 14, kiuhalisia haifiki bajeti ya shilingi trillioni 14. Kwa mtindo huu wa kupeleka mpaka akanunue *quarter* ya pili ya bajeti chini ya asilimia 50, hatuwezi. Tunawadanganya Watanzania, tunawapa matumaini Watanzania, lakini uhaliisa ni kwamba maendeleo yatachelewa sana kwa stahili ambayo mnaitumia kupeleka fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni pale Serikali ilipokubali kwamba itatoa fidia katika Halmashauri zetu zote za mapato. Halmashauri yangu ya Mji wa Mpanda ilikuwa inakadiriwa kupata shilingi milioni 26 na kidogo kila mwezi kutohana na fidia ya mapato. Lakini mwezi Aprili imepelekewa shilingi milioni tano, hatuwezi kwenda stahili hii. Hili jambo linasikitisha. Naiomba Serikali kuitia Ofisi ya Waziri Mkuu wajaribu kuangalia ni namna gani fedha hizi zinapelekwa kwa wakati ili miradi iliyokusudiwa iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo lilikuwa ni eneo moja. Maendeleo hatuwezi kuyapata kwa kasi tunayoitarajia, moja likiwa ni hilo. Lakini la pili, tunaporejea taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, inaainisha bayana ni namna gani kuna upotevu mkubwa wa fedha za umma. Upo wizi, upo ubadhirifu, upo udanganyifu, upo utuzaji mbaya wa vitabu, kutokuwepo kwa nyaraka sahihi na kadhalika na kadhalika. Lakini cha ajabu ni kwamba pale Mkaguzi anapokagua na hakuna viambatanisho anashindwa kuchukua hatua, anawapa muda wahusika watafute viambatanisho.

Jambo hili ni la ajabu na linafanyika katika nchi hii tu, na kama tutaendelea, kwa hali hii na kwa stahili, kila siku wataendelea kuiba hela na hakuna chochote mtakachokifanya. Ni lazima tubadilike, tuchukue hatua mara tunapogundua upotevu, basi hatua za kinadhamu na kisheria ni lazima zifuatwe. Kwa kufanya hivyo, naamini kabisa tutakwenda mbele, kwa sababu hata hizo hatua zinazochukuliwa haziwatii moyo wala haziwafurahishi Watanzania kabisa. Ni lazima twende mbali zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya hayo, yako matumizi mabaya sana ya mali za Serikali, mfano ambao nataka kuutolea ni vyombo vyaa usafiri, magari, magari yanayoletwa katika Halmashauri zetu. Kwa mfano, magari ya mradi ya maji, hayatumiki katika miradi iliyokusudiwa, gari za kubebea wagonjwa, *ambulance* katika Halmashauri yangu tunayo *ambulance* kwa ajili ya *town clinic*. Gari ile imekwenda kuwekwa kwenye Ofisi ya Mkurugenzi, kazi yake ni kumpeleka Meya na Mkurugenzi nyumbani kwao, ndiyo makusudio ya *ambulance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Serikali iagize kwamba kuanzia sasa ile gari inahama, inakwenda kukaa kwenye Kituo na inasimamiwa na Mganga wa Kituo na siyo Ofisi ya Mkurugenzi au Daktari wa Mji. Kwa kufanya hivyo, tutajua matumizi ya magari,

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajitahidi, lakini nani anayesimamia? Matumizi ni mabaya ya vyombo vyaa umma. Naomba eneo hili liangaliwe na lisimamiwe

na litolewe kauli kali, magari ya miradi yatumike kwa ajili ya miradi na siyo kwa ajili ya kuwasafirisha maafisa wa utawala katika Halmashauri zetu. Mtindo huo naomba ukome. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa eneo lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia, ni suala la uwekezaji. Suala la uwekezaji ni dhana ambayo imejengwa na tunaamini kabisa kwamba hatuwezi kuendelea isipokuwa ni lazima tuwaite wawekezaji. Jambo hili halikubaliki. Nchi zote zilizoendelea zimewategemea watu wake, India ni mfano, China ni mfano, nchi za mashariki ya mbali zote zimendelea bila msaada wa Wazungu. Sisi leo badala ya kuwaendelea watu wetu, tunafikiria kuwaleta Wazungu katika nchi yetu waje wachukue ardhi zetu. Jambo hili halikubaliki.

Mfano mzuri ni uwekezaji mkubwa wa kilimo unaotaka kuwekwa katika Wilaya ya Mpanda. Jambo hili mimi sikubaliani nalo na wala sitaki kuwa sehemu ya watu wanaowadhulumu watu wa Mpanda ardhi yao. Uwekezaji ambao hauna tija, uwekezaji ambao unaangalia sijui maslahi ya nani, haiangalii maslahi ya watu, mpango mzima unasikitisha.

Tunazo nyaraka, tunafahamu, tozo ambalo anataka kutozwa Mzungu ni Sh. 200/= kwa ekari, Sh. 500/= ushuru wa Halmashauri, Sh. 700/=, Sh. 700/= zitatusaidia nini Watanzania? Tuna mgogoro mkubwa ndani ya nchi yetu, maamuzi hayachukuliwi, wakulima na wafugaji wanagombana, ardhi tunataka kumpa Mzungu badala ya kuwapa wafugaji wetu ambao wanahangaika kila kukicha. Jambo hili kwa kweli naomba wanaohusika na hasa Ofisi ya Waziri Mkuu iingilie kati ihakikishe kwamba jambo hili wanalinzia. Ardhi hii wapewe hata hao wafugaji, watalipa hizo shilingi 700 ambazo wanataka kumdati Mzungu. Kwanini tunashindwa kuwaangalia watu wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunafikiria suala la uwekezaji, sipingi kuwepo na uwekezaji, lakini ni lazima uwekezaji uwe na tija na faida, siyo kwa stahili hii ya kudai tozo la Sh. 200/= na ada ya Sh. 500/=, haikubiliki na mimi sitaki kuwa sehemu ya ufisadi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Chuo cha Afya Mpanda. nimezungumzia kwa miaka mitano mfululizo Mpango wa Serikali wa Maendeleo ya Afya ya Msingi unasisitiza pia kuwepo kwa wataalam. Wataalam hauwezi kuwapata kama vyuo hivi hamjaviendesha, hamjaviwezesha kwa miaka mitano mfululizo. Nimekuwa nikisemea Chuo hiki kiweze kuanza kufanya kazi na kutoa wataalam, mpaka leo bado hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Inasikitisha na inaumiza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nafikiri pia lina upotevu mkubwa wa fedha za umma ni maonyesho ya Nanenane. Leo kama unakwenda Dar es Salaam ukipita pale Nanenane, nenda kaangalie majengo yaliyojengwa pale, mwaka mzima yanakaa, hayatumiki, yanangojea tarehe 8/8. Wanaoonyesha maonyesho hayo ni watu wa Dodoma Mjini, Mbeya Mjini, Arusha Mjini, Dar es Salaam lakini siyo wakulima. Majengo yale yamegharimu mamilioni, ofisi zote zimejengwa pale lakini wanaonufaika ni watumishi wanaokuja, wanalipwa posho, wanakaa pale wakati wa wiki ya maonyesho

lakini hakuna tija kwa mkulima tunayemsemea ambaye yuko kijijini. Majengo yanajengwa mijini na baada ya kujengwa hayatumiki ipasavyo. Hizi fedha tunazichezea, tuna matatizo ya maabara katika shule zetu, kila Shirika na Idara iliyojenga banda pale, fedha waliyotumia wangeambiwa wajenge maabara, kila shule leo ingekuwa na maabara. Hela tunazichezea kwa maonyesho yasiyokuwa na tija kwa mtu tunayemkusidia, yana faida lakini haimgusi mkulima moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofî*)

MWENYEKITU: Ahsante sana, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Deo H. Filikunjombe!

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii adimu ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba niwashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Ludewa kwanza kwa imani kubwa waliyonayo kwangu mimi kama Mbunge wao lakini pili kwa ushirikiano wao wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Napenda kuwahakikishia wananchi wa Ludewa kwamba yale ambayo niliyaahidi, nitayatekeleza. Kwa niaba ya Viongozi wenzangu wa Serikali pamoja na Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa pamoja na Chama changu, Chama cha Mapinduzi, napenda kuwahakikishia kwamba yale ambayo tuliyaahidi tutayasimamia na kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza kwa upana sana kuhusu maendeleo ya nchi yetu kwa miaka mitano ijayo. Zimetajwa sababu na changamoto mbalimbali lakini mimi napenda kuitazama changamoto moja kubwa ya kwanza ya watumishi wetu ambao wanafanya kazi hasa wale wa Kada ya Chini, ni lazima Serikali iwatazame kwa jicho zuri zaidi katika kuwaboreshea maslahi yao pamoja na mishahara yao. Nayasema hayo kwa dhana kwamba huwezi kumkamua ng'ombe maziwa kama humpi majani ya kutosha. Watumishi wote wa Kada ya Chini ukilinganisha mishahara yao pamoja na Watumishi wa Kada ya juu haiendani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupa mifano miwili tu ambayo nimekuwa nikiisitiza mara kwa mara. Mfano wa kwanza ni Askari wa Jeshi la Polisi. Mshahara wanaopata Askari Polisi ni mdogo sana ukilinganisha na majukumu makubwa ambayo wamepewa. Askari wetu hasa wa Kada ya Chini wanapata mishahara midogo. Naiomba Serikali yako Tukufu iwatazame kwa jicho la huruma ili waweze kutumikia nchi hii ipasavyo vinginevyo tutakuwa tunawatia kwenye majaribu, kila siku tunawalaumu kwamba wanaingia kwenye rushwa kumbe kosa ni la kwetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haiwezekani kuongeza posho au mishahara ya Askari Polisi basi naiomba Serikali itekeleze kile inachopaswa kufanya. Hivi navyozungumza Askari wanakopwa haki zao, Askari wanahamishwa hawalipwi mishahara wala posho zao. Askari wanaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni 10,

haiwezekani Askari umpe bunduki halafu umkope haki yake. Kwa hiyo, naisihi sana Serikali yako Tukufu iwatazame Askari Polisi kwa jicho la upendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili ni Madiwani na nimekuwa nikilisema hili mara kwa mara kila napopata fursa ya kuchangia. Sote tunafahamu kabisa kwamba Madiwani ni nguzo muhimu na wao ni watu muhimu sana kwenye kusimamia maendeleo kwenye Kata zetu mpaka vijijini na sisi tunakuwa mbele mara kwa mara hasa tunapoomba kura tunapita vijijini na kwenye Kata zetu tukisisitiza mafiga matatu leo tupo madarakani tunahudumia vizuri mafiga mawili tu figa moja la Madiwani tumelisahau na tumelitekeza. Tunaomba Madiwani watazamwe kwenye maslahi yao kwa vile mazingira wanayofanyia kazi ni magumu sana. Kwa mfano, Diwani wa Ludewa ambaye yuko Kata ya Lwilo ili kusudi aende kijiji cha Liugawi anapaswa kutembea kutoka Lwilo mpaka Liugawi kwenda na kurudi ni kilomita 24. Diwani wa Iywela ili atoke Mkomang'ombe mpaka Iwela na usafiri hakuna anapaswa kutembea zaidi ya kilomita 40. Diwani wa Ibumi ili aje Ludewa anapaswa kutembea kwa miguu kwani usafiri hakuna zaidi ya kilomita 120, Diwani huyu hawezi kuwa na ufanisi mzuri katika kutekeleza majukumu yake. Kama haiwezekani kuwaongezea posho na kuwaboreshea maslahi yao basi Serikali walau iwatazame kwa jicho la huruma Madiwani hawa ikizingatiwa utendaji na umuhimu wao katika nyanja ya mafiga matatu walau kwa kurekebisha na kuboresha tu hata sheria zilizopo. Shelia ya Fedha ibadilike, Shelia za Serikali za Mitaa zibadilike ili Madiwani nao waweze kukopeshwa vyombo vyta usafiri kama wanavyokopeshwa Wabunge pamoja na Mawaziri. Hiyo ilikuwa ni upande wa Maslahi ya Watumishi wa Kada ya Chini. Mimi namshukuru Mheshimiwa Waziri kwenye majibu yake amesema kwamba walau hili watalifikiria lakini unaposonga ugali ni lazima maji yachemke basi maji hayo yachemke upesi kwa sababu maendeleo hayawezhi kusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake ametaja Liganga na Mchuchuma lakini ndani ya Bunge lako Tukufu toka tumepata uhuru, kama kuna eneo ambalo linaongoza kutajwa mara kwa mara hata ukiangalia *Hansard*, ni Liganga na Mchuchuma. Muda umefika sasa Liganga na Mchuchuma visiwe vinatajwa tu, hiyo haitoshi, Liganga na Mchuchuma ifanyiwe kazi kwa maslahi ya Watanzania wote na kwa maslahi ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tunakaa kwenye giza na kwenye mazingira magumu. Mwenyezi Mungu anatushangaa, rasilimali tunayo lakini tunabaki kulalamika na kila mmoja analalamika, tufike mahali sasa tuchukue maamuzi magumu, tutekeleze mradi wa Liganga na Mchuchuma uweze kuwanufaisha wana Ludewa na Watanzania wote kwa ujumla wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Liganga na Mchuchuma peke yake *investment* ikifanyika pale, zaidi ya trilioni 10, itaongeza kipato cha zaidi ya 25% kwenye *GDP* ya Taifa. Leo hii Mheshimiwa Waziri Mkuu anazungumzia Liganga na Mchuchuma na ukitazama tunasema mwekezaji amepatikana, mwezi Januari 2011 lakini barabara ya Njombe - Ludewa haitengenezwi, barabara ya Njombe – Manda haitengenezwi, barabara ya kutoka Njombe – Lupingu hazitengenezwi kwa kiwango cha

lami. Mradi huu hauwezi kuwa na manufaa kwa Watanzania kama hatuwezi kutengeneza barabara hizi ili Watanzania kutoka maeneo mengine kama Kilimanjaro, Njombe na kutoka ndani ya Wilaya ya Ludewa waweze kunufaika na fursa zile. Naisihi Serikali iwe makini kwenye uwekezaji wa madini, tujifunze kutokana na makosa yaliyopita, turekebishe, tuandae miundombinu, tupange, tupime viwanja vyetu ili Ludewa ikifika mahali...

(Hapa Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said aliishiwa nguvu ndani ya ukumbi wa Bunge)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, samahani kidogo naona kuna Mgonjwa pale, naomba apewe huduma ya kwanza. Mheshimiwa Mbunge, naomba ukae kwanza. Tafadhali naomba apewe msaada unaostahili.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge endelea!

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali yako ambayo imekuwa ikitoa ruzuku kwenye pembejeo ili kuweza kuboresha na kuwasaidia wakulima wetu kule Ludewa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, naomba usubiri kidogo, naomba mgonjwa apewe huduma inayostahili.

MBUNGE FULANI: Yuko Daktari anamhudumia!

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa leo la mwananchi wa Ludewa siyo pembejeo wala siyo *power tiller*, mwananchi wa Ludewa leo anahitaji uhakika wa soko la mazao yake. Napenda nikuhakikishie kwamba wananchi wa Ludewa leo wakihakikishiwa kwamba soko la mahindi lipo, watalima kwa kiwango kikubwa sana kuliko wanavyozalisha sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde.

MWENYEKITI: Tunaotoa huduma kwa mgonjwa tufanye haraka, Mheshimiwa Mbunge naomba uendelee.

(Hapa Mheshimiwa Mwanahamisi Kassim Said Aliondolewa Ndani ya Ukumbi wa Bunge)

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini dakika zangu umenitunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuwakumbuka na kuwathamini wananchi kwa kuwapatia mbolea ya ruzuku lakini mkulima wa Ludewa, shida yake kubwa si punguzo la pembejeo wala siyo apewe mkopo wa *power tiller*. Mkulima wa Ludewa leo ili kusudi alime na kuzalisha kwa kiwango kikubwa, anahitaji uhakika wa soko. Kwenye suala hili Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alipokuja Ludewa alizungumza na wakulima, wakulima walimwomba soko la kununua mahindi lisogee jirani yao yaani kutoka Shaurimoyo na kutoka Mlangali na hivyo ununuzi wa mahindi uweze kufanyika Ludewa Kijiji au Mjini, Mheshimiwa Rais alikubali ombi hilo lakini mpaka navyozungumza kutoka mwaka 2008 mpaka leo hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wepesi sana kuwalaumu wenzetu wa upinzani kwamba wana macho hawaoni, wana masikio hawasikii lakini napenda kusema kwamba hata ndani ya Chama na Serikali yetu kuna Watendaji wana masikio hawasikii na wana macho hawaoni. Haiwezekani Mheshimiwa Rais atoe maagizo na atoe ahadi halafu Watendaji wake hawatekelezi. Watendaji hawa wanataka kuwaambia nini wananchi wa Ludewa? Soko la Mlangali ili kusudi mkulima wa Mkomang'ombe na Ibumi aweze kusogeza mazao yake labda ana magunia 15 au 20 ni zaidi ya kilomita 120 kutoka Mkomang'ombe kitu ambacho mkulima wa kawaida hawezi kukifanya. Rais amewasikia wananchi wa Ludewa, amekubali kwamba atawaleta soko Ludewa Mjini au Kijiji lakini Watendaji hawatekelezi. Kwa hiyo, nakuomba, Serikali yako ilitazame hili kwa umakini zaidi ili kuweza kuwapatia unafuu wa maisha wananchi wote wa Ludewa Kijiji kutoka Ibumi na maeneo yote ya Mkomang'ombe hasa ikizingatiwa kwamba ilikuwa ni ahadi ya Rais kutoka mwaka 2008 ambayo haijatekelezwa mpaka leo. Itafika mwaka 2015 tutatumia fedha nyangi za umma kufanya utafiti, kwa nini tumepata kura chache au kwa nini baadhi ya maeneo tumeshindwa lakini baadhi ya makosa tunayafanya sisi wenyele tulipo madarakani. Tunaahidi lakini hatutekelezi, tufanye maamuzi magumu, tutende yale ambayo tunayaamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa miaka Mitano wa Maendeleo, Tanzania tuna maziwa matatu yaani Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika ambayo ndiyo maziwa makubwa lakini ndani ya Mpango ule unazungumzia kuendeleza na kujenga magati Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria peke yake lakini Ziwa Nyasa limeachwa. Sasa kwa miaka mitano unamwambia nini mwananchi wa Ziwa Nyasa yaani mwananchi wa Manda, Kilondo, Lumbila, Makonde na mwananchi wa Lifuma?

Mheshimiwa Rais alipokwenda kwenye kampeni aliahidi kupeleka meli ya tani 400 hivi, hii meli itapita wapi lakini vilevile Mpango hautambui. Hata Mpango wa mwaka huu Ziwa Nyasa haimo, kwenye miaka mitano pia haimo na Rais ameahidi kupeleka meli ya tani 400 hii meli itapita wapi? Kwa hiyo, mimi nakusihi sana na ninaisihi Serikali yetu kwamba ifike mahali tuwe makini na utekelezaji wa yale tunayoyaahidi na kuwaambia wananchi. Tutafika mahali tutaanza kutafiti kwa nini tumeshindwa kumbe kinachotufanya tushindwe ni sisi wenyele na siyo Wapinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Miaka Mitano hautambui Ziwa Nyasa na tuna maziwa matatu, huu ni upendeleo. Haiwezekani wananchi wa Ziwa Nyasa wanabaguliwa. Kwa hiyo, kwa miaka mitano watakuwa hawana kitu. Naiomba Serikali

yako Tukufu ilizingatie hilo, iweze kuliingiza kwenye Mpango wake ili kuleta unafuu wa maisha na ubora wa maisha siyo kwa wananchi wa Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika peke yake, bali kwa wananchi wavuvi kutoka Ziwa Nyasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naogopa sana kwamba hii ahadi ya Rais kwa Mpango huu uliopo sasa itakuwa haitekelezeki kwa sababu kama hatujengi gati wala bandari meli itasimama wapi?

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge tunakushukuru sana.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde muda wangu ulipotea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, ulihifadhiwa na saa ilikuwa imesimamishwa, kwa hiyo, muda umekwisha, tunakushuru sana.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYYEKITI: Anayefuata ni Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Awali ya yote, naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kibiti kwa imani kubwa waliyoonesha katika uchaguzi wa mwaka jana 2010. Walinipatia kura nydingi na mimi naahidi sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii kwanza niangalie dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nne ambayo ilikuwa ni kutaka kuleta maendeleo katika Mikoa ile ambayo kwa sasa iko nyuma. Dhamira hiyo ilikuwa ni kuleta uwiano wa maendeleo katika nchi yetu lakini jambo la kushangaza katika bajeti ya mwaka huu ile Mikoa ambayo ilitajwa kwamba iko nyuma kimaendeleo na ambayo ilitakiwa iongezwe nguvu ili iweze kupata maendeleo kama inavyopata Mikoa mingine, katika bajeti kwa kweli haikupewa kipaumbele hicho. Mkoa wa Lindi ambao fedha za maendeleo umepewa shilingi bilioni 20 pamoja na Mkoa wa Pwani, ni Mikoa miwili ambayo ni duni sana, miundiombinu yake ni mibaya na maendeleo yake kwa ujumla si makubwa lakini ndiyo Mikoa ambayo inaoongoza kwa kupata fedha ndogo za maendeleo. Kwa hili nitamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anahitimisha atueleze kwa nini hii Mikoa miwili ambayo ni duni kimaendeleo bado imepewa kasma ndogo sana ya fedha kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika hilohilo, Wilaya ya Rufiji ni kubwa sana na katika Mkoa Pwani ndiyo inayoongoza hasa kwa upande wa umaskini. Wilaya hii ina

eneo ambalo halifikiki, eneo la Delta. Ni eneo kubwa, lina urefu wa kilomita 70 na upana wa zaidi ya kilomita 50, ukiangalia *square* kilomita za eneo lile ni 3500 lakini eneo hili kwa muda mrefu Serikali haijaweka mkakati wa kutaka kuliendeleza. Ni eneo tajiri sana kwa upande wa samaki aina ya Kamba, 80% ya Kamba wa Tanzania wanatoka katika eneo hili. Eneo hili ni zuri sana kwa miti ya mikoko, zaidi ya 70% ya miti ya mikoko katika nchi yetu inatoka katika eneo hili. Ni eneo zuri sana kwa kilimo, sehemu kubwa ya chakula cha watu wa Wilaya ya Rufiji inatoka kwenye eneo hili la Delta, lakini halifikiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006 Waziri Mkuu aliyejita, Mheshimiwa Edward Lowassa, samahani kwa kumtaja jina, aliamua kwa makusudi namna ya kuliendeleza eneo hili na alipanga utaratibu wa kuwatafuta katika Wizara zote wawakilishi wa kwenda kuangalia mahitaji maalum ya watu wanaoishi katika eneo lile kwa sababu kuna wakazi zaidi ya 40,000, kuna shule za msingi zaidi ya 20, kuna zahanati zaidi ya 20, je, watu wa kule watapata huduma za jamii kwa kutumia njia ipi? Aliamua kuunda timu kutoka Wizara ya Elimu, Miundombinu, Maji, Afya na zile Wizara zote zinazohusika wapite katika maeneo yale ili waangalie ni kitu gani ambacho wananchi wa kule wanahitaji kwa sababu zaidi ya elimu na afya, hakuna huduma nyingine zozote za jamii ambazo zinapatikana katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana mkakati ule haukukamilika na mpaka sasa hivi bado Wizara na hasa Ofisi ya Waziri Mkuu hajifuatilia. Mimi namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 10 mwezi wa pili alipokwenda kutembelea ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Nakayama pale Nyamisati, alisema na aliagiza wasaidizi wake kwamba atakapokwenda katika Wilaya ya Rufiji kufanya ziara basi ataanza na eneo la Delta. Sasa hii ni ahadi ya Rais anataka kwenda kuangalia nini kinachoendelea kule, nilikuwa namwomba Waziri Mkuu na wasaidizi wake basi wao *wa-pave way* ya Rais kwenda kule. Waende wakaangalie waone ni namna gani ya kuweza kuwasaidia wananchi hao wanaoishi katika mazingira magumu, hawana maji safi, *dispensary* nzuri, watumishi hawaendi, kuna kila aina ya mabaya ambayo yako katika maeneo yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alifuatilie suala hili na hasa kwa kuzingatia kwamba Naibu Waziri wa TAMISEMI anayeshughulika na Wizara ya Elimu alikuwa *DC* wa Wilaya ile, mimi nadhani atatoa picha nzuri zaidi kwa Wizara hii ili kuweza kuwasaidia wananchi wale wanaoishi katika mazingira magumu kule Visiwani. Eneo hili la Visiwani lina matatizo makubwa sana. Wakati wa ukoloni magari yalikuwa yanafika Mbwera ambako ndiyo Makao Makuu ya Tarafa, lakini baada ya uhuru magari hayafiki Mbwera, hivi tatizo ni nini? Naomba yale maeneo ambayo kwa bahati mbaya barabara zimekata, kuna madaraja makubwa matatu; kuna daraja la Mbelambe ambalo linaunganisha Mbwera, kuna daraja la Kipoka, kuna daraja la Usimbe, tumeomba katika *RCC* kwamba maeneo haya yaweze kupatiwa fedha za ziada ili tuweze kufika kwa urahisi eneo la Delta. Kama tukiyajenga madaraja haya na tukaimarisha barabara hizi, kwa kweli usafiri wa Delta utakuwa ni mzuri na wananchi wa kule watafurahia matunda yao ya uhuru. Wakati wa ukoloni hili liliwezekana, sasa hivi tunashindwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la matumizi ya fedha za Serikali hasa za TAMISEMI. Kuna matatizo makubwa sana ambayo yanajitokeza hasa kwa wenzetu wa Idara ya Ukaguzi. *CAG* anapokagua vitabu vyake, anatueleza wazi kwamba kuna matumizi mabaya ya fedha katika Halmashauri zetu. Namshukuru Waziri Mkuu ameamua, katika taarifa yake amesema kwamba anataka kuwapatia semina Waheshimiwa Madiwani, kuhusiana na namna ya kuendesha Halmashauri hizi lakini tatizo haliko kwa Madiwani, tatizo liko kwa watumiaji. Fedha hizi za Serikali zinakwenda moja kwa moja vijijini, haziendi kwa Madiwani, Madiwani wao wanapeleka cheki kule vijijini, vijiji ndivyo vinavyotumia. Je, Serikali imewaandaaje hawa wanaotumia fedha hizo za Serikali ili waweze kuzitumia vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kama kuna uwezekano basi ni vizuri sana tukaweza kuwapatia mafunzo ya kiuhasibu Watendaji wa Vijiji kwa sababu katika vijiji vyetu hatuna Wahasibu. Tukiweza kuwapatia mafunzo ya kiuhasibu namna ya kutumia vizuri fedha hizi za Serikali, fedha zitatunzwa vizuri. Baada ya kupata mafunzo hayo, nina imani wanaweza kutumia fedha zetu vizuri na hizi ripoti mbaya za ukaguzi zinaweza zikakosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la Idara ya Elimu, hasa Kitengo cha Ukaguzi. Idara ya Elimu ndiyo Idara ambayo kwa kiasi kikubwa inasimamia maendeleo yote, huwezi kuendelea bila kuwa na elimu. Kwa bahati mbaya Serikali yetu imewaweka nyuma Wakaguzi ambao ndiyo wenyewe jukumu la kuangalia mwenendo mzima wa elimu, wao ndiyo wanaojua kwamba sasa hivi tunakwenda mbele au tunarudi nyuma. Kwa miaka mingi Idara hii wanapata fedha za kuombaomba tu, leo wanapewa shilingi milioni moja na Mkurugenzi, kesho wanamfuata *DC* kumuombahela ya kwenda kukagua mahali fulani, hawana kasima maalum ya kazi zao. Mwaka huu Serikali ilianza mchakato wa Idara hii kuweza kupata fedha zao moja kwa moja katika Halmashauri zao za Wilaya, lakini bahati mbaya Wizara ya Elimu imeamua fedha zile za ukaguzi zote zipelekwe kulekule Wizara ya Elimu wao ndiyo watoe hizo nusunusu, elimu yetu tunaipeleka wapi? Wakaguzi hawa watafanya nini? Wataendelea kuomba mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Idara ya Ukaguzi ipewe mafungu yake ya pesa ambayo yatawawezesha wao wenye kujipangia kwamba leo wanakwenda kukagua sehemu fulani, kesho wanakwenda sehemu nyingine lakini wakiendelea kuombaomba, hawatafanikiwa. Wana gari halina mafuta, wana gari linatakiwa lifanyiwe *service*, lazima wamwombe Mkuu wa Wilaya au Mkurugenzi, siyo vizuri. Bila Idara ya Ukaguzi elimu haiwezi kuwa nzuri. Naomba ile kasma ya Idara hii ya Ukaguzi ipelekwe moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ili fedha hizo ziweze kuwasaidia wale Wakaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais mwaka 2005 alipokuwa anatembelea Wilaya ya Rufiji, aliahidi kujenga kwa kiwango cha changarawe barabara ya kutoka Kibiti – Rwaruke – Nyamisati. Ahadi hii ya Rais kwa miaka sita (6) imetekelezwa kwa kujenga kiwango cha changarawe kilomita tisa (9) tu na barabara hii ina kilomita 42. Hivi ni muda gani utatumika kukamilisha

barabara hii, mpaka Rais aweze kustaafu kweli? Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu iliangalie hilo iweze kurekebisha barabara hiyo iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la pembejeo za kilimo. Wilaya ya Rufiji tumenufaika sana mwaka jana kwa stakabadhi ghalani. Kwa mara ya kwanza korosho katika Wilaya ya Rufiji ilifikia shilingi 1700/= kwa kilo, wakati bei ya *dealer* ilikuwa ni shilingi 800/=. Watu wamehamasika, wamelima sana korosho bahati mbaya mwaka huu mpaka hivi tunavyozungumza pembejeo zile za kupulizia korosho ambayo ni *sulphur* haijapatikana na wakati huu ndiyo wa kupulizia dawa. Hivi Serikali inatwambia nini? Kweli inataka kuendeleza zao hili la korosho au inataka kuwakandamiza wakulima wake? Hivi Serikali hawajui ni wakati gani wa kupulizia korosho? Naomba suala hili lishughulikiwe kwa haraka, wananchi wanahitaji *sulphur*, mpaka leo *sulphur* haijapatikana, mikorosho inakauka, tunawarudisha nyuma wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Wilaya ya Rufiji tuliomba toka mwaka 2007, kwamba tuna Vituo vyetu vya Afya tumevianzisha, tuna Zahanati zetu, kila mwaka Wizara ya Afya wanatwambia tumetenga fedha za dawa, kutoka mwaka 2007, huu sasa ni mwaka 2011 bado vituo hivyo havijapewa fedha za kununulia dawa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunakushukuru, sasa hivi tutakuwa na wachangiaji wawili kama muda utaruhusu. Tutakuwa na Mheshimiwa Azza H. Hamad na Mheshimiwa George B. Simbachawene, tunaanza na Mheshimiwa Azza Hamad.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu ili nami niweze kuchangia kwa mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa afya ya kutosha hatimaye leo nimesimama ndani ya Ukumbi huu. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuongea, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Wanawake wa Mkoa wa Shinyanga, kwa kuniamini na kuweza kunichagua ili niweze kuwawakilisha, naahidi sitawaangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nianze kwa kusema hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nzuri, inasomeka vizuri na imepangika. Pamoja na mazuri yote hayo, nitakuwa sijawatendea haki wananchi wa Shinyanga kama sitaanza na suala la njaa, kwa sababu yote haya hayatafanyika kama tumboni hakuna kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kabisa Mkao wa Shinyanga hali ya hewa imekuwa ikisuasua kwa miaka kadhaa sasa, tutakuwa tunaomba chakula cha njaa mpaka lini? Ni afadhalii miaka mingine wanaokutwa na tatizo hili wanakuwa ni wachache. Kwa sasa hivi ukifika Mkao wa Shinyanga, nitoe mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, debe la mahindi linauzwa shilingi 10,000/= na ndiyo msimu wa mavuno. Gunia la mpunga linauzwa shilingi 60,000/= mpaka 70,000/= ndiyo kipindi cha mavuno, tunategemea mwezi wa kumi na mbili, wananchi hawa wanaishi maisha gani? Sijui mpaka sasa hivi Serikali ina mpango gani pamoja na kilio hiki ambacho kila Mbunge anayesimama anazungumzia suala hili mpaka wanaotoka Mikoa mingine wanatusaidia kusema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona mpango wowote ambaa umefanyika mpaka sasa hivi, hali ni ngumu, inatisha na wanaohangaika sana kwa kipindi hiki ni wanawake kwa sababu asilimia kubwa ya wanaume wanakimbia familia zao. Anamuaga mama nyumbani kwamba anakwenda kutafuta chakula, matokeo yake humuoni wiki mbili, mwezi mmoja, mwaka mpaka ahakikishe kwamba njaa imekwisha ndipo atakaporudi nyumbani. Tunamsaidiaje huyu mama aliye Shinyanga kuweza kumudu familia aliyonayo? Naiomba sana Serikali iutazame Mkao wa Shinyanga kwa macho mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo kwa sababu ni tatizo ambalo linajirudia, naomba nitoe ushauri wa kudumu katika tatizo hili. Nimpongeze aliye kuwa Waziri Mkuu kipindi kilichopita, Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Edward Lowassa, alifika katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga akazindua mradi mmoja wa umwagiliaji, mradi wa Masengwa. Alipozindua mradi ule akasema mradi huu hautakuwa na mafanikio kama hakuna bwawa na akaahidi kama Waziri Mkuu kwamba atahakikisha bwawa linachimbwa katika kijiji cha Masengwa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Kinachonisikitisha ni kwamba sijui ni nani anayetekeleza ahadi hizi, mpaka leo hii ahadi ile ambayo ingesa idia kuondoa tatizo hili tulilonalo katika kilimo cha umwagiliaji haijakkamili. Niwaombe sana Watendaji wetu mlioko Serikalini, ahadi hizi zinapotolewa zikamilisheni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shinyanga tuna mito ya kutosha lakini hatuna pa kuyaweka hayo maji. Kuna mito inayopeleka maji ziwa Victoria, kuna eneo linaitwa Mwakitalyo, eneo lile maji yanakaa pale mpaka miezi minne au sita lakini kwa sababu hatuna sehemu ya kuyahifadhi, tunakuwa hatuna faida nayo. Naomba sana na naishauri sana Serikali, ituangalie Mkao wa Shinyanga kwa kilimo cha umwagiliaji, iende ikabaini maeneo ambayo yanapatikana maji ili waweze kutuchimbia mabwawa tuweze kuondokana na tatizo la kuwa tunapiga kelele za njaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, naomba sasa nichangie kwenye *SACCOS*. Kule vijijini tuna *SACCOS* nyingi sana, lakini hazikopesheki kwa maana ya kwamba masharti yanayotolewa na benki ni magumu, hayafanani na mazingira ambayo wananchi wetu wapo. Unakuta kweli *SACCOS* imeundwa pale na wana fedha za kutosha lakini wanaambiwa sharti la kwanza ni lazima wawe na ofisi ambayo inafanana na benki. Hivi kweli kule kijijini unafika hata nyumba ya bati haiko, hiyo ofisi ya kufanana na benki wanaitoa wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaambiwa ni lazima wawe na Mhasibu, kule kwetu Usukumani pengine kijiji pale mtoto ambaye amefanikiwa kuwa na elimu labda ni hawa wa sasa hivi ambao wamemaliza *Form Four*, huyo Mhasibu tunamtoa wapi? Mimi nadhani ni wakati muafaka Serikali kuangalia vikundi hivi nya *SACCOS* vinapataje mikopo hii lakini siyo kwa masharti yanayotolewa na benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri katika eneo hili. Kuna Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ambao unatoka Serikalini unakwenda kila Halmashauri, mfuko huu masharti yake siyo magumu na wanawake wengi wa vijiji wanaweza kuumudu, lakini ukiangalia fungu linalotengwa na Serikali yetu ni dogo sana. Naomba nitoe mfano, Halmashauri yangu ya Shinyanga mwaka 2009 ndiyo mara ya mwisho wamepewa fedha zile, vikundi 66 waliomba mkopo ule, fedha iliyotoka Serikalini ni shilingi milioni nane, Halmashauri ikachangia 10%, shilingi milioni 2.1 ndani ya fedha zile 10% wanatakiwa akina mama hao wapate mafunzo na yule mtaalam wa maendeleo ya jamii atumie hiyohiyo fedha kwenda kule vijiji, mtaalam huyuhuyu wa maendeleo ya jamii hata gari la kumfikisha kijiji hana, matokeo yake katika vikundi 66 ni vikundi 21 tu vilivyopatiwa mkopo huo kwa sababu fedha hazitoshi. Naishauri Serikali iwatazame kwa jicho la huruma wanawake wote wa Tanzania, kwa kuuongezea mfuko huu fungu kwa sababu masharti yake siyo magumu na wanamudu kulipa deni hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hapo, naomba niende kwa watoto wanaishi katika mazingira magumu. Mwanzo Serikali ilikuwa na mpango wa kuwalipia watoto ambao wanafaulu na ambao wako shule za msingi, lakini sasa hivi suala hili limerudishwa kwenye Halmashauri, Halmashauri zetu hazina uwezo wa kulifanya hili. Watoto wanafaulu kutoka Darasa la Saba kwenda *Form One* lakini Halmashauri hazina uwezo wa kuwalipia wote, matokeo yake watoto hao wanabaki wanahangaika kurudishwa nyumbani, atasoma mwaka wa kwanza, mwaka wa pili, wengi wao wanakata tamaa na kuacha masomo haya, tunawasaidiaje watoto hawa wanaishi katika mazingira magumu? Naishauri Serikali iridishe utaratibu wake uliokuwepo mwanzo wakisaidiana na Halmashauri ili watoto hawa waweze kupata haki yao ya msingi ya elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kama sitaongelea suala la maslahi ya Madiwani kwa sababu mimi nimekuwa Diwani kwa kipindi kilichopita. Naelewa matatizo aliyonayo Diwani, Diwani anafanya kazi kubwa sana, sisi sasa hivi tuko Bungeni lakini kazi alizonazo Diwani ni nyingi. Posho ya Diwani ni shilingi 120,000/=, Diwani huyu hakaposheki. Ukiangalia watu wanaomzunguka mara huyu ana mgonjwa, mara mwanafunzi anataka kulipiwa ada, hiyo shilingi 120,000/= anaifanyia kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Madiwani waingizwe kwenye utaratibu wa kulipwa mishahara. Kama sheria hiyo haipo basi nniombe Serikali ifikirie kuleta sheria hiyo ili Madiwani waingie kwenye utaratibu wa kulipwa mishahara. Kama haiwezekani kwa sasa hivi kuwalipa mishahara basi iangalie utaratibu mwingine wa kuweza kuwaongezea posho zao, lakini sio posho ya shilingi 120,000/. Tunawakatisha tama, tunafika mahali tunasema hawawezi kusimamia miradi ya Halmashauri, lakini inabidi

wakae kufanya kazi zingine kwa ajili ya kujitafutia riziki. Naiomba sana Serikali iwafikirie Madiwani kwa kuwaongeza posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji mbovu uliopo katika Halmashauri zetu, Watendaji wanatuharibia miradi yetu mingi. Kuna miradi ambayo mtu kama una macho yako ukitazama tu unajua hapa ni sawa au sio sawa lakini Diwani anapofikia mahali anasema hapa hapana, kwa sababu kuna vitu ambavyo havitaki utaalamu, majibu ya wataalamu yanakuwa ni kwamba wewe Diwani sio mtaalamu, mimi ndio mtaalamu, tunawapeleka wapi Madiwani hawa. Tunafika mahali tunawalaumu kwamba hawasimamii shughuli za maendeleo. Kama yeze pale hata kitu kinachotizamika tu kwa macho anaambiwa yeze sio kazi yake atasimamia vipi? Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusema kwamba wametenga siku saba kwa ajili ya kuwapa mafunzo Madiwani na naomba zoezi hili liendelee kila mwaka ili tusiendelee kuwapa lawama Madiwani wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Msemaji wetu wa mwisho mchana huu au asubuhi atakuwa Mheshimiwa Simbachawene.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi. Kipekee nichukue nafasi hii ya awali kabisa kuwashukuru sana wananchi wa Kibakwe kwa kuniamini kwa mara ya pili na kunipa nafasi hii kubwa na muhimu katika kuwawakilisha ili niweze kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya kwanza kusema mambo ya haraka haraka ambayo sijakubaliana kabla sijaingia kwenye hotuba yangu yenyewe. Nilipokuwa nasikiliza hotuba hizi zote, kwanza nichukue nafasi hii kumpungeza pia Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mkuchika kwa hotuba zao nzuri na watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Idara zote kwa kuandaa hotuba nzuri kuliko wakati wowote ambaa nimekaa katika Bunge hili. Zinajieleza, majedwali yanajieleza, unaiona Tanzania katika vitabu vyao, hakika ni hotuba nzuri ya kiwango cha juu, tunawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikiliza vizuri hotuba ya upande wa Upinzani, mengine yote sina nafasi ya kuyasema, lakini hili la *CDA* kwamba Makao Makuu kuhamia Dodoma iwe basi, mimi nilisikitika sana. Kama wanapenda tuwe tunawapokea vizuri hapa Dodoma, hili neno wasirudie tena kulisema. Tunawapenda sana, lakini kwa mpango huu hatutakuwa pamoja. Makao Makuu kuhamia Dodoma ni mpango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiongozwa na Chama cha Mapinduzi, ni Sera ya CCM na nashauri Serikali yangu iendelee kuitekeleza sera hii kwa utaratibu wowote unaofaa pamoja na shukrani nazotoa kwa kuleta Chuo Kikuu cha Dodoma na mambo mengi yanayofanyika katika Mkoa wa Dodoma, tunawashukuru sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili hapo ni kuhusu masuala mazima ya utekelezaji wa miradi katika eneo la ahadi za Serikali na hasa Viongozi wetu. Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuja aliahidi suala la umeme, sisi tunaotunza lile Bwawa la Mtera, vijiji vyangu karibu sita vyote vinazunguka Bwawa la Mtera lakini watu hao hawana umeme, tunachoambulia kuona ni nyaya tu zinazosafirisha umeme kupeleka Mikoa mingine. Mheshimiwa Ngeleja tumechoka na habari hii na nadhani Mheshimiwa Makamu wa Rais aliahidi na sasa nasimamia ahadi, safari hii nitakusikilizasikiliza kwa sababu ni bajeti yetu ya kwanza lakini *next time* umeme lazima upite Kisima uje Chipogolo uende mpaka Rudi, bila ya kufanya hivyo wale watu watafanya tambiko zao maji yale yatakauka, kwa hiyo hutazalisha umeme pale, maana hawaoni faida wanayoipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze na kushukuru kwamba miradi ya *MCC* inaendelea na wananchi wa Kibakwe wanajua kabisa kwamba umeme watapata. Harakati zinaendelea na wakati wowote waondoe mashaka kwamba miradi hiyo ya *MCC* itatekelezwa na nina uhakika kwa sababu naona mchakato unavyoendelea na nawawakilisha vizuri katika jambo hili wasiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda nilizungumzie ni kuhusu posho za watumishi wa Halmashauri ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu. Vijiji vyetu vinatofautiana sana. Haiwezekani mtu anayefanya kazi Mpwapwa pale Mjini akalipwa sawasawa na mtu anayefanya kazi Gwamuhungile au Mang’aliza, haiwezekani! Yule ili afike kwenye kituo chake cha kazi ni lazima atembee kwa miguu masaa karibu matano kwa sababu hakuna usafiri wa gari. Nimerudi hapa *this time* kwa sababu ya kutengeneza barabara kufika maeneo yote katika Jimbo. Hakuna kijiji hata kimoja ambako barabara haifiki, lakini vyombo vya usafiri sasa vinatoka wapi? Maeneo ni milimani, hali hiyo inapelekea watumishi wetu kupata taabu kubwa kutoka kule anakoishi mpaka afike kuchukua mshahara wake, mpaka aupate ameshatumia karibu robo ya mshahara. Huyu mtu ni lazima alipwe *allowance* ya kufanya kazi katika mazingira magumu. Kama Serikali hamtaliona hili, hakika hakuna mtumishi atakayekwenda kule akubali kukaa. Nawaombeni sana mlione hili na muone namna ya kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya *CAG* imeonyesha upungufu mkubwa katika usimamizi wa miradi na ubora wa miradi ya Halmashauri, hapa ndipo kwenye tatizo kubwa. Wataalamu wetu ni wataalamu wa mezani, lakini hawana *manpower* ya kutosha ya kusimamia miradi yote inayofanyika ya afya, kilimo, elimu na miradi mingine. Sio rahisi kwa namna yoyote kwa idadi ya viwango vya wataalamu wa ujenzi wakawenza kusimamia na ndiyo maana unakuta Daktari wa Mifugo anasimamia ujenzi wa josho ambako kunatumika sementi, kokoto na mchanga anajua wapi? Huwezi kupata ubora na huwezi kupata kitu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali tuone namna ya kufanya *setup* hii ya Halmashauri pale kwenye *level* au kuwe kuna mtu anaitwa Meneja wa Miradi au Mhandisi wa Miradi. Maana yule Mhandisi aliyepo ni wa ku-*design* kwenda kwenye

semina, kupokea maagizo ya Serikali lakini yule anayesimamia miradi tuangalie hiyo *setup*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane pia na Mheshimiwa Lowassa kusema kwamba kwa kweli Wizara hii mkubwa pamoja na kwamba ipo kwenye mtu mwenye nguvu pia, lakini ni kubwa mno iangaliwe namna ya kuigawanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio tuliyonayo. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya mambo makubwa katika nchi hii. Hizi siasa za leo za kuamini kila kitu kilichofanyika ni kibaya ni dhambi kubwa sana. Dhambi hii malipo yake ni matokeo yatakayokuja baada ya kudhani kuna neema baada ya kuiua CCM. Watanzania tumefika hapa tulipofika, ndani ya miaka 50 yaliyofanyika ni makubwa sana ambayo yanaonekana lakini badala ya kujivunia, yanayoonekana ni manung'uniko kati ya mtu na mtu. Leo utaiondoa CCM madarakani kwa kutumia njia haramu, je, wewe utatawala namna gani baada ya kumaliza huo mkakati wa kuiondoa CCM?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Watanzania, nayajua maisha ya mtu maskini, niliyezaliwa nikachunga ng'ombe na ndama mpaka nafika Kidato cha Kwanza. Niliyekulia kwa kuvalaa kaptura moja, ninayaona mabadiliko yaliyopo kwa sababu hata sasa kijijini hakuna mtu anayekosa kunywa chai. Ni kweli changamoto katika maisha zipo ni lazima tuhakikishe tunaboresha maisha ya Watanzania zaidi ili *reflect* hii hali ya sasa ambapo tunaona uchumi wa Taifa umekua, lakini jamani tusikatishane tamaa kwamba eti hakuna kilichofanyika, hii ni dhambi kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Watanzania, siasa hizi tuachieni Wanasiisa kwa sababu ni kazi yetu na hatuna shughuli nyingine ya kufanya. Wote mkiwa Wanasiisa mtaacha kufanya kazi, mtakwenda kwenye maandamano mwisho wa siku hakuna tija tutakayoipata. Mimi nawaomba tuvumiliane, makubwa yamefanyika, nchi ambayo tunapata uhuru hatuna barabara hata kilomita 200 za lami, leo tuna kilomita karibu kilomita 6,500 ambazo zimejengwa barabara za lami kwa sasa kuanzia mwaka 2006/2011 ni kilomita 11,300 ukijumlisha na ambazo ziko tayari kilomita 6,500 tunazungumzia kuwa na kilomita 17,000 ndani ya miaka hii miwili, mitatu. Ukijumlisha na barabara za Kenya, Uganda, Rwanda hawafikii urefu wa barabara hizi. Haya ni mafanikio makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Vyuo Vikuu vyote nchini, toka tunapata uhuru tuna wasomi wachache, *graduates* wawili, watatu, leo hii tuna udahili wa wanafunzi walioko vyuoni zaidi ya laki moja na haya yamefanyika ndani ya miaka mitano tu, ndani ya miaka 10 tu, tuna udahili wa sasa wa zaidi ya wanafunzi laki moja kwenye. Nchi hii itakuwa ni nchi ya watu wasomi badala ya kukaa vizuri tufikirie namna ya kujenga uchumi mzuri, namna ya kushirikiana kujenga amani katika nchi yetu ili hawa wasomi wanaokuja waje waishi katika mazingira mazuri tunafikiria namna ya kuibomoa nchi yetu, hatuwezi kufika na Mungu atatulaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni mifano michache tu, lakini pamoja na mafanikio haya nilitaka nizungumzie changamoto tuliyonayo katika nafasi ya wazalendo

katika uchumi huu unaokua sasa na kwamba nchi yetu inakuwa na uchumi wa kati. Changamoto tulionayo sasa ni kulinda, Serikali yetu kulinda nafasi ya wazalendo. Watanzania wengi wanaonewa huko viwandani wanakofanya kazi. Uwekezaji tija yake ni kwamba tupate ajira hata kama pengine tunasema tunasamehe kodi, lakini pale tunapokuja kumnufaisha Mtanzania wa kawaida ni pale atakapokuwa amepata ajira na anatunza familia yake na maisha yanakwenda lakini kama kule halipwi vizuri, kama kule anapata TB, hapati huduma za afya anazostahili tunawatengenezea vifo badala ya kuwatengenezea raha katika maisha yao. Nafasi ya Watanzania Serikali ii琳de. Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali ya watu wanyonge, haiwezekani hata siku moja tukalinda wawekezaji kuliko wazalendo. Nafasi yao iheshimike, ilindwe, Wizara ya Kazi ifuatilie viwandani ione kuna nini, Waswahili kule wananyanyaswa kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika sekta ya madini, wazalendo hawa msipowaangalia tutakuwa *dispersed*, *the industry is very big*, wako wengi sana wale. Mimi ilipotokea ile *rush* ya kwenda Winza kule ambako mpaka leo hatujaweza kufanya kitu chochote cha maana, niliona waliingia watu karibu 10,000 nikaogopa kwamba hii *industry* sio ya kuchezeachezea, sio kundi la kuchezea hili. Leo watu wanafanya utafiti, wanapata leseni kwa kupita juu kwa helkopta hatujajui vijijini kwetu, hatujajui kwenye Kata zetu wala kwenye Wilaya, ukienda gusa unaambiwa hili eneo lina leseni kubwa, ya nani ambaye kijijini hatumjui. Tunasema hapana lazima wazalendo waandaliwe nafasi yao na wasaidiwe na Serikali. Mimi *ni-declare interests*. Kule Kibakwe nimekamata maeneo kama heka tano au sita za *copper*. Nimeambiwa hiyo leseni inaisha ndani ya miaka mitatu, pamoja na Ubunge wangu nimeshindwa kufanya utafiti mpaka leo leseni ile nitanyang'wanywa, sasa Mswahili wa kawaida hataweza kama asiposaidiwa? Kwa hiyo, Wazungu watakuja, watachukua tu mali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme neno moja kwamba, kuna Mwanafalsafa mmoja anasema suala sio *what you have, but what you do with what you have*, hiyo ndiyo itakayo-determine your success or failure. Not what you have, but what you do with what you have". Kwa hiyo, tuna rasilimali kubwa, tunayo makaa ya mawe Kiwira, Mchuchuma maneno yanayosemwa hapa hivi kama Serikali iko *serious* lazima tufike mahali tufanye maamuzi magumu kwa ajili ya kusaidia nchi yetu. Kama tunatakiwa kukopa, tukakope hata tuweke dhamana ya watu wetu, tuko milioni 40 tu, idhamini wote tupate umeme, hatujezi kujenga nchi yeye uchumi ulio wa kati kama hatujawa na umeme madhubuti. Haya yatafanyika kama tutaamua kuwekeza kwa nguvu kwa njia yoyote ile lakini kuwekeza kwa nguvu, kwani tukikopa kuna ubaya gani? Mimi nadhani ni vizuri Serikali ikakopa ili kufanya mambo ambayo yatarithiwa na vizazi vinavyokuja, nchi hii hatuishi sisi tu viko vizazi vingi vinavyokuja vinahitaji kuona yale tuliyoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ambalo napenda kulizungumzia, nizungumze tu namna ambavyo nafasi yetu ilivyo. Kuna msomi mmoja Profesa Latigo wa Uganda anasema hivi katika maneno yake, naomba ninukuu yameandikwa Kiingereza "One way is for Africa to change its' strategy to raise intellectuals with godly values and sound decision making abilities. Without African intellectual, capital, timber, mineral and other abandon resources from Africa will continue to be manufactured elsewhere and exported back to Africa at exorbitant cost"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapaswa kufanya maamuzi magumu hata kama ni kwa gharama ya mateso ya watu wake. Ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli zetu mchana huu, napenda kuwapa taarifa moja kuhusu Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said ambaye ameugua ghafla, amekimbizwa Hospitali ya Mkoa. Taarifa yake tutakupeni baadaye kadri tutakavyokuwa tumejata kutoka hospitali.

Baada ya taarifa hiyo, naomba kuwataja ambao watachangia tutakaporejea saa 11.00. Tutaanza na Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilifi, Mheshimiwa Brig. Jeneral Hassan Ngwilizi na wengine tutawataja baadaye.

Nawashukuru sana kwa ushirikiano wenu, naomba kusitisha shughuli zetu hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza majadiliano, napenda kwanza niwajulishe kuhusu hali ya Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said. Sasa hivi anaendelea vizuri, anatembea mwenyewe, amepata chakula, alikuwa amepata *stress* na pia alikuwa kama ana-*pressure* kidogo, ndiyo iliyosababisha tatizo la mchana lakini sasa hivi hajambo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Kama tulivyowatangazia, tutaanza na Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Msabaha, baadaye Mheshimiwa Vicent Nyerere na Mheshimiwa January Makamba naye ajiandae. Sasa tunaanza na Mheshimiwa Mkiwa.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu na uhai mpaka siku hii ya leo nami nikawa hapa jioni kwa kuchangia bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anaahirisha Bunge la Tisa, Kikao cha Ishirini alipotamka katika bajeti yake wakati anafanya majumuisho, akasema katika Jiji la Mwanza sasa hivi tutakuwa na Manispaa mbili,

Manispaa ya Nyamagana na Manispaa ya Ilemela. Kwa wazo hili na kauli hii, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kauli yake hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini basi nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu? Katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza imeshakuwa tabu kwa wananchi kufuata huduma mbali, kupoteza muda wakati muda ni mali kufuatilia huduma, watu wanatoka mbali na kwa kuwa tayari tuna Wilaya ya Ilemela na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatamka wazi kwamba tutapata Manispaa ya Ilemela, ni vizuri zaidi tukawa na Manispaa ya Ilemela ili kuokoa muda wa wananchi na ili kuwasogezea wananchi huduma karibu. Nafikiri dhana ya Serikali ni kuwasogezea wananchi huduma karibu na si kuwarundika wananchi eneo moja wakikaa kusubiri huduma moja ambayo inaweza isipatikane kwa siku tatu mfululizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya watu wanataka kufukiafukia jambo hili. Kwa nini wananchi wanaoishi katika Jiji la Mwanza wao wanahitaji wawe na Manispaa, lakini Watendaji wa Serikali hawataki wananchi wa Jiji la Mwanza kuwa na Manispaa? Nina imani kabisa huenda wanafaidika na Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Ni bora tukagawanywa tukawa na Manispaa, kila watu waelewe wako katika Manispaa ipi na wajibu wao ni kitu gani. Tumeona Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuna malipo yenye nyaraka pungufu yako katika Jiji la Mwanza yana mamilioni ya shilingi. Mishahara ambayo haikurudishwa Hazina ni mamilioni ya shilingi, pesa hizi zinakwenda wapi na ninaona mwelekeo huu, ndiyo sababu hata Watendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza hawataki ziwe Manispaa mbili wanataka iwe Halmashauri moja ili waendelee kufanya haya wanayoyafanya. Yametosha, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na tunaendelea kumwomba atugawie Manispaa ya Jiji la Ilemela. Nafikiri hili atakayelihitaji kwa kirefu na ni nani katoa kauli hiyo, ninaweza nikamweleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda kuzungumzia wavuvi wa Tanzania kwa ujumla wao kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu amegusia wavuvi. Wavuvi wa Tanzania kwa ujumla wao matatizo yao yanalingana na wavuvi wanaotoka katika Ziwa Victoria hasa maeneo ya Jiji la Mwanza na Mkoa wa Mwanza kwa ujumla. Tulipitisha Sheria ya wavuvi kuwa na leseni. Sasa imefikia sehemu hata kibarua anayeingia katika mtumbwi kwa ajili ya kwenda kusaidia uvuvi ule naye anatakiwa awe na leseni. Cha ajabu, vibarua wanaokoroga zege hawana leseni, vibarua wanaokata nyasi kulisha ng'ombe hawana leseni, vibarua na makondakta wanaopakia watu hawana leseni lakini ni namna gani mvuvi wa Tanzania anavyodhalilishwa, ambavyo hasaidiwi. Pamoja na hayo, kama hiyo haitoshi, leseni ya mvuvi mdogomdogo huyohuyo ambaye ni kibarua inachanganywa kwenye leseni ya mwenye chombo, ina maana inambana huyu kibarua kwa sababu mtaji wa maskini ni nguvu zake, inambana huyu kibarua hata kama anahitaji kwenda kufanya kazi sehemu nyingine ambapo ina maslahi zaidi anashindwa kwa sababu leseni yake imechanganywa kwa mwenye chombo. Kwa hiyo hawesi akatoka kwenda kujitafutia maisha hata kama anaweza akapata mshahara mkubwa kule anakokwenda lakini inambidi amalize muda wake ili aweze kukata leseni nyingine. Huu ni uonevu, huku ni kumnyonya mtu nguvu zake kwa sababu mtaji wa maskini ni nguvu zake, kwa maana hiyo hawa wavuvi wamekuwa kama si Watanzania na kama ni Watanzania, tunaiomba Serikali jinsi ambavyo inapenda vibarua wengine ambao hawana leseni,

kibarua anayekwenda kusaidia naye awe na leseni ili watu wote watendewe haki sawa.
(*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi mwenye chombo cha uvuvi katika Ziwa Victoria, nahisi huenda ni wavuvi wote wa Tanzania, anatakiwa akate leseni akiwa katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza, lakini akitoka katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza akiingia tu eneo la Sengerema anatakiwa awe na leseni nyingine akaikate Sengerema na nafikiri akitoka hapo akienda Magu katika eneo la Ziwa anatakiwa awe na leseni nyingine, atakata leseni ngapi huyu mtu kwa uvuvi wa Ziwa hilohilo? Hivi mbona wenyenye mabasi au wenyenye magari madogo anapokata *Road Licence*, anatembea Tanzania nzima? Kama kaikatia Kigoma atafika Mtwara kwa *Road Licence* hiyo hiyo, inakuaje mvuvi anaonekana si Mtanzania na anapoingia kufanya shughuli za uvuvi na analipia kipato halali ambacho kajiwezesha mwenyewewe Serikali haijamwezesha, kajituma mwenyewewe Serikali haijawapa elimu wavuvi wadogowadogo lakini bado ananyanyaswa kiasi kwamba anaonekana kama yeye ni mharibifu zaidi. Wavuvi wa Tanzania wako tayari na wenyewewe wawawezeshe waweze kuvua kwa tija, waweze kupata maendeleo na waweze kuchangia pato la Taifa liweze kuinuka. Tunasema mapato ni madogo, lakini hatujui jinsi gani tuwawezeshe wananchi walio wengi ambao hawana kazi na waweze kuturudishia mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, napenda kuongelea maji. Tunafurahi zaidi ndugu zetu wa Shinyanga, Kahama wamepata maji kutoka Ziwa Victoria, hilo halina ubishi, sote ni Watanzania lazima tutumie maliasili za Tanzania lakini wale wakazi wa Jiji la Mwanza baadhi yao wana mabomba ndani ya nyumba zao lakini maji hawajawahi kuyaona. Muumba vyungu hulia kwenye vigae lakini si vigae vya aina hii, maji yafike Kahama na sasa hivi yanaenda Tabora lakini Jiji la Mwanza kuna watu hawajawahi kunywa maji safi na salama, maji wanayaona yale pale lakini kuyashika hayashikiki. Maji yafike mpaka hapa Dodoma, yafike Kibaha lakini tunaiomba Serikali iwaangalie wananchi wa Jiji la Mwanza, waweze kuwawekea mabomba. Kuna haja gani ya kumchimbia mwananchi kisima kisichotoa maji, wakati maji yako mita mia moja? Tunaomba waweze kuleta maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia eneo la Uwanja wa Ndege wa Mwanza, ni aibu. Tunasema tumeingia kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki lakini hii ni aibu miaka nenda miaka rudi, miaka mitano nimekuwa Mbunge, awamu ya kwanza nasikia kwamba ni *BADEA* watakuja kutengeneza uwanja ule. *BADEA* wameshakubali lakini mpaka leo nasikia hadithi za *BADEA* lakini ni uwanja ambao haufai kuwa katika Jiji kama lile. Ni jiji la pili Tanzania lakini uwanja wa ndege unatisha. Mvua ikinyesha Magu maji yote yanakuja ndani ya Uwanja wa Ndege wa Jiji la Mwanza, halafu wanasema kwamba wametengeneza Uwanja wa Ndege lakini ukijiuiza wametengeneza wapi, haionekani. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, Mkoa wa Mwanza na Jiji la pili Tanzania, waangalie hili, mvua inanyesha, mabegi ya watu yanalowana mpaka yanakatika, ukianza kufuatilia kulipwa begi lile unaweza ukamaliza muda mrefu hujalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hii ni uzembe na kuacha Jiji la Mwanza katika hali ile, uwanja unakuwa katika hali ambayo hairidhishi, sidhani kama kuna uwanja mbovu katika Majiji haya kama wa Mwanza. Maana Uwanja wa Jiji la Arusha naufahamu na ule ndiyo unafuatia Uwanja wa Mwanza ukifuatiwa na uwanja wa Jiji la Tanga. Kwa sababu sasa hivi ndege zimekuwa nyingi, zinawashushia watu kwenye *cargo*, hakuna gari ya kuwachukua, kuna watu wengine ni wazee, hawawezi kutembea, hakuna gari ya kumtoa mzee ambaye ameshukua kule kwenye sehemu ya *cargo* aje mpaka kwenye maeneo ya kuweza yeze kukaa akisubiri ni jinsi gani anaweza kutoa mzigo wake. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iweze kuboresha Uwanja wa Ndege wa Mwanza, kwani uwanja huu katika Jumuia hii ya Afrika Mashariki utatusaidia na nafikiri tukiutengeneza tunaweza kuongeza kipato kwa sababu ndege zitawenza kutua. Japokuwa wenzetu wanatuambia kwamba ndege zimehamia wapi kwa ajili ya kupakia samaki lakini nina imani kabisa ndege zimehamia kwa sababu uwanja hauridhishi. Uwanja uko kandokando ya maji lakini uwanja hauridhishi. Kwa hiyo, nachoomba Serikali iangalie hili japokuwa kwenye bajeti ya kwanza ya Wizara ya Uchukuzi, viwanja vya ndege vyote havikutengewa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti hii ya Waziri wa TAMISEMI, ameongelea kufufua na kuendeleza sekta ya ngozi. Si sekta ya ngozi tu tuongelee na viwanda vya ngozi, lakini tarehe nane hapa nilisikia jibu la ajabu, kile kiwanda kilijengwa karibu na Ziwa Victoria na maji machafu yakaingia Ziwan. Wakati huohuo pembeni mwa Kiwanda cha Ngozi cha Mwanza kuna shimo la majitaka. Maji machafu yaliingiaje kwenye Ziwa Victoria wakati kuna shimo la majitaka pembeni? Tunamwomba Waziri wa Viwanda au Waziri wa Uwekezaji aje Mwanza kile kiwanda kama mwekezaji kashindwa kukiendesha akirudishe Serikalini tunahitaji vijana wapate ajira. Tunasema hatuna ajira za kuwapa vijana wakati viwanda tunaviuza vinafanywa *godown*. Aliyekinunua kama alikinunua kukifanya *godown*, Serikali mtatuambia na kama alikinunua kama kiwanda cha ngozi na hapa mnasema mnataka kuboresha sekta ya ngozi nafikiri kiwanda cha Mwanza kitaongoza na tunaomba kiendelezwne na kwa sababu sasa hivi maji machafu ya Mji wa Mwanza yote yanaingia pale, namwomba Waziri alifutilie suala hili ili vijana wa Mwanza waweze kupata ajira na ajira ni nyingi Mwanza, lakini tunashangaa Serikali kuzibania ajira hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Serikali imesajili vijiji. Katika usajili wa vijiji hivi imetoe hati za vijiji, lakini nina imani kwamba vijiji hivi vimesajiliwa lakini wananchi wanaoishi katika vijiji hivi wanaambiwa wanaishi ndani ya hifadhi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu.

Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba Mbingu na Ardhi na leo hii kunajalia niko mahala hapa. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wangu wote wa Kitaifa wa Chama akiwemo Dkt. Willibrod Slaa na aliyekuwa Mgombea Mwenza Said Mzee kwa upande wa Zanzibar. Tunatambua kazi yao ngumu waliyoifanya na kuongezea Wabunge wengi wa CHADEMA. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kuchangia kwenye sekta ya Muungano. Zanzibar tumekuwa na kero za Muungano.

MWENYEKITI: Mheshimiwa nakuomba usisome.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Hapana sisomi. Zanzibar tumekuwa na kero nyingi za Muungano na kero hizi zimekuwa sio kama Wazanzibar hawataki Muungano, Muungano tunautaka lakini tuna kero ambazo zimekuwa sugu na kero hizi zikitatuliwa Wazanzibar na sisi tutakuwa tuko huru tukisikilizana baina ya Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha Mafunzo cha Ziwanu, kimekuwa ni kero kwa Polisi wetu na kimekuwa ni kero hata kwa nyumba zile wanazokaa, kwa kweli inasikitisha sana. Kituo cha Mafunzo Ziwanu ukiangalia kwa kweli hakina hadhi na hakina hata huduma za jamii. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye mwenyewe binafsi angalau aje atembelee Chuo hicho cha Mafunzo cha Ziwanu. Polisi wako katika hali mbaya na Polisi hawa wanalala kwenye chumba pamoja na mtoto wa miaka kumi na sita na pembeni ameweka pazi na huku amelala na mama na juu paa linavuja. Hii ni kuzalilisha Polisi na naomba mfanye juhudzi za makusudi kabisa, mje muangalie Kituo kile cha Polisi Zanzibar na mje mtembelee Kambi za Jeshi, muangalie mazingira Wanajeshi wetu wanayoishi Zanzibar. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kambi za Jeshi zimekuwa na migogoro na wananchi, kama Kambi ya Bavuai kuna wananchi wa Kaburi Kikombe wamechukuliwa sehemu za mashamba yao na mpaka leo hawajajua mwisho wao ni wapi na kero zao hizi zitatulika wapi. Kwa hiyo, tunaomba kwa makusudi kabisa Serikali na Wizara iangalie kero hizi za wananchi ambazo zinaingia kwenye sekta za Muungano na mzitatue kwa muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na vijana wetu ambao wanakuja Tanzania Bara kwenye sekta za Muungano kama vile Polisi na Jeshi. Vijana hawa wanakuwa wamepimwa afya Zanzibar lakini wakifika Tanzania Bara wanakuwa tena wanapimwa afya. Kwa kweli wakishapimwa afya wanaambiwa warudi, sasa sijui ni kitu gani, sijui ni utapiamlo, kwa kweli Wazanzibar tunazidi kusikitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la wastaa fu. Kuna wazee wetu wamefanya kazi katika sekta za Muungano. Wazee hawa wamefanya kazi siku nyingi na wanavyofuutilia mafao yao wanaambiwa nenda rudi nenda rudi. Sawa kuna hawa ambao

wanatumia nauli zao kutoka Zanzibar na kuna Tanzania Bara kufuatilia mafao yao na hawapati. Hili suala la mafao si la Wazanzibar tu, tumeona hata wazee wa Tanzania Bara ambao walikuwa wanafanya kazi *East Africa* leo wanalala barabarani wakidai haki zao. Mimi sidhani kwa kweli kama wale wazee ni wagonjwa wa akili. Walilitumikia Taifa hili lakini haki zao hawakupatiwa mpaka leo. Kwa hiyo, naomba sana Serikali na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie suala hili na kama kweli hawa wazee wanadai haki yao na wao wapatiwe lakini leo hii unamwona mzee analala barabarani, analia, anavuja damu, sisi kizazi kilichobaki tunapata lawama. Kwa kweli Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu muangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchaguzi Zanzibar huwa tunalitewa Wanajeshi na Polisi wengi sana lakini hawa Polisi wanavyomwagua kipindi cha uchaguzi kule Zanzibar wakilinda na sijui wanakuwa wakilinda kitu gani kwa sababu Zanzibar mimi najua wamekomaa kisiasa lakini sasa unakuta Polisi hawa na Wanajeshi kwenye doria zao za usiku pia kuna vitendo ambavyo huwa wanavifanya na sisi kama Wazanzibar tunakuwa hatupendezewi navyo. Kwa hiyo, pia muangalie Jeshi hili kwa makini sana wakati wa Uchaguzi na wakati huu tupo katika mfumo wa Vyama vingi. Kuna kero za kuepukika na Serikali kama itakuwa inafuatilia mambo haya katika Wizara mbalimbali kwa kweli tutafika hapo tulipopakusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie katika suala zima la ajira, vijana wetu wamekuwa wakihangaika na ajira, vijana wengi wanasoma na wengine wanafika *Form Four* wanarudi majumbani, wengine wanamaliza Vyuo Vikuu wanarudi majumbani. Katika sekta za ajira kumekuwa na rushwa. Naomba Waziri uwe unakagua Wizara zote na Serikali. Kwa kweli nafasi za kazi zimekuwa zinatolewa kwa upendeleo, leo utamkuta kijana kasoma mpaka Chuo Kikuu ana vyeti vyake vizuri lakini katika kuajiriwa anazunguka anarudi mpaka vyeti vyake vinapaukia kwenye mifuko. Hili ni jambo la kusikitisha sana, kwa kweli Serikali muangalie nchi hii tunaipeleka wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuna watu wanasema kwamba CHADEMA tunapenda maandamano, hapana! Katika maandamano pia tunatoa elimu ya uraia. Kuna Watanzania wengi sana hawajui hata Katiba ya Jamhuri ya Muungano iko vipi. Ukifika kijijini mtu anakuambia kabisa mimi Katiba ya Jamhuri ya Muungano sijui hata sura yake iko vipi, kwa hiyo, sisi kama Vyama vya Siasa tunapokuwa kwenye majukwaa ya siasa tunakuwa tunatoa elimu ya uraia na kuwafahamisha Watanzania kwamba Vyama vingi siyo ugomvi, Vyama vingi ni kuleta maendeleo na kupigania maslahi ya Watanzania wachache ambao ni maskini. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la ajira linapelekea vijana wengine hata kuzalilishwa kijinsia. Leo wanakwenda ofisini kijana huyo anataka ajira lakini akifika huko kwenye ajira anakutana na mambo mengi, maadamu ye ye anataka ajira hasa watoto wetu wa kike, wamekuwa wakidhalilishwa sana na watu wenye uwezo hapa Tanzania. Hili liangaliwe kwa makini, kwa kweli mtu unapata ajira umeshadhalilishwa na

UKIMWI umeshapata, sidhani kama hiyo itakuwa ni ajira. Waziri Mkuu na Serikali, angalia Wizara zako zote, masuala haya yapo wala hatusemi uwongo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala zima la mikopo ya wanawake, kuna mabilioni ya Kikwete yalitoka, tukasikia na kule Zanzibar ni mabilioni wakati huo ni ya Rais Amani Abeid Karume ambaye sasa hivi ni mstaafu, pesa hizi ziliishia mikononi mwa wajanja wenye akili zao, wanaojua kucheza na kalamu, lakini wanawake wengi maskini hawakupata pesa hizi. Serikali iangalie zinapotoka pesa kama ni za kusaidia akina mama maskini na akina mama wa vijiji wasiojiweza, basi ziwafikie walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la watoto wa mitaani hili ni janga la Kitaifa na wala siyo janga la mtu mmoja wala la Wizara fulani. Najua watoto wengi hawa siyo kwamba wanatoka Mkoa wa Dodoma, watoto hawa wanatoka Mikoa mbalimbali ya Tanzania na hata wengine wanazalilishwa pale kwenye kituo cha mabasi Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu kwa makusudi kabisa, kuliko kuwasaidia watoto hawa amba wanalala katika Kituo cha Ubungo Dar es Salaam, wanawarubuni watoto hawa, wanawakogesha vizuri, wanaenda kuwafanyia vitendo ambavyo havina maana na kuwarejesha pale. Wengine hata wanafuatiliwa na raia wema na hata kukamatwa na kupelekwa kwenye vyombo vy ya sheria na hata magari yao kukamatwa lakini baadaye unakuta rushwa imeshapita katikati na gari lilishaondolewa na yule mtu haonekani. Kwa kweli watu kama hawa na Vyombo vy Ulinzi na Usalama viangalie masuala kama haya. Janga la watoto wa mitaani ni janga letu sote Watanzania wala siyo janga la mtu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa wanataka elimu, wanataka malazi bora, watoto hawa wanataka mahitaji kama watoto wa matajiri na watoto wa Kitanzania. Ukiangalia huku tunakokwenda kama hali hii itazidi kuendelea, kwa kweli hata wageni wetu wanaofika katika Jiji la Dar es Salaam wanaona wenyewe kwamba hii Tanzania imekuwa vipi, kwa sababu wote wale amba wanakaa Dar es Salaam wanaombaomba siyo kama wanapenda, haya ni matatizo ambayo yapo katika Mikoa yetu, Serikali za Mitaa na katika Halmashauri zetu. Tuangalie mapato yetu ya Serikali tutayapeleka vipi Mikoani kwenye Halmashauri zetu na kwenye Mikoa yetu ili kuhakikisha watoto hawa wanasaidiwa na wanapata elimu na maisha bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nzungumzie suala la afya, katika vituo vyetu vy afya ukifika huko ndiko kwenye rushwa kabisa na naomba Waziri utenge muda wako kutembelea Wizara hizi uangalie kwa sababu ukiwa maskini hupati huduma za afya, hata zile dawa za mseto utakuta unauziwa. Hili tuliangalie kwa makini, dawa hizi zinaletwa na Serikali ziwhudumie Watanzania walio wengi na siyo zichukuliwe na watu wachache kwenda kwenye *pharmacy* zao na kufanya biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni zito. Katika hospitali zetu kuna mambo mengi yanatendeka, unakuta mama anapanga foleni kuanzia asubuhi na anabaki kwenye kiti pale hajui aende wapi na cheti chake, hata zile *panadol* hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huo ndio mchango wangu na mimi sitaunga mkono bajeti hii mpaka mambo mengi muhimu hasa Zanzibar tupatiwe huduma zetu na tupatiwe haki zetu ndiyo nitaiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sasa nitamwita Mheshimiwa Vincent Nyerere na Mheshimiwa Janauary Makamba ajiandaye atafuatiwa na Mheshimiwa Ole-Sendeka na Mheshimiwa Modestus Kilufi ajiandaye.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo.

Awali ya yote, nawashukuru ndugu zangu wa Musoma Mjini hasa wana CCM wa Musoma kwa kuniletea mgombea ambaye ilikuwa rahisi sana mimi kumshinda.

Pili, nimshukuru Waziri Mkuu kwa hotuba aliyoitoa jana japokuwa sikubaliani nayo sana hasa kwenye ukurasa wa 62 aliposema kwamba Tanzania ni nchi mojawapo inayokua sana kiuchumi na umaskini unapungua, akawa amenukuu kitabu cha Mwandishi mmoja. Mimi bado sikubali, sijui Mwandishi huyu alichukua vigezo gani, hali za Watanzania zinazidi kuwa mbaya kila siku na vigezo ambavyo unaweza ukajua hali ya Mtanzania inakuwa mbaya kila siku ni hasa kwa Wafanyakazi wa Serikali wa Kada ya Chini kama Walimu, Polisi na wengine, nenda mwisho wa mwezi Benki ya *NMB* uangalie foleni iliyopo kwenye *ATM*, wale hawaweki faida wanatoa fedha, kwenda kulipa madeni na kunusuru maisha ya familia zao. Hali ya Walimu sasa hivi siyo tena ya kuweka faida, kwa hiyo, umasikini haupungui isipokuwa unaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri Mkuu kazi yake mmoja ni shughuli zote za hapa Bungeni, naomba sasa arudishe mahusiano mazuri kati ya Wabunge na Wabunge, tukubali ukweli unaosemwa na upande wa pili. Leo Mbunge wa CHADEMA akisema Cocacola ina sukari, CCM watakataa na tukipiga kura watashinda, lakini ukweli unabaki palepale. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri Mkuu ajitahidi kurudisha mahusiano na kuwaomba Wabunge wote tuwe tunakubali ukweli hasa unapotoka katika upande wa pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite katika shule zetu za Kata, huwa nawashangaa sana Wabunge wanaosifia Shule za Kata. Kazi ya Mbunge siyo kusifia Shule za Kata isipokuwa kuweka mikakati ya kuboresha shule hizi halafu sifa tuwaachie wazazi na watoto watakaoshinda katika Shule za Kata, lakini siyo sisi kusifia Shule za Kata. Kama tunataka kuzisifia basi watoto wetu wakasome pale. Shule hizi zimeandaliiwa kuwa shule za wapiga kura lakini wapigiwa kura hawasomi katika shule hizo na sisi Viongozi huwa tunarudi kule vijijini na maeneo mengine tunawajaza ndugu zetu vitu kichwani kwamba chagua mwenye elimu kwa sababu elimu bora haitoki katika Shule za Kata tunawaandaa watoto wetu sisi tulipo hapa wachaguliwe tena baada ya sisi. Leo ukiwaliza Wabunge hapa katika Shule za Kata za Jimbo lake, ipi inafundisha kilimo, ipi ni ya sayansi, ipi ya biashara, hakuna, zipo tu kiujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Wabunge, huu ni muda muafaka sasa wa kuhakikisha Shule za Kata zinakuwa bora. Zamani mtoto alikuwa akishindwa akaenda shule ya *private*, mzazi ana-struggle aende Shule ya Serikali, siku hizi imekuwa kinyume. Kama watu binafsi wanaweza Serikali inashindwa nini? Mimi nadhani tusipoteze muda kukaa tunasifiana sifa ambazo siyo za kweli, sifa ambazo hazitoki miyoni mwetu. Tushughulikie shule hizi. Nakubaliana na aliyeanzisha wazo hili, ni zuri sana lakini tusiridhike mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado matumizi ya rasilimali watu yana shida, tuna matatizo makubwa sana ya madawati, tuna misitu ya kutosha, lakini ukienda gerezani utakuta kuna wafungwa amba ni mafundi seremala wanapasua mawe, kwa nini wasitoke wakatusaidia kutengeneza madawati, hili linawezekana kama tutaweka utaratibu mzuri wa kuwasimamia na hakuna sababu ya Magereza ya Vijijini kulalamikia umeme wakati kuna kusanyiko la watu amba wanaweza wakatumia *biogas* kwa kinyesi chao wenyewe. Kuna vijana wengi wa Chuo Kikuu wana elimu hiyo, tunawaacha tu. Kwa hiyo, matumizi ya rasilimali watu hatujatumia vizuri. Magerezani kuna Walimu wamefungwa, sisi hatutetei uhalifu lakini hakuna sababu ya kumfunga Mwalimu halafu akapasue mawe au kuni wakati kuna shule zina upungufu wa Walimu. Tuweke utaratibbu mzuri aende kwenye shule zetu za Kata afundishe, muda wake ukiisha anarudi gerezani, lakini kuwaacha Walimu hawapo shulen i wapo gerezani wanapasua kuni ni matumizi mbaya ya rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina Mawaziri hapa kila mifano wakitoa wanatoa kwa maendeleo ya China, China imeendelea kwa *discipline* na adhabu kali walizowekewa, sisi bado *discipline* haipo, fedha za umma zinatumika ovyo. China hata rushwa ndogo unanyongwa. Nasikia wiki ijayo tunakuja kujadili habari ya *Radar*, tusifikiri kujadili tumedhulumiwa na Waingereza, tuwafikirie kwanza waliotufikisha hapa. Siku tukijadili mimi nitasikia raha sana waliotufikisha hapa wakiwa hawapo uraiani halafu sisi ndiyo tujadili. Kama kweli tunataka maendeleo kama ya Wachina, nidhamu na adhabu kali ziendane pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kusherehekea miaka hamsini ya uhuru, lakini mimi nasikitika sana mpaka sasa uhuru bado, pale Musoma Mjini tuna shilingi milioni mia moja themanini na tisa za programu ya maji miaka miwili wamekataa tusizitumie kwa sababu ni za wafadhali mpaka watupe ruhusa, sasa sisi tupo huru kwa lipi? Nimemwomba Waziri wa Maji anasema fedha zetu pale ni kidogo nyingi za Wafadhili. Sasa sisi tutazitumia kwa sababu watu wa Musoma Mjini wanataka fedha zile kwa ajili ya maji, hawataki lile gari lililoandikwa programu. Kiu ya maji haibadilishwi na gari. Waziri ukichelewa sisi tutazitumia na kama hao Wafadhili watatudai tuko tayari kuuza lile gari tulipe, zikipungua Waziri Mkuu atalipa lakini hatuwezi kukaa hatuna maji tunasema tuna fedha za Wafadhili halafu tumepewa hela tunaambiwa hatuwezi kuzitumia mpaka waamue wao. Kama tunasubiri waamue basi uhuru sherehekeeni wengine lakini Musoma Mjini tubaki maana hatuko huru kwa sababu Wafadhili hawajatuamulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa sipingi kwamba CCM hajafanya mambo mazuri, yapo mazuri ambayo CCM na Serikali yake imefanya, lakini pia mkubali kwamba mambo haya mazuri waliotangulia kuyafanya wenzenu ninyi mnayaharibu. Sisi hatupingi, tunachoppinga ni yale mazuri ambayo wenzenu wameanzisha mnayaharibu. Kwa mfano, mbio za Mwenge zilianzishwa kwa nia nzuri tu, lakini hapa tulipofikia hata umuhimu wake sasa haupo. Zamani mbio za Mwenge zilikuwa ni kumulika walangazi, wahujumu uchumi na wengine lakini siku hizi haumuliki unawamulikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msafara mkubwa wa mbio za mwenge, kinachofanyika hakionekani, tunachagishwa fedha, hatusomewi zimekusanywa kiasi gani na zimetumika kiasi gani kwenye mbio za mwenge. Kabla sijachaguliwa walikuja kwangu, mimi ni mjasiriamali, wanataka fedha za mchango wa mbio za mwenge (mafuta ya Mwenge), nikawaambia chukueni kigaloni tukawape mafuta, wakakataa wanataka hela. Nikawaambia tokeni, hela sitoi na Mwenge ukipita kwangu zima kwa sababu sijachanga mkawashie mbele. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kuukimbiza mwenge kwa madhumuni aliyoyatengeneza Baba wa Taifa, tuhakikishe unamulika siyo kuwamulikia mafisadi. Hatuna sababu ya kupeana majina wengine sijui nini, wakati hatutaki kuchukua uamuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Polisi wetu wana hali ngumu sana, kuna fedha wanachangishwa shilingi elfu tano wanasema za mazishi na wanachangishwa bila wao kupenda. Mshahara wa *RPC* na *Constable* haufanani lakini wanachangishwa wote shilingi elfu tano. Kama kuna mchango wa namna hii basi waangalie ukubwa wa mshahara wa Askari husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna shida, fedha hizi zinachangwa kwamba ni fedha za mazishi wakati wao ni wafanyakazi wa Serikali, ni jukumu la Serikali kuwazika kama wamepata matatizo wao na wategemezi wao lakini siyo wao wajizike wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri Mkuu kwa sababu anahuksika moja kwa moja na uteuzi wa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, kuna Vyeo vya Zawadi na Polisi wapewe. Sijawahi kusikia Polisi au *RPC* mstaafu au Afisa Magereza amekuwa Mkuu wa Mkoo au Mkuu wa Wilaya. Kama ni lazima wapewe Askari, basi watoe waliopo kazini, hawa waliostaafu wamekwishachoka, wamepata kiinua mgongo, hawana uwoga tena wa kupoteza haki zao kwa sababu kiinua mgongo walishaweka mfukoni, unampa Mkoo au Wilaya anaweza kufanya vibaya tu kwa sababu hakuna cha kumwogopesha na kiinua mgongo cha kwanza alishachukua anasubiri kiinua mgongo cha pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali iangalie uteuzi wa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kama ni Askari wanatakiwa, basi Akari Magereza na Polisi pia wapewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaunga hoja mkono kama haya niliyoyasema yatatekelezwa. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru, anayefuata sasa ni Mheshimiwa January Makamba.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa fursa hii ya kuzungumza katika Bunge lako Tukufu. Ninayo mambo kadhaa ya kuzungumza na nitaanza na yale walijonituma wananchi wa Jimbo la Bumbuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Bumbuli wanataka Wilaya yao. Kwa muda mrefu tumekuwa tunaomba, mchakato ulianza tukaambiwa vigezo bado. Tukaendelea ni miaka kumi sasa, vigezo bado, tukakata tamaa, lakini baadaye tukaomba ushuri tukaambiwa basi ombeni Halmashauri. Tukaitisha Baraza la Madiwani tukapisha Azimio kwamba tuwe na Halmashauri. Wilaya yetu ya Lushoto ina Madiwani 64, hata kuendesha kikao cha Baraza ni tatizo. Tumekuwa tunasikia haya maeneo mapya ya utawala yanatajwa, sisi pamoja na kuomba tunapitwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefadhaika na tumenyong'onyea kwa sababu tunaposukuma hili jambo ni kwa sababu sisi ni viongozi, siyo kwamba naomba suti yangu ila naomba Serikali isogee karibu zaidi na watu ili huduma zipatikane na maendeleo yakue kwa haraka. Kule kwangu Bumbuli uhusiano wa baadhi ya watu wangu na Makao Makuu ya Wilaya ni wakati wakienda kufungwa katika Geraza la Wilaya kwa maana gereza ni moja. Lakini wako watu pale wanakua, wanazeeka hawana mahusiano yoyote na Makao Makuu ya Wilaya yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeongea na viongozi wa Serikalini, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekuwa msikivu, ameonesha dhamira ya kusaidia. Nisiseme mengi ila tunayo mategemeo, watu wake amewaambia wamletee vigezo, wamesema Bumbuli bado haifikii vigezo, akawambia sasa wakatulee ni vigezo gani, kwa taarifa zangu mpaka sasa hivi hawajamletea. Sasa, aidha hawaoni umuhimu wa jambo lenyewe au wanataka lipotee tu hivi hivi. Haya mambo yanasicitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu kule wanakipenda sana Chama cha Mapinduzi, lakini tunawakwaza kwa sababu tunaposema vigezo tunajua kwamba zipo sehemu ambazo vigezo bado lakini wamepata. Serikali imezingatia sababu nyingine za msingi tu za kufanya uamuji huo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, amefika kule, anapajua. Naomba watendaji wake, naomba Waziri Mkuchika naye aende akaone ile milima, akaone zile barabara, akaone jinsi gani kazi ya kuleta maendeleo inavyokuwa ngumu kutokana na huduma kuwa mbali na watu. Ni mategemeo yangu kwamba ndani ya mwaka huu kwa sababu kuanzisha Halmashauri ni uamuji wake tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, hata kesho anaweza kwa sababu anasaini tu *Government Notice*. Naamini ananisikia na ananisikiliza na watu wa Bumbuli pia wanasiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la elimu. Sisi wengine tumebahatika kupata elimu nzuri. Lakini tunao wadogo zetu sasa hivi wapo kwenye hizi shule za sekondari ambazo tumejenga nyingi tu. Bunge hili na Serikali ya nchi yetu haitawatendea haki kama watakuwa wanakwenda shule katika masomo tisa wanao walimu wawili. Mtihani ukija pale mwisho wa mwaka au mwisho wa elimu hiyo ya sekondari au elimu ya msingi wanafanya mtihani katika masomo ambayo hawakufundishwa. Nadhani tuamue kwamba Bunge letu hili, urithi wake uwe ni kuboresha elimu kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina shaka kwamba tunatengeneza Tanzania mbili ndani ya moja kwenye masuala ya elimu. Ukiangalia taarifa za Serikali *public expenditure tracking survey* inaonyesha kwa kadri shule inavyokuwa mbali na mjini, kwa kadri inavyokuwa mbali na Makao Makuu ya Wilaya, ufaulu ndio unakuwa mdogo, matumizi ya fedha kwa kila mwanafunzi ndio yanakuwa mdogo na walimu ndio wanakuwa wachache. Shaka yangu ni kwamba, wakati tunapanua miundombinu ya elimu tuna kundi la Watanzania wanaosoma maeneo ya Vijiji ambao hawapati elimu bora sawa na wenzao wanaosoma maeneo ya mijini. Sasa kama tunaongea mambo ya usawa na msingi wa kujenga hizi shule kwenye kila Kata ni usawa, kwa maana kwamba watoto wa Tanzania bila kujali wanapoishi wapate elimu, basi ubora wa elimu hiyo na wenyewe uwe sawa, ndio chama chetu Chama cha Mapinduzi kinavyoagiza. (*Makofî*)

Kwa hiyo, nimesoma Hotuba ya Waziri Mkuu, nimesikiliza Hotuba ya TAMISEMI, sijaona *ambition* kubwa ya kuboresha elimu kwa watoto wetu. Tuondoke kwenye kujali *input* zaidi, majengo zaidi, maabara zaidi, vyoo na mabati twende sasa kwenye kutazama je, elimu inayotolewa kwa watoto wetu inakidhi mazingira ya dunia ya sasa na dunia inayokuja? Bahati nzuri nikitembelea shule hizi kwenye Jimbo langu huwa natazama madaftari ya wale wanafunzi. Naomba Waheshimiwa Wabunge, wengine tufanye hivyo ndipo utakapoona kwamba tuna tatizo. Takwimu ni nzuri, tumezitoa kwenye jedwali hili. Ipo takwimu inasema kwamba waliofanya mtihani mwaka jana ni 894,000, waliochaguliwa awamu ya kwanza na ya pili, 447,000 hawa wengine 416,000 wamekwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 watoto ambaو hawakufaulu darasa la saba ni 500,007. Mwaka 2009 ni 500,005. Kwa hiyo, tunapoandika kwamba waliofanya mtihani na waliofaulu, tuandike ambaو hawakufaulu na tujue wanakwenda wapi. Kila mwaka ukiwa na watoto 500,000 wa darasa la saba ambaو hujui wamekwenda wapi na kwa sababu elimu ya darasa la saba haiwapi *skills* za ku-manage maisha yao na hili na lenyewe tulitazame sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina mapendekezo kadhaa hapa, la kwanza, ili kuboresha mfumo wa elimu tubadilishe *incentive structure* nzima kwa maana ya jinsi walimu wanavyolipwa. Kwa hali ya sasa wakienda shule, wasipokwenda shule, watoto wakifaulu au wasipofaulu mshahara wao uko pale pale. Sasa kwenye kazi nyingine huwa siyo hivyo, tunapimwa kwa *performance* na kwa walimu iwe hivyo hivyo. Lakini nataka tuwalipe walimu fedha zaidi hasa wale wanaokwenda kufundisha kwenye mazingira magumu kwa sababu tunajua jinsi ilivyo shida kuvutia walimu kuja sehemu kama

Bumbuli. Kama ni mshahara tuwalipe *double* au mara tatu ili na sisi tupate walimu wa kutosha na walimu wazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka sasa tuiondoe Kurugenzi ya Ukaguzi kwene Wizara ya Elimu, iwe ni Kurugenzi Huru kama alivyo CAG kila mwaka walete ripoti ya ubora wa elimu kwa kila shule kwa kila mwanafunzi. Ripoti tuione ni shule gani zinafanya vizuri na kwa sababu gani, wanafunzi gani wanafanya vizuri, wanafunzi gani hawafanyi vizuri na sababu ni zipi? Ripoti ijadiliwe na nchi nzima kwa sababu suala la elimu siyo suala dogo. Hii inawezekana kama Kurugenzi hii itakuwa Kurugenzi Huru. Lakini sasa tubadilishe mfumo, hatuwezi kupata maendeleo makubwa kwenye elimu kama wanaokwenda kwenye ualimu ni wale waliopata *division four* na *division three*. Wale wanaofanya vizuri kabisa wanakwenda kwenye mambo mengine, ualimu unaachiwa kwa wale ambao wanasesma basi bwana nenda ualimu. Sasa tunataka tuwakabidhi watoto wetu watu ambao ni *the best in the bright*. Ualimu iwe ni kazi inayolipa kuliko kazi yoyote katika mfumo wetu wa Serikali. Wawe wanakwenda watu ambao katika nchi yetu ndio wamefaulu vizuri na inawezekana. La sivyo tutakuwa tunaongea tu juu juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napendekeza sasa tuunde Tume au Kamisheni ya kutazama upya mfumo wetu wa elimu nchini, kutazama mihula, kutazama tunavyopata walimu, kutazama tunavyotumia fedha za walimu. Sasa hivi kila mwanafunzi wa shule ya msingi kila mwaka anapangiwa shilingi 10,000 kama ruzuku. Sekondari shilingi 25,000, fedha hizi hazifiki kwa wakati, matokeo yake ni kwamba vitabu havitoshi. (*Makofi*)

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu nilikuwa nashangaa, kila shule ya msingi Tanzania hii ina akaanti, kwa nini fedha zisitoke Hazina kwenda moja kwa moja kwenye shule na taarifa zikawa wazi kwamba leo tarehe fulani fedha zimehamishwa kutoka Hazina kwenda kwenye shule ya msingi na zijilikane zinavyotumika.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Makamba. Sasa hivi namwita Mheshimiwa Ole- Sendeka na wafuataao wajiandae. Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa na Mheshimiwa Capt. John Komba.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE- SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Awali ya yote kwa kuwa siku ya leo ni siku yangu ya kwanza tangu nilipopata ridhaa ya kurejeshwa katika Bunge hili kwa mara ya pili naomba nichukue nafasi hii ya kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu hasa ukizingatia kwamba niliaga kwenye Bunge hili nakwenda likizo ya miezi mitatu baada ya hapo ningerejea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliaga hivyo kwa sababu nilijua kwamba wananchi wa Simanjiro wako na mimi na ushahidi wa kutosha ni kupitishwa bila kipingwa kuwa Mbunge wa Jimbo hilo na kuwa mionganoni mwa Wabunge wachache waliopita bila

kupingwa. Lakini jambo lingine ni kwamba Biblia inasema nayaweza mambo yote katika ye ye anitiae nguvu. Lakini inasema pia walio wangu sitawafanya kamwe kuwa mkia bali nitawafanya kuwa kichwa. Nilikuwa napata faraja nikija dhahiri kuwa Mwenyezi Mungu hawezi kunitupa katika majoribu yaliyokuwepo, ndio maana leo niko pamoja nanyi.

MBUNGE FULANI: Haleluya.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE- SENDEKA: Ahadi yangu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, ni kutimiza wajibu wa mwakilishi aliye makini kwa kusimamia mambo yenye maslahi kwa wananchi wangu na Watanzania kwa ujumla wao kwa kuyapa sauti matarajio yao na ya wananchi wa Tanzania bila kuogopa wala bila kumwomba radhi mtu ye yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, nimesimama hapa nikikumbuka kabisa na kutambua kwamba tulitoka kwenye uchaguzi mkuu. Waswahili wanasema chanda chema huvisiwa pete na si stahili ya kichwa cha jogoo kuvisiwa kilemba. Niruhusu nichukue nafasi hii ya mwanzo kuwashukuru Watanzania kwa kuendelea kuchagua Chama changu, Chama cha Mapinduzi na kumpa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, ushindi wa kishindo, narudia kusema ushindi wa kishindo maana ushindi wa zaidi ya asilimia 60 ni ushindi wa kishindo, kama wenyе asilimia 20 wanazunguka Tanzania nzima na kutamba na kufurahi, sisi tulipata zaidi ya asilimia 60 kwa nini tusijitambue kama ni ushindi wa kishindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kabla sijarejea mambo ya Jimbo langu, naomba nizungumzie moja linalotuhusu sisi sote. Nilikuwa nasoma katika Gazeti la Mwanahalisi, pia narejea katika baadhi ya mitandao, kuna tabia mbaya ya watu wasiokuwa na ubinadamu, watu wasiokuwa na shukrani, wanazunguka na kumtukana Baba wa Taifa kupitia mitandao ya hovyo wakimtaja Mwalimu Nyerere kama mmoja ya viongozi madikteta, viongozi wasiosikia ushauri, wakimwita haambiliki na kwa maana hiyo nataka nichukue nafasi hii kwa niaba ya Watanzania kuitaka Serikali ya Chama cha Mapinduzi ifanye uchunguzi na kubaini juu ya maharamia hawa wanaochafua jina la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye ataendelea kuwa alama ya kutukuka ya Taifa letu na Bara letu la Afrika. Mtueleze ni nani baada ya uchunguzi huo ili kama ni maadui wetu wa nje tuwatenge, kama ni maadui wetu wa ndani tuwazomee na kujitenga nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, nachukua nafasi hii kurejea baadhi ya mambo ya msingi ya Jimbo langu niliyotumwa na wana Simanjiro. Jambo la kwanza ni kwamba, mwaka huu hali ya ukame inaendelea katika Jimbo letu la Simanjiro. Lakini bado ni matarajio yangu kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, itaendelea kuwatupia macho wananchi wa Simanjiro ili kuhakikisha kwamba hakuna binadamu ye yote atakayekufa kwa njaa.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, ni rai yangu pia kwamba Serikali itachukua changamoto hii kwa kuhakikisha kwamba baadhi ya vijiji vinavyopitiwa na Mto Ruvu ambavyo vina maeneo mazuri ya umwagiliaji vitapewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka huu ili tuweze kupata chakula kwa wakati wote. Vijiji hivyo sitaona haya

kuvitaja ni Kiruani, Msitu wa Tembo, Kambi ya Ichokaa, Ngage, Roibosoiti, Ngunge na Ruvu Remiti. Tuko katika ukanda mzuri ambao tungeweza kuwezesha kwa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji ambapo hali yetu ingekuwa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia baada ya kutoa ombi langu kwa Serikali yetu ambayo nina hakika ni Serikali sikuvi, nikumbushe pia juu ya tatizo kubwa la maji. Tumezungumza na wenzetu wa *BADEA* na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, ametuongoza kwenye hili na Waziri wa Maji Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, tumezungumza pia na wenzetu wa Kampuni moja ya Ufaransa *Elips Projects*, naomba sana Wizara ya Fedha iendelee kumalizia mazungumzo na watu wa *Elips* ili mradi huo uweze kuanza, tuweze kuvuta maji kutoka Mto Ruvu na kupeleka maji Olokesmeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru Serikali, imeweza kuwezesha upatikanaji wa shilingi bilioni 1.8 katika mradi wa dharura wa kunusuru maisha ya wananchi wa Wilaya ya Simanjiro. Nina kila sababu ya kumshukuru sana Waziri Mkuu na Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa niaba ya wananchi wa Simanjiro. Tatizo la maji Wilayani Simanjiro ni kubwa sana maeneo ya Mererani hali yake ni mbaya, Kata ya Inesinye hali yake ni mbaya, Kata ya Shambalai hali yake ni mbaya, katika maeneo matatu haya niliyoyataja watoto wanakunywa maji yanayosababisha miguu kupinda. Ni rai yangu kwamba Serikali yetu itawezesha kupatikana kwa maji ya mradi ule wa Hai yaliyofika katika uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro ambao ni kilomita 20 tu kutoka Mji wa Mererani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabisa kwamba, Serikali yetu ni sikuvi. Nataka nichukue nafasi hii pia kuiomba Serikali kama unavyofahamu wafugaji wa Kanda ya Kaskazini walipatwa na ukame miaka miwili iliyopita na Serikali iliahidi kuangalia uwezekano wa kuwapa kifuta machozi. Serikali yetu ilitenga shilingi trilioni moja *point* saba kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wakulima wetu hawataathirika na mtikisiko wa hali ya kiuchumi duniani. Nashukuru kwamba kwa hatua hiyo ya kijasiri. Lakini ni rai yangu pia kwamba, nategemea Serikali yetu itawatazama wafugaji ambao walipoteza mifugo yao na kwa kweli nitangulize kusema Jimbo la Longido na Wilaya ya Longido, hali yao ni mbaya maana umaskini uliotokea umezidi. Sisi wengine wa Wilaya ya Simanjiro, Kiteto na Ngorongoro na Wilaya za Mwanga na Same na Wilaya ya Hanang, tulipoteza mifugo lakini angalau bado tunayo kidogo. Rai yangu ni kwamba, Serikali ione uwezekano wa kuwapa kifuta machozi wafugaji wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama Serikali itenye shilingi trilioni 1.7 lakini kulingana na ripoti ya *Controller and Auditor General* ziko shilingi bilioni 48 ambazo matumizi yake hayajawa wazi. Naomba Serikali iweke bayana juu ya ubadhirifu huo ulioripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali. Bilioni 48 ni fedha nyingi, tunataka kujua fedha hizo zilitumikaje. Kama zimetumika kwa njia ambazo hazistahili wanaohusika wachukuliwe hatua za kijasiri ili waweze kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima wakati mwengine tufanye maamuzi kama alivyosema Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa leo asubuhi. Siyo kwamba amesema

leo tu peke yake ni msimamo wa Chama cha Mapinduzi na Serikali yake kutaka wale ambao wanafisadi, wanaohujumu uchumi wa nchi yetu wachukuliwe hatua. Napoleon aliyekuwa Kiongozi wa Ufaransa aliwahi kusema naomba kunukuu kwa ridhaa yako: "Wakati mwingine ninakuwa na hulka za mbweha na wakati mwingine hulka za Simba, Serikali nzuri na ya welevu ni ile inayofahamu ni wakati gani wa kuwa mbweha na ni wakati gani wa kuwa simba".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeamua kunukuu kauli hii ya Kiongozi wa zamani wa Ufaransa Napoleon ni kwa sababu najua wazi kwamba, kuna haja ya Serikali yetu kuchukua wakati mwingine ukali wa simba, katika baadhi ya mambo ya msingi na hasa pale ambapo tunapata watu wanaotuingiza na kuiingiza nchi yetu kwenye mikataba isiyokuwa na tija isiyokuwa na maslahi na nchi yetu. Katika Bunge hili tumesikia juu ya Mikataba ya Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro na jinsi ambavyo baadhi ya watu waliotuingiza kwenye mikataba hiyo ambayo Serikali ilisema haina mpango wa kuwachukulia hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hamwezi kupiga vita ufisadi, wakati watu wanatuingiza kwenye mikataba ya hovyo na watu hao hao wanaruhusiwa kutoka na kuendelea na mali walizozikwiba na bado hakuna hatua zinazoweza kuchukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kwamba kuanzia sasa Serikali yetu itakuwa na ukali wa simba kwa watu wanaotuingiza katika mikataba isiyokuwa na tija kwa maslahi ya nchi yetu. Ni rai yangu pia na ni ombi kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tutunge sheria sasa ambayo itatamka tangu mwanzo kwamba mali zote zinazopatikana kwa njia ambazo hazina maelezo kwa viongozi waliopewa dhamana ya umma ambazo hawawezi kuzielezea wamezipata wapi wao na watoto wao zitamkwe kwamba ni mali za Taifa, vinginevyo Bara la Afrika litaendelea kuwa viongozi ambao watalimbikiza mali kwa manufaa yao na wajukuu wao wakati Taifa linaendelea kuangamia, wimbi la ufisadi sasa hivi ni kubwa katika Bara la Afrika na katika baadhi ya nchi zetu maskini duniani. Hatuwezi tena tukalia, tukamnyoshea na kumpigia magoti Mwenyezi Mungu kwamba sisi ni maskini, wakati mwingine sisi wenywewe ni sehemu na chanzo cha umaskini tuliokuwa nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa *ALAT* Taifa na wenzangu Madiwani walinituma niwasilishe kilio chao cha kuhakikisha kwamba maslahi ya Madiwani yanaboreshw. Lakini jambo lingine mnakumbuka kwamba tunao utaratibu wetu wa ugatuaji, wa kupeleka madaraka karibu na wananchi, ni rai yangu kwamba kulingana na maombi ambayo nina hakika yamewasilishwa kwa Waziri Mkuu, kwamba kuanzia sasa *Secretariat* ya Ajira na Wakala wa Manunuzi ambao sasa unapelekwa Dar es Salaam na maeneo mengine ya Kanda, huko ni kunyang'anya mamlaka, Halmashari zetu za Wilaya badala ya kuziwezesha zifanye kazi katika maeneo hayo. Ni rai yangu kwamba, haya nayo yatapewa kipaumbele na Serikali yetu sikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine ambalo ningependa kuligusia kwa sasa nalo ni hatua nataka nikamilishe hilo la uchukuaji wa hatua. Nilipokuwa naondoka kwenye Bunge hili nilisema nitakaporejea tutaendelea na msimamo ule ule wa kutetea

maslahi ya Watanzania. Bado nauliza walioitungiza katika mikataba, walioweza kuchukua fedha kutoka katika Benki Kuu ya Tanzania, wengine wamefikishwa Mahakamani, kuna wengine bado hatujasikia, tunasubiri kusikia na wao wakifikishwa huko. Tunataka kujua waliochukua fedha za kampuni ya *Deep Green Finance* walioko mitaani wakizunguka, kwa nini wanaachwa, hatuwezi kusema tunapigana vita dhidi ya ujisadi wakati tunatazama sura za baadhi ya mafisadi na tunaangalia hadhi ya baadhi ya mafisadi, ni lazima waliohusika kuiba fedha za *Deep Green Finance* na KAGODA wachukuliwe hatua na Watanzania waweze kuridhika. Kutokufanya hivyo sio kurejesha imani kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme wazi jambo moja ili tufike mahali tuelewane. Haiwezekani ukapenda kuhusishwa na mafanikio maana hapa wote tunapenda tuhusishwe na mafanikio mazuri, hakuna ambaye hataki ahushishwe na mafanikio, uwepo wa Chuo Kikuu cha *UDOM*, hakuna ambaye hapendi kuhusishwa na mafanikio yaliyofanywa na Serikali ya CCM na hakuna namna ambayo unaweza kutenganisha mahusiano hayo na Serikali iliyoko madarakani, kama ambavyo huwezi kutenganisha mazuri yaliyotendeka katika kipindi cha uongozi wa Serikali iliyoko madarakani, ndivyo ambavyo inakuwa ni vigumu kutenganisha uozo na uovu unaotokea katika kipindi ambacho umepewa dhamana. Namna pekee ya kuweza kujitenga na uozo huo na ujisadi huo ni kwa kuchukua hatua madhubuti ili uonekane wewe sio sehemu, ukiacha kuchukua hatua madhubuti dhidi ya mafisadi kwa kutazama sura utaonekana wewe ni sehemu. Serikali yetu haiwezi kuwa sehemu ya kunyooshewa kidole wakati walionufaika ni watu wachache, tuondoke hapa na Bunge hili lisimame kwa miaka mitano, liwasemee Watanzania bila kuangalia sura za waliotenda haya. (*Makofi*)

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge walishangilia kwa kupiga vigelegele*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, MEREMETA, nenda Buhemba leo walioko Buhemba madini yanayochimbwa yanapelekwa kwa wageni nje, yanachimbwa na kufadhiliwa na makampuni ya nje kwa kisingizio kwamba wanaochimba ni wachimbaji wadogo, leseni ya MEREMETA imeondolewa wamepewa wenzetu wa *STAMICO*, lakini *STAMICO* mpaka leo hawajaingia, madini yanayovunwa pale yanawanufaisha jirani zetu na wanaochimba ni wachimbaji wadogo. Nataka kuiomba Serikali na namsubiri Mheshimiwa rafiki yangu Ngeleja, wakati wa bajeti yake kama hapatakuwepo na maelezo ya kutosha ya Buhemba, kama hapatakuwepo na maelezo juu ya ujisadi wa MEREMETA, hapa hapatatosha kama alivyowahi kusema Mama Anna Kilango, tutabanana mpaka kieleweke. (*Makofi*)

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge walishangilia kwa kupiga vigelegele*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa samahani sana, shangilieni, lakini vigelegele hapa sio kwenye kilabu, tuko kwenye eneo Takatifu sana. Endelea.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kutoa maelekezo. Nataka nimwombe Waziri Ngeleja najua ni msikivu na ni mchapa kazi na siwezi kutilia mashaka uadilifu wake, tumeanzisha Wakala wa Nishati

Vijijini, bado wananchi wa Kata za Msitu wa Tembo katika vijiji vya Msitu wa Tembo, Kiruwani, Madgadini, Ngoreka A, Ngoreka C, Kariat wanasubiri ukamilishaji wa mradi ule. Wananchi wa Kata wa Naberera, Namalulu, Lendanai, Tera, Tweiborokishul, Ololokare, Loiboisol wote wanasubiri kuona kwamba mradi Wakala wa Umeme Vijijini tunawafikishia umeme hawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia suala la maendeleo yenyewe uwiano. Hatuwezi tukaleta maendeleo kwa Watanzania bila kuangalia kiwango cha maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Maeneo ambayo yako nyuma ni vizuri tukawa na mpango mahususi wa kuzisaidia jamii hizo ili ziweze kwenda kwa kasi ile ile ya wale wengine. Hatuna sababu ya kuwanyooshea kidole waliowahi kutangulia, kwa sababu walitumia fursa vizuri na pengine waliweza kunufaika kufikia hatua hiyo kutokana na keki ya nchi, nao kupata nafasi ya kwenda shule, tusaidieni basi na sisi wengine kwamba sasa tuwapatie wafugaji anuani za uhakika kwa kuwapatia maji kwa ajili ya mifugo yao na wao na kwa ajili ya wafugaji wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutumie nafasi hiyo hiyo pia kuwa na mpango mahususi wa kusaidia ujenzi wa shule zile za sekondari, mabweni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya maeneo ya Wilaya zetu ambazo ni kubwa umbali kati ya kijiji hadi kijiji ni kilometra kati ya arobaini mpaka sabini. Kwa maana hiyo shule zote za Kata ni za bweni na kwa maana hiyo Serikali iwezeshe upatikanaji wa hosteli na nyumba za Walimu katika maeneo hayo ya wafugaji ili watoto hao wa wafugaji nao waweze kupata elimu na waweze kupata ajira katika maeneo yanayohitaji elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kugongewa kengele, najua imekaribia, lakini nataka niseme jambo moja la mwisho. Tumepewa dhamana, tuitumie vizuri. Miaka hii mitano ya Bunge hili, tutimize wajibu wetu kama wawakilishi walio makini, katika mambo ya msingi tuache ushabiki, tukubaliane kwenye mambo yenyeye maslahi kwa nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka nimsaidie sana rafiki yangu Freeman Aikaeli Mbewe, naipongeza sana hotuba yake japo mengi siyakubali. Ni lazima na vyama hivi navyo vya Upinzani vijitambulische vinasimamia wapi maana wakati mwingine mnasimama, ninyi tunawajua mnasimama katika mrengo wa kulia, lakini mnanukuu mambo ya mrengo wa kushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekatiwa, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana anayefuatia sasa hivi ni Mheshimiwa Kilufi.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba nishukuru sana kwa kupata nafasi hii lakini niwashukuru sana ndugu zangu wananchi wa Mbarali kwa kunipa heshima hii kubwa ya kuwawakilisha hapa Bungeni na naahidi kwamba sitawaangusha, naomba ushirikiano wao, tuendelee kushirikiana nao vizuri, Mwenyezi Mungu atatujalia tufike pale ambapo tulikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami niipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa Mpango ambao ultingazwa rasmi wa maendeleo, lakini vile vile nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Kamati ya Bunge ya Fedha pamoja na ndugu yangu Wasira, Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Rais kwa mipango mizuri na taarifa nzuri ambayo waliitoa ambayo kwa kweli inaonyesha sura na dalili nzuri ya kupiga hatua ya maendeleo. Ni ukweli usiopingika kwamba ukitaka maendeleo maana yake ni lazima kwanza uji-*tune* kutoka kwenye hatua uliokuwa nayo kwenda mbele, tumefanya mambo mengi ni kweli, lakini bado haitoshi kama hatutabdalika. Tatizo la Tanzania ni kwamba tuna mipango mingi mizuri, lakini kwenye usimamiaji bado tuko nyuma. Naomba mipango hii iende pamoja na kujibadilisha sisi wenyewe, tuache kufanya mambo kwa mazoea, tukubali kuwa ni lazima tubadilike, mazoea hayo kama ni mazuri basi Watanzania watatuunga mkono, lakini mazoea yetu kama sio mazuri, nina hakika hawa Watanzania itafika siku tutaaachana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana bajeti iliyosomwa na Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa imezingatia mambo mengi ya msingi kwa maendeleo ya Watanzania. Upande wa kilimo kuna miradi mingi ambayo kimsingi naomba nishukuru sana na napongeza sana bajeti hii kwa sababu imetaja maeneo mengi ya kilimo katika Jimbo langu la Mbarali, ndugu zangu ni ukweli usiopingika kuwa Wilaya ya Mbarali ni *potential* kwa kilimo kwa nchi hii. Mbarali kama inatunzwa vizuri, inaangaliwa vizuri tunaweza tukalisha Taifa hili. Kuna maeneo mengi mazuri, mchele wote unaoliwa Dar es Salaam unatoka Mbarali, sifa ya Mkoa wa Mbeya kwa upande wa kilimo cha mpunga sehemu kubwa mpunga mwangi unatoka Mbarali. Kwa nini tusiweke mkazo na kusimamia vizuri mabonde mazuri ambayo yanaweza kulilisha Taifa hili. Niipongeze sana Serikali kuwa tumepata miradi mingi kwenye maeneo mengi ambayo *scheme* hizi nikizitaja muda hautatosha, ni nyingi. Kwa kweli niipongeze sana Serikali imeona umuhimu wa kuliendeleza Bonde la Mbarali kwa ajili ya kulisha Watanzania, kwa ajili ya kunusuru uchumi wa Taifa kwa maana ya kuendeleza kilimo kwanza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi ambayo wana Mbarali tunaishukuru Serikali. Upande wa miradi ya barabara, vilevile kuna miradi mingi, ombi langu ni kuwa, miradi hii ambayo imeainishwa iweze kupewa fedha kama ambavyo bajeti imetolewa. Vile vile *scheme* nyingi za umwagiliaji ambazo nyingine zinaendelea kuboreshwa lakini zilikosa fedha na nyingine ambazo zitakosa fedha baada ya bajeti hii, naomba kwa nguvu zote Serikali iangalie jambo hili muhimu kwa uchumi wa Taifa ili kusudi miradi hii yote iweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda sana uwekezaji, lakini uwekezaji huu tuuangularie una tija gani kwa wananchi wetu na hasa mahali ambapo uwekezaji huu unapelekwa. Lakini kama tutakuwa tunaangalia maslahi tu ya wawekezaji bila kuangalia wananchi ambao wanazunga maeneo ya miradi hiyo, tutakuwa tunawatafutia umaskini Watanzania ambao kuna siku watatukatalia hawatakubaliana na sisi, ushahidi upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi kule Mbarali walitaka wachukue lile shamba wenyewe kwa sababu ardhi ile waliitoa wenyewe kwa Serikali, likawa shamba la *NAFCO*, baada ya hapo Serikali imeshindwa, wakataka kulichukua lile shamba ili waendeleze kilimo, wakaambiwa hapana, tunataka sasa hivi miradi yote tuibinafsishewapewe wawekezaji, shamba lile alipopewa mwekezaji zile neema ambazo Baba wa Taifa aliziweka wakati linaanzishwa, zote zikaondolewa, hawa wana Mbarali waende wapi? Uwekezaji kwao umekuwa balaa! *Waka-react*, kilichotokea Mbarali mnafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kuwa baada ya lile shamba kuchukuliwa kutajengwa *intake* nyingine ambayo itawasaidia wananchi wale ambao kwa sasa hawana sehemu ya kulima. Kuna *intake* ya Mwendantitu, nilikuwa nikiangalia utekelezaji wake unakwendaje. Ndugu zangu bado sijaona dalili kwa sababu fedha zilizotekeleza mradi ule Bajeti iliyopita hazikuja. Sasa hivi sijajua ni kiasi gani nimeangalia bado sijaona. Lakini kwa upande wa Halmashauri ilitimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishe ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla, wana Mbarali hawatakubali kudhulumiwa kama huu mfereji hautatengenezwa na wananchi wale wakapata sehemu ya kulima. Itakuwa uwekezaji umeleta umaskini kwao, kitu ambacho hawatakubali, mtawaua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi tumeshuhudia maeneo mengine kama Babati, tumeshuhudia Watanzania wamekataa kabisa kuwa haiwezekani ardhi yetu ikaenda na sisi tukabaki maskini. Hali ile siyo ya kuiachilia, ni vizuri tukaikabili, tukaona ukweli uko wapi, wananchi wale tusiwabeze. Hali hiyo ndiyo iliyotokea na Mbarali, wana Mbarali ndugu zangu nataka niwahakikishie kama mfereji ule wa Mwendantitu hautachimbwa yule mwekezaji hawatamwacha, wataendelea kupambana naye mpaka na wenyewe wapate riziki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie, upande wa *NAFCO* Kapunga, bahati nzuri nilikuwa na maeneo mawili, yule bwana kidogo ameanza kuwa mstaarabu. Naona mahusiano na wananchi kidogo yanaanza kuwa mazuri, lakini kama hali hii haitajirekebisha, basi Watanzania itafika siku huu uwezekaji itaonekana kama kwao tumewaletea msiba. Kwa hiyo, naomba hali hii iangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbarali kwa maana ya Ubaruku, ni maeneo ambayo yana mitambo mikubwa ya kukoboa mpunga. Kuna viwanda zaidi ya kumi nikihesabia na kile cha mwekezaji. Lakini barabara ile ambayo inaleta uchumi mkubwa kwa Taifa mpaka leo iko katika kiwango cha changarawe ambacho hata ukitengeneza miezi miwili haiwezi kuendelea kuhimili. Mizigo ya mchele inayotoka hapo kulisha Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine hapa Tanzania. Tumeanza kwa *TANROAD* wanajisukuma kidogo kidogo, kalami ka hapa na pale kilomita mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza wanajitahidi, sasa hivi wanakwenda kilomita moja na pointi nane (1.8). Lakini mahali penyewe pana kilomita 17 tu. Kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuimarisha barabara hii kwa kiwango cha lami, mahali ambapo uchumi mkubwa wa nchi unapatikana. Kila siku pale gari 15

mpaka 20 zinatoka, ambazo zinabeba mchele kuja Dar es Salaam. Sasa kwa nini Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ndugu yangu Magufuli na Mheshimiwa Mwakyembe, chonde chonde wanisaidie, barabara ile imeua mtu safari hii kwa sababu ya mgogoro wa hiyo hiyo kuzuia mazao yao yasiende sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina barabara muhimu ya kwenda Madibira. Barabara ile inaanzia Rujewa kwenda Madibira. Ni ukweli usiopingika kuwa kila mtu anafahamu Madibira inavyozalisha mpunga. Lakini barabara ile ambayo inakwenda kule mpaka leo iko katika hali mbaya sana. Hawana umeme pamoja na uzalishaji wao mzuri. Kiwanda kile kimeshindwa kufanya kazi kwa sababu umeme hakuna. Je, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini haoni sasa wakati umefika wa kuhakikisha Madibira inayozalisha mchele mwangi wa kulisha Taifa hili inapata umeme na kuhakikisha kwamba mitambo ile sasa inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania sisi siyo maskini. Tuna rasilimali nyingi sana. Tunao wafugaji amba ni rasilimali za Taifa, lakini wafugaji hawa wameachwa utafikiri nchi hii haina mwenyewe. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mifugo ambaye yuko sasa, waonekane wafugaji wana mwenyewe sasa. Haiwezi kabisa watu hawa wanaambiwa hapa mwondoke, mara pale mwondoke, mara pale mfanye hivi, inaonekana ni watu wasio na maana. Lakini kila siku sisi hapa ni lazima tupate nyama ya ng'ombe, sasa kwa nini watu hawa tusiwijali? Kwa nini tusiimarishe Viwanda vya Nyama ili kusudi mifugo yao ipate soko tukaiheshimu na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa dhati kabisa kuwa, sasa wakati umefika wa kuona wafugaji ni marafiki sio maadui kama ambavyo tunawafikiria. Ndugu zangu lipo tatizo kubwa Mbarali, naomba Serikali hii mnisaidie Mbarali ipate utulivu, hakuna utulivu Mbarali hata kidogo. Naongoza Jimbo ambalo wananchi wake wana mashaka. Toka *TANAPA* waingie Mbarali tulichokitegemea sicho, *TANAPA* sasa imekuwa ni mzigio. Wananchi wa Mbarali walitegemea kuwa *TANAPA* imekuja ni neema, lakini imekuwa ni bahati mbaya. Kwa sababu kikao cha *RCC* kilichokaa tarehe 25 Julai, 2006 kilikubali kuridhia *Usangu Game Reserve* iunganishwe na *Ruaha National Park* kwa masharti kwamba mipaka yake itafuata makubaliano ya *RCC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 18 Februari, 2008, Baraza la Madiwani baada ya uhamisho ule ulioridhiwa na *RCC* kuviondoa vijiji vile vya Hifadhi baada ya kuunganishwa kuwa sasa wananchi wanaozunguka eneo lile wahame kupisha vyanzo vya maji na vitu vingine. Wananchi wale tukawahamasisha, wakahama, wakaondoka na wakalipwa stahili zao japo mpaka leo bado wako Mahakamani wanadai walipunjwa na mimi nasema Serikali hii kama itakuwa inapeleka fedha kulipa watu, haifuatili kukagua kwamba fedha zile zimefanyaje. Nina uhakika, fedha zile kama zingefuatiliwa kuna watu wangekuwa hawapo kazini sasa. Fedha zile zimechakachuliwa lakini hakuna mtu aliyefuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uhamisho ule amba vile vijiji viliviyohama vilikuwa ni Kata nzima ya Msangaji, kulikuwa na shule nane kule, nitapata tabu ya kuzitaja zote, muda haunitoshi. Shule zile nane zilizotakiwa kujengwa kwa ahadi ya

Serikali kuwa mtahamishwa na shule zenu ni shule mbili tu zilizojengwa. Wanafunzi wengine wote walipotea hivi hivi, haieleweki waliishia wapi. Kama hiyo haitoshi tulipokaa tarehe 18 Baraza la Madiwani mwezi wa pili, mwaka 2008 tulifanya tathmini ya uhamisho ule, tukagundua kuwa kwa kweli wananchi wamepata hasara kubwa sana. Tumepoteza wanafunzi wengi ambao hawajakwenda shule, ahadi ya Serikali haikutimia. Sasa tarehe 18 hiyo tulipokaa, Baraza lilikataa, tukawa tumeletewa taarifa nyingine kuwa, vijiji vingine tena vinatakiwa vihamishwe. Tukahoji, tena tulikuwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwenye kikao hicho. Tukasema kwamba, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, hatuwezi tena kukubali kuhamisha wananchi wakati wale wengine tu bado wanapata shida.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, nakushukuru sana, muda wako umekwisha.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Mkaofi)*

MWENYEKITI: Anayefuatia sasa hivi ni Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi. Wafuatao wajiandae, Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Kigwangala Hamisi na Mheshimiwa Desderius Mpata. Mheshimiwa endelea Brigadia Generali Ngwilizi.

MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti na awali ya yote nami nichukue nafasi hii kuwashukuru ndugu zangu wa Jimbo la Mlalo kwa kunipigia kura za uhakika asilimia 80 na kuweza kuja kuingia kwa safari nyingine katika Bunge lako Tukufu. Vile vile nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali hasa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo wameweza kuwasilisha kwa upande wa Mheshimiwa Rais Mpango ule wa Maendeleo wa Miaka Mitano na vile vile Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwa sisi wenye Watanzania kupongezana, kupongezana kwa jinsi ambavyo tumeweza kutimiza miaka 50 ya uhuru. Tumetimiza miaka 50 ya uhuru tukiwa na amani. Hilo siyo haba, ninachoomba ni kwamba, sisi ambao tumepewa fursa hii ya kuwa katika nafasi hizi tuwe na jukumu moja, jukumu la kudumisha amani. Jukumu la kudumisha amani ambayo imejengwa na viongozi waasisi wa Taifa letu ili na sisi viongozi watakaotufuata miaka 50 ijayo wawe na sababu ya kutushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Miaka Mitano tuliuopitisha hapa wiki iliyopita, ni mpango ambao una malengo mazuri sana. Ni mpango ambao unatekelezeka. Lakini mpango ule utatekelezeka tu iwapo Watanzania tutakuwa na nidhamu ya kazi. Nidhamu ya kazi katika Taifa letu sasa hivi ni kitu cha mashaka kidogo. Siwalaumu wakulima na watu walioko vijijini kwa sababu ni watu ambao wanafanya kazi kweli

kweli. Kitu ambacho kinatia wasiwasi ni wenzetu ambao wako maofisini. Tunajua jinsi gani ambavyo katika ufanyakazi wetu hatuzingatii muda wa kwenda Ofisini. Mfanyakazi unamkuta badala ya kufika kazini saa 1.30 anaingia saa nne, anakaa ofisini saa moja, saa mbili anaondoka. Katika hali hiyo kama huo ndiyo ufanya kazi, ukweli ni kwamba Mpango ule wa Maendeleo hautekelezeki, utabakia katika maandishi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la huduma za jamii. Huduma za jamii kwa maana ya elimu, afya, barabara, maji na kadhalika. Mpaka sasa tunachukulia huduma za jamii kana kwamba ni kitu cha anasa. Huduma za jamii siyo kitu cha anasa ni kitu cha kufa na kupona. Kuna maeneo ambayo yana ukame wa maji, ni lazima Serikali ifanye kila kitu na kila njia kuhakikisha kwamba wananchi wale wanafikishiwa maji. Barabara sasa hivi tuna ngazi za barabara za Taifa, Mkoa na barabara za Halmashauri. Lakini ukweli ni kwamba iwe ni barabara ya kijiji ama barabara ya Taifa bado mwananchi yule anahitaji barabara hiyo na kama hawezi kuipata basi kwake ni kilio kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu, ni kweli tumepiga hatua nzuri sana. Tumejenga shule nyingi tu lakini tuna matatizo ya Walimu, maabara na kadhalika. Lakini kitu ambacho napenda kuishauri Serikali ni kwamba sasa hivi hasa kwenye shule za msingi na shule za sekondari bado kuna utaratibu wa kuwafukuza watoto wa shule kama baba yake hajalipa hiki ama kashindwa kutoa mchango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mwanafunzi ambaye anategemewa kujilipia fees au kujitafutia mchango. Mtoto wa shule anapokwenda shule inajulikana mzazi wake ni nani. Rai yangu ni kwamba, Serikali sasa ingekuja na sera au mtazamo kwamba itaje waziwazi, hakuna mtoto wa shule anayekwenda shule atarudishwa shulen. Kama kuna tatizo linahusu michango na kadhalika mzazi wake atafutwe. Hapo ndiyo jinsi ambavyo tunaweza kuanza kujenga nidhamu. Mzazi yule atafutwe na kama ni kulimishwa vibarua alimishwe, kama ni kufungwa afungwe. Lakini mwanafunzi yule asiwe na haja ya kukatishiwa maendeleo yake na haki yake ya kuhudhuria shulen. Naamini kwamba Serikali ikiweza kusema hilo wazi basi tutakuwa tumewapatia wanafunzi wetu haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye suala la hali ya chakula. Waheshimiwa Wabunge wa Kanda ya Kaskazini wamezungumza sana. Napenda kuzungumza vile vile hali hiyo inahusu sehemu ya Jimbo la Mlalo. Kuna Tarafa mbili kule, Tarafa ya Mlalo na Tarafa ya Mtae, hali ya chakula siyo nzuri, hatukupata mahindi kabisa kabisa katika msimu wa vuli na mvua pamoja na kwamba zimenyesha katika maeneo mengine lakini kule Mlalo mvua ile haikunyesha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali wakati inasambaza chakula katika maeneo mengine isisahau vile vile wakulima hawa na wananchi hawa wa Tarafa mbili za Mlalo na Mtae. Wakati huu tunazungumzia kwamba Serikali inatoa chakula kwa ajili ya msaada, imepunguza gharama, imepunguza bei. Lakini mahindi yale tusipoangalia

yanakwenda nchi jirani kwenda kulisha watu wengine kule. Itabidi kwa kweli Serikali ichukue kila hatua kuhakikisha kwamba pamoja na kwamba tunawasaidia Watanzania lakini chakula kile hakifujwi kwenda katika nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la umeme. Suala la umeme kama nilivyosema kwenye huduma za jamii kwamba siyo suala la anasa, umeme unahitajika na kila mtu. Kule kwenye Jimbo langu la Mlalo, umeme ultakiwa ufile vile vile kwenye Tarafa ya Mtae. Tarafa ya Mlalo imekwishapata umeme, Tarafa ya Mtae ilikuwa bado haijapata umeme. Umeme ule pamoja na kwamba sasa tunaambiwa *REA* inafanya hiyo kazi, lakini mpaka sasa hivi imekuwa ni kitendawili. Hii nitapenda Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa majumuisho yake aweze kuwaambia watu wa Mtae watapata lini umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuje kwenye suala la utawala bora. Nazungumzia suala la ugatuaji wa madaraka wa mamlaka (*D by D*) tumefanya hivyo tumepeleka Mikoani, tumepeleka Wilayani. Lakini ugatuaji utakuwa na maana kama utakwenda mpaka vijiji na tutakopakabidhi vijiji mamlaka zaidi itawezekana tu iwapo tutakuwa tumewatayarisha viongozi, viongozi kwa maana ya Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, wapewe mafunzo. Tusipowapa mafunzo wale Serikali hii hata tungefanya nini siku zote lawama zitaendelea kuja kwa Mheshimiwa Rais na zitakwenda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini wanaofanya madudu wako kule vijiji. Ni lazima tuhakikishe kwamba, Semina za maelekezi za mafunzo zinaendeshwa ili viongozi wa vijiji wapate mwanga huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya 1960 na 1970 tulikuwa tunasema ili tuendelee tunahitaji vitu vinne, watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Hiyo ilikuwa ni upande mmoja tu wa shilingi. Lakini dunia ya sasa ili tuendelee tunahitaji maji, tuahitaji nishati, tunahitaji miundombinu kwa maana ya barabara, reli, viwanja vya ndege na bandari na tunahitaji chuma *iron and steel*. Hivi ili tuweze kuvitumia ipasavyo ni lazima tukakope. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi ambayo imewahi kupelekwa Mahakamani kwa sababu ya kukopa. Tukakope ili tuweze kukuza vyanzo vyetu hivi, tuweze kukuza rasilimali zetu hizi ili ziweze kuwatumikia Watanzania vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kugongewa kengele. Naamini kwamba niliyoyasema Serikali itayazingatia. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 67(7), naomba mwongozo wako kuhusu utaratibu unaotumika wa watu kuchangia. Kwa sababu katika *list* ambayo ipo hapo ambayo naamini na wewe unayo jina langu ni la 16. Lakini mpaka sasa hivi umemwita mtu wa 18 bado jina langu halijaitwa. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, toka mchana niliombwa nitangaze. Lakini bahati mbaya nilisahau kutangaza. Pamekuwa na orodha mbili, Wabunge mmefanya *lobbying* kwa Watendaji wetu, ikatengenezwa orodha hii. Hii orodha haikuzingatia orodha ambayo ilitangazwa toka jana. Kwa hiyo, orodha ambayo ninyi mnafuata siyo, niliyo nayo ndiyo *original*, hii hapa. Nimepokea maombi mengi sana ooh umenipita, umenipita, sijampita hata mmoja wenu. Orodha ambayo mnayo ninyi ni feki. Naomba tuendelee. (*Kicheko*)

Naomba msifanye *lobbying*. Kuna *memo* nyingi sana hapa, Mheshimiwa mimi nimefiwa, tusifanye hivyo. Tufuate utaratibu, jinsi ulivyoomba na ndivyo ulivyoorodheshwa. Kama ulipeleka *late* maombi yako, subiri ukibahatika utaitwa, hukubahatika changia kwa maandishi. Naomba tuendelee.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Waheshimiwa kwanza napenda nitoe tangazo hili. Habari ya taarifa tutapoteza muda mwingi sana badala ya kuzungumza maneno kwa ajili ya Watanzania, tutaanza taarifa, utaratibu, mwongozo. Naomba mjizue. Tuendelee. (*Makofi*)

Napenda kuwaita wachangiaji, sasa hivi Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa. Kama hayupo Mheshimiwa Capt. John Komba aendeleee.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniruhusu kuwepo hapa na nimwombee afya njema dada yetu Mheshimiwa Mwanakhamisi ambaye alipata dharura ya kuugua asubuhi. Mungu ampe afya njema na *Inshallah* atapona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuongoza jahazi hili vizuri na kwa nia njema kabisa. Kuna usemi unaosema ukiona adui yako anakupongeza sana na anainuka na bango, anakupongeza kwa nguvu zote ujue hapo kuna kasoro. Lakini ukiona adui yako anachukia kwa mafanikio yako mazuri, unafanya vizuri yeye inamuumma, inamkera, hapo umepatia, songa mbele moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu tumepatia, tumekwenda sawa sawa. Bajeti hii ni nzuri, ukienda kuwauliza watu wangu wa kule Nyasa na kule Umatengo, Jimbo la Mbanga Magharibi, watakwambia sisi tulikuwa tunapata mafuta kwa bei ya shilingi elfu tatu kwa lita. Leo mmeshusha mafuta kwa elfu moja mia sita na themanini karibu nusu ya wale watu kule wamepata unafuu. Hiyo ni nafuu kubwa songa mbele umepatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu sasa linatimiza miaka 50. Ni kipindi kirefu, lakini wapo wengine wanasema hayo tuliyo nayo sasa siyo maendeleo na Tanzania

haikupigana vita, wanatoa mifano ya Msumbiji, Zimbabwe, Botswana, walipigana. Wale hawakupigana vita, vita tulipigana sisi hapa Tanzania. Huko ni kukosa tu historia ilikuwaje. Mwalimu alipata uhuru wa nchi hii, alisema uhuru wa Tanganyika hauna maana kama majirani zetu hawatakuwa nao wamepata uhuru. Kwa hiyo, tukaanza kukomboa. Ukizungumza habari ya uhuru wa Zambia, ni Tanganyika au Tanzania. Ukizungumza habari ya Zimbabwe, ni Tanzania. Ukizungumza habari ya Msumbiji, ni Tanzania. Ukizungumza habari ya Botswana, ni Tanzania. Zungumzia Angola, ni Tanzania, zungumzia Namibia, ni Tanzania, zungumzia Shelisheli, ni Tanzania, zungumzia Uganda, ni Tanzania, zungumzia Afrika ya Kusini ni Tanzania, zungumzia Guinea Bissau, ni Tanzania na zungumzia Comoro, ni Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mafanikio mengine ambayo kwako wewe hayana tija sana, lakini yana tija nzuri kwa mwenzio. Yale yana baraka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, uchumi wetu sisi tumeupeleka huko ambako leo wenzetu wanajitawala na wanaonekana ni binadamu. Kwa hiyo, kazi yao ilikuwa ni kutufikiria na sisi sasa. Tumewaokoa, wamejitetawala, watulipe kidogo kidogo, hawajafanya, shauri yao. Lakini tumeendelea kuwepo na sasa hivi tunaendelea kuwepo na tunafanya vizuri. Kaza uzi, tumepatia kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe shukrani kwa Jimbo letu hili la Mbinga Magharibi ambalo naliongoza sasa. Kabla yake tulikuwa hatuna Wilaya mpya, leo Serikali hii imetupa Wilaya mpya. Kwa niaba ya wananchi wale tunaishukuru sana Serikali yetu. Tulikuwa hatuna barabara ya lami, leo hivi ukienda kule baada ya mwaka mmoja tutatembea na lami toka Songea mpaka Mbiga. Hayo ni mafanikio ya Sera nzuri na siasa nzuri za Serikali hii na Chama chake. Tulikuwa hatuna boti za ulinzi katika Ziwa Nyasa, leo tuna boti za ulinzi katika Ziwa Nyasa. Hayo ni mafanikio pia ya watu wetu kule. Tulikuwa hatuna usajili wa hospitali mbalimbali, lakini leo tumepatia. Tulikuwa hatuna vituo vya mawasiliano ya simu, leo karibu Jimbo zima lina simu isipokuwa Kata tatu. Kwa hiyo, hapa nachukua nafasi hii kumwomba Waziri wa Mawasiliano atusaidie katika kupata mawasiliano katika hizi Kata chache zilizobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba akiingia madarakani ataifanya zahanati au Kituo cha Afya cha Mbamba Bay kuwa hospitali. Mpaka leo bado ni Kituo cha Afya. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali kwa vile Mbamba Bay sasa itakuwa ni Makao Makuu ya Wilaya ya Nyasa, basi kituo kile kiharakishwe kupata Hospitali mpya ya Wilaya kama ahadi ya Rais inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo jambo lingine katika usafiri wa Ziwa Nyasa. Ziwa Nyasa, ni Ziwa ambalo wakitaja Maziwa katika Tanzania, watu wengi wanatusahau sana. Wanaanza Victoria, wanakuja Tanganyika, halafu wanasema na Nyasa; kama vile hatupo hatupo vile! Sasa hii mantiki hii igeuke sasa, kuna siku nilisema humu msifikiri majina haya ambayo sisi kule tunayatumia, sijui watawala wetu wa kule walikuwaje sijui! Wanatumia Komba sijui, Mapunda sijui, nani, Tembo, Nguruwe! Haya nilisema ni majina tu, lakini sisi ni watu kama nyie humu ndani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kusafiri kama nyie, tunapenda kupata huduma kama nyie! Kwa hiyo, msifikirie majina, majina yaweke pembeni, sisi ni binadamu! Kwani mie unanionaje hapa? Mimi ni nguruwe? Mimi ni komba? Mimi ni binadamu, mimi sio mnyama! Kwa hiyo, wote wana majina haya kule lakini ni binadamu wasaidieni, Ziwa Nyasa mmelitupa, limetupwa kabisa! Ziwa Victoria leo linachangamkiwa kwa sababu walipandikiza samaki. Leo watu wanakuja pale, minofu ya samaki, tukiwaambia jamani na sisi tupandikize samaki, leo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, imetuambia kwamba sisi tuhamasishe mabwawa ya samaki yaani jambo hili nikienda kulieleza Nyasa kule, mimi sitakuwa Mbunge! Yaani niache kuhamasishe samaki Ziwa Nyasa, nihamasishe haya sasa jengeni mabwawa ya samaki! Yaani watu waache kuvua kwenye maji mengi, wavue kwenye mabwawa? Mimi sitarudi tena hapa! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nikubaliwe tupandikize samaki. Malawi wanapandikiza samaki, Malawi wanalisha samaki, samaki hawako huku Tanzania wako Malawi kule! Sisi, ooh, Sheria inabana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lowassa yule, alitoa maji kutoka Ziwa Victoria mpaka Kahama, wakati Sheria inasema msitoe maji, mpaka watu wa Libya kule watu gani sijui wa Misri kule waseme! Tuna maji hatuna maji?

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maji.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa nini samaki msipandikize? Mnaniambia mimi nikachimbe mabwawa, mimi nipande samaki! Hii itakuwa ni aibu kweli kweli! Mna maji mengi, unasema chimba bwawa! Halafu nifanyeje, niogelee au nifanyeje? Naomba Waziri wa hivyo vitoweo hivyo, mifugo na samaki, unapotoa sera kama hizi, ufikirie tayari kuna watu tayari wana maji mengi, wanahitaji samaki, wavue vizuri, sio bwawa! Bwawa wanafuga hao Wamasai, wanafuga akina Mheshimiwa Lowassa, kwa ajili ya wanyama. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa samahani. Taja wadhifa wa Mheshimiwa Lowassa. (*Makofi*)

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lowassa mimi ni rafiki yangu sana na wadhifa wake naujua. Hata nikintaja Mheshimiwa Lowassa, anajua tu kwamba Komba ananitaja mimi, basi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kuhusu walimu. Katika maeneo ambayo walimu hawapo, hawapo kabisa, sio wapo nusu au wapo kidogo, hawapo kabisa, ni wilaya hii mpya ya Ziwa Nyasa. Hakuna walimu kabisa, shule haina walimu, sekondari zote zina mwalimu mmoja ama si mwalimu mmoja, kuna wanafunzi wa *form six*, wamegeuzwa kuwa walimu wako kule, sasa elimu itatoka wapi? Kwa hiyo, leo nimeambiwa tupata walimu wengi baada ya miaka miwili, anza na Mbinga Magharibi, tupelekee walimu kule. Sisi kule watu wengi sana waliosoma katika nchi hii wametoka

upande ule kule. Akina Alfred Tandau, akina Kambona, akina sijui Komba, John Komba, akina nani, wote tumetoka huko! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule tulikuwa tunasomeshwa na wazungu, wazungu hawapo sasa! Tupo Watanzania, peleka walimu kule, wanasomeshwa na wanafunzi wa *form four, form six!* Utamu wa elimu utatoka wapi? Kwa hiyo, mimi naomba sana kwa sababu mmesema miaka miwili, nina hakika Mungu atanipa afya, nitabaki kwenye Bunge hili na ninajua mtanisaidia kupeleka walimu kule katika shule zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuhusu minara ya simu; ni muda mrefu sasa nimezungumza habari ya kampuni hii inaitwa *Tigo*. *Tigo* imejenga mnara miaka minne iliyopita, imeweka mnara pale haufanyi kazi yoyote na kila nikiuliza swali humu ndani, ooh, watakwendu kesho, wataenda kesho kutwa! Sasa nakwambia Waziri unayehusika na hii, kawaambie wakang'oe; tumechoka kuangalia juu, shingo zinatuma. Kawaambie sasa wakang'oe maana sisi si akina komba, akina nyani sisi, wakang'oe! Miaka minne mlingoti uko pale, mnara uko pale, haufanyi kazi! Ahadi juu ya ahadi, ahadi juu ya ahadi! Tutafika wapi? Kwa hiyo, nawaomba ama waka... lakini nirudishe kidogo, ama mkang'oe ama mrekebishe sisi tupate simu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho niwaambie wananchi wangu, kwamba wenzangu wamepewa hela za kununua gari, wamenunua magari sijui mashangingi, manini! Mimi wananchi wangu niwaambie msikie, nimenunua trekta, nimenunua *harrow*, nimenunua majembe, nimewaleteeni huko mlime mashamba, hakuna kulima kwa jembe la mkono sasa. Kazi yao ni kuchangia mafuta tu, lakini watatumia trekta la Mbunge, kufanya kazi hiyo, nimefanya kazi hiyo. Na naomba Wabunge wengine, fuata mfano huu mzuri, mashangingi achana nayo, lima, tafuta trekta peleka kule, utakuwa Mbunge wa kudumu kama mimi nitakavyokuwa wa kudumu mpaka naacha. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naomba nitumie fursa hii adhimu sana kwangu, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mimi siku hii ya leo kusimama hapa katika Bunge hili lako Tukufu, ili ikuwasemea wana Nzega, walionitura na walionichagua mimi kwa kura nyingi na kwa kunipa ushindi wa kishindo ili niweze kuja kuwasemea hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kusema kwa niaba ya Mzee Shaibu Sudi wa Kitongoji cha Mkwajuni na wazee wenzake. Naomba nitumie fursa hii kusema kwa niaba ya Mama Fatma Mhina na wazee wenzake, ambao miaka 13 iliyopita walidhulumiwa ardhi yao halali ya asili, urithi wao kutoka kwa wazee wao, wakanyang'anywa na ardhi hii ikapewa kwa wawekezaji wa Mgodi wa *Resolute*, leo nitawasemea. Nitawasemea kwa sababu wamenipa nguvu ya kuja kwawakilisha ili nije

niseme yale ambayo wao yanawakera. Ni dhuluma kubwa, ni dhuluma ya kipekee, ni dhuluma ambayo haiwezi kukubalika hata dakika moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba niwasemee watu hawa ili Serikali iweze kuwatendea haki. Walipwe fidia, walipwe ardhi yao, wapewe mahali pa kulima, lakini zaidi ya yote wawe *compensated* kwa kunyang'anywa ardhi yao ambayo ilikuwa ni halali. Uwekezaji katika migodi umekuwa hauna faida yoyote kwa Taifa letu. Hata fidia hawapewi, wakati huo huo migodi hailipi kodi, wakati huo huo migodi inaendelea kuwafadisha wananchi wachache ambaao ni wajanja kuliko wengine, wakati hata wale ambaao walikuwa na haki ya kumiliki ardhi hawapewi fursa ya kulipwa fidia yao, hawapewi fursa ya kuchimba dhahabu yao ambayo iko katika ardhi yao, asili yao! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo hii niiombe Serikali, kama kweli ni sikuvi basi isikie kilio cha wananchi wa Nzega, katika Vitongoji vya Mkwaluni, Isanga, Lusu, Batinge, wapewe haki zao. Ndugu zangu wa Isundangwanda, wapewe haki zao, walipwe fidia, la sivyo wana Nzega wamenituma nije niseme na salamu za wana Nzega zinasema kwamba, kama Serikali ikiamua kuendelea na msimamo wake ambaao umedumu kwa zaidi ya miaka 13 leo hii, kama Serikali itaendeleza msimamo huu, wananchi wa Nzega wamenituma nije niseme hapa kwamba wao watachukua sheria mkononi, wataamua kwenda kuufunga ule mgodi kwa mikono yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa *Resolute* ulianzishwa takribani miaka 13 iliyopita na katika *design* yake ulikuwa unatakiwa uzalishe *ounce* 160,000 za dhahabu ambazo kwa kipindi kile zilikuwa na thamani ya dola za Kimarekani 230. Miaka mitatu baadaye thamani ya dhahabu ikapanda kufikia dola za Kimarekani 640 kwa *ounce* moja ya dhahabu. Leo hii tunapoongea hapa, *ounce* moja ya dhahabu ambayo inachimbwa pale Nzega, ina thamani ya dola za Kimarekani, 1,600. Lakini watu wa Mgodi wa *Resolute*, wameweza kuchimba dhahabu hiyo na wanaendelea kuiba maliasili ya Watanzania kila siku na wanavuna zaidi ya 160,000 na wanauzwa kwa bei ya juu zaidi, lakini hawalipi kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameanza kulipa kodi mwaka jana baada ya kuchimba dhahabu kwa zaidi ya miaka 12! Hii haikubaliki na sisi wana Nzega tunasema kwamba imetosha. Imefika wakati mtu asimame, asimame imara na aseme imetosha. Wizi huu umetosha na tumechoka kuendelea kuvumilia wizi wa maliasili ya Tanzania bila faida yoyote ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasaeme kwa sababu ninajua. Miaka 20 au 30 ijayo, watoto wangu na wajukuu zangu watahoji, baba ulipata fursa, babu ulipata fursa ya kutuwakilisha Bungeni, ulisema nini kuhusu maliasili yetu ya dhahabu? Ni bora dhahabu hii ikabaki ardhini kuliko kuendelea kuwafadisha wachache ambaao wanasaini mikataba ambayo haina tija kwa Taifa letu. Leo nasema ili historia siku moja isije ikanihukumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanda kwa thamani ya dhahabu hadi kufikia dola za Kimarekani 1,600 kwa *ounce* moja, ni ongezeko kubwa sana. Kwa Serikali iliyio makini, kama inavyotaka kuaminika kwamba Serikali yetu ni makini, naomba sasa Serikali ichukue hatua za dhati za kudhibiti, za kudai *windfall gains tax* na pia *ringfalls tax* ili basi Tanzania iweze kufaidika na ongezeko la thamani kwenye dhahabu inayochimbwa nchini kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mgodi wa uchimbaji wa dhahabu wa *Golden Prime* ambao unamilikiwa na kampuni ya Kiaustralia ya *Resolute* ufunguliwe pale Nzega mwaka 1998 na Rais Benjamin William Mkapa, umezalisha zaidi ya *ounce* milioni 2.2 ambazo kwa hesabu za haraka haraka kwa *average price*, ina-fall kuleta thamani ya mauzo yote ya dhahabu ambayo imechimbwa pale kwenye ardhi ya Nzega, isiyopungua trilioni 1.2.

Lakini mapato ya Tanzania kwa ujumla ukichukua *royalties* kwa maana ya mrahaba, ukichukua kodi ambayo wawekezaji hawa wa *Resolute* wamelipa kwenye Serikali yetu, *total* toka kampuni hii imeanzishwa mpaka leo hii ni milioni 30 tu za Kimarekani, ni chini ya 4%! Na katika mrahaba ambao Serikali yetu inalipwa na kampuni hii, tayari tunafahamu kuna madudu kama *Alex Stuart Affairs* wanachukua 1.9% ya *royalty* ambayo inalipwa kwenye Serikali yetu! Huu ni udhalimu, ni wizi wa wazi na Watanzania tusiendelee kuukubali wizi wa aina hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba nipewe Mkataba baina ya Serikali na Kampuni ya *Resolute*, leo hii ni zaidi ya miezi saba. Kwa masikitiko yangu makubwa naomba niseme, kwa kutumia *channels* za kihalali za Serikali, mimi kama Mbunge, sijapata fursa ya kupata kuuona Mkataba huu. Mkataba umefanywa siri, nimefuutilia kwa nguvu, kwa ushahidi, kwa *dispatch*, kwa barua, kwa kila aina ya jitihada ambazo ningeweza kuzifanya mimi kama Mtanzania, kama Mbunge mwenye uzalendo na mwenye uchungu na maliasili ya Tanzania, sijapata Mkataba mpaka leo hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namshukuru Mungu, wasamaria wema wamenikabidhi Mkataba huu na nimeusoma. Yaliyomo humo ni madudu matupu, unashindwa kuelewa kuna uzalendo au kuna usaliti katika nchi hii! Leo hii Wabunge, Mawaziri, tunafaidi ma-*Range Rover*, tunafaidi mashangingi, yote haya ni mali ya Watanzania. Sitaki kusema kwamba tunyang'anye magari haya, sitaki kusema Mawaziri wanyang'anywe magari haya, lakini nataka kusema je, tunafanya kazi ambayo ina thamani ya heshima tunayopewa na Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhoji je, sisi tunafanya kazi ya halali ambayo tunapaswa kufanya kama tulivyotumwa na Watanzania? Je, ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja, anapokaa kwenye lile gari lake, anajifikiria nini? Je, ndugu yangu Mheshimiwa Ngeleja, ambaye amepewa dhamana ya kumshauri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anapokaa kwenye lile shangingi, anapokaa kwenye *oval office*, kwenye *first grade car*, kwenye *first grade house*, anafifikiria nini? Je, anamfikiria Mtanzania kweli? Ameisoma hii mikataba na kuielewa? Nafahamu ni

Mwanasheria. Amesoma ripoti ya Jaji Mark Bomani? Nashindwa kuuona uzalendo kwa viongozi ambao wamepewa dhamana ya kuliongoza Taifa letu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kuuona uzalendo kwa viongozi ambao wamepewa dhamana ya kuliongoza Taifa letu. Kama kweli tungekuwa tunawatendea haki Watanzania, kama kweli tungekuwa tunaipenda nchi yetu kwa dhati, basi bila shaka tungeweza kuangalia upya mikataba ya madini na hata ikiwezekana basi tukaacha kuwekeza kwenye madini, mali hii ikabaki chini pengine watoto wetu na wajukuu zetu, watakuwa na akili zaidi yetu, wataweza kuzi-utilize hizi *resources* ambazo tumekuwa-endowed na Mwenyezi Mungu, bila gharama yoyote ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiombe Serikali isitishe uwekezaji zaidi katika madini. Leo hii ukiangalia akina *Jimmy Sinclair* na makampuni yao *Tanzania Exploration*, wanaendelea kufanya uchunguzi, wanaendelea kumiliki leseni za maeneo, nchi nzima imeuzwa kwanye migodi! Nilikuwa nasoma hapa ripoti, ni ripoti kubwa sana, ni ripoti ya watafiti. Nimesoma ripoti mbalimbali, ya akina *Curtis*, ya akina Lissu, nimeona mambo mengi ya ajabu, nikashindwa kuelewa, nikashindwa kuelewa uzalendo wetu unaanza wapi na unaishia wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali watoto wa nchi hii tuseme sasa basi na leo hii naomba niseme, Serikali ifanye maamuzi magumu, kama imeshindwa ku-nationalise *resources* za Watanzania, basi ni bora tukaishia hapo, tukaacha kuwekeza na hii migodi ikabaki kuwa ni historia, ikabaki kuwa historia mbaya ambayo haijatufaidisha katika Taifa hili. Naomba sana Serikali izingatie ushauri huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili inakwenda moja kwa moja kwenye *accountability and responsibility*. Tumeshuhudia mikataba mingi mibovu, tumeshuhudia watoto wengi wa Tanzania, wamepewa dhamana, wamepewa elimu ya kutosha, wamekwenda kusoma, wamerudi, wamekuja ku-draw mikataba ambayo haina faida ambayo haina tija kwa Taifa letu. Lakini hata siku moja hatujasikia mtu akiadhibiwa kwa kuliingiza Taifa katika mikataba mibovu, kwa kuliingiza Taifa katika mikataba mibovu, kwa kuliingiza Taifa katika hasara kubwa. Naomba Serikali iwe *accountable*, naomba Wabunge tuwe *accountable*, naomba Wabunge na Serikali kwa ujumla tuwe *responsible*, tuweze kuitendeka haki nchi yetu la sivyo, hatuwezi kufikia ndoto za watoto wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa naomba niseme kwa niaba ya watoto wa Nzega, naomba niseme kwa niaba ya akinamama wa soko la Kikwete ambao wanahangaishwa, wanazumbuliwa, wananyanyaswa kila siku na Maafisa wa Kodi. Naomba niseme kwa niaba ya ndugu zangu wa Kata ya Ndala ambao kila siku wanadaiwa kodi, lakini leo hii tunakaa hapa tunajadili wakati makampuni makubwa yanayochimba dhahabu, maliasili ya Taifa letu yanaondoka bila kulipa kodi, yanaondoka na asilimi amia moja ya faida ambayo wanapata katika migodi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda niseme sasa basi! Kama tunashindwa kuchaji kodi kubwa kutoka kwa mashirika haya makubwa, basi tuwaache na mama ntilie

bila kuwachaji kodi wala ushuru, tuwaache wenye vioski vyenye mtaji wa shilingi 300,000/= bila kuwachaji kodi wala ushuru, hapo tutakuwa tumewatendea haki Watanzania, tutakuwa tumeitendea haki nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa niaba ya watoto ambao leo hii wakiniona nasimama naongea hapa, wanatamani nao kuwa Wabunge. Mimi nimetoka mbali, nimetoka kwenye mitaa ya uswahilini ya Nzega Mjini, nimebahatika, nimekwenda mpaka Chuo Kikuu na leo hii nimefika kuwa Mbunge, hii ni historia ya matumaini kwa watoto wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Kabwe Zitto ametoka mitaa ya Mwanga, amefika mpaka Chuo Kikuu leo hii ni anajenga hoja katika mjengo huu. Mheshimiwa Waziri Mkuu Pinda kutoka katika mashamba ya kule Mpanda, amesoma kwa fedha za Watanzania, amefika Chuo Kikuu, leo hii amefika kwenye Bunge hili akiwa kama Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya ni *story* za matumaini ya Watanzania. (*Makofi*)

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunibariki na kunikirimu uzima na leo nipo kwenye Bunge, nafasi ambayo nimeigombea muda mrefu sikuipata. Naomba nikishukuru chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kunitueua, naomba niwashukuru wana Nkasi kwa kuwekeza imani yao kwangu, kwa kutazamia kwamba mimi nitawasemea kwa niaba ya Jimbo zima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Nkasi Kusini lina changamoto nyingi na changamoto ambazo zinaweza kuwa tofauti na majimbo mengine, niishukuru Serikali leo tunashuhudia barabara ya lami, mafanikio makubwa sana kwa Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Leo tunashuhudia hatua nzuri sana za kupata umeme, tumewasumbua sana Mawaziri hapa lakini leo tunaona matokeo ambayo hatujawahi kuyaona tangu tupate Uhuru, ni mafanikio makubwa sana ya Chama cha Mapinduzi, naamini kwa *trend* hii tutakwenda vizuri lakini zipo changamoto, juzi niliuliza swalii moja hapa la barabara, ipo barabara ya Nkana-Kala kilomita 67, ipo barabara ya Kitosi-Wapembe, kilomita 68, ipo barabara ya kutoka Namanyere kwenda Ninde, kilomita 40, barabara hizi ni changamoto kubwa kwa jimbo zima la Nkasi Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa jimbo la Nkasi Kusini wamegawanyika katika kanda mbili, kanda ambazo zinategemeana, ukanda wa juu ukiwa unashiriki katika kilimo, ukanda wa chini ni wavuvi, maskini wenzangu wale bila kuapelekea chakula kuititia barabara hizi hawawezi kuendesha maisha yao. Hizo barabara nilizisemea majibu yale sikuridhika sana naomba Ofisi ya Waziri Mkuu na bahati nzuri Waziri Mkuu anazifahamu vizuri, Mheshimiwa George Mkuchika anazifahamu vizuri, mnisaide barabara hizi na wananchi wanasiakia kwamba nazisemea kwa kasi inayotakiwa. Ni barabara ambazo hazitakiwa kupuuzwa wananchi na akinamama wamefia njiani wengi wakiwa katika kunusuru hali ya uzazi, wamefia njiani mara nyingi, Mheshimiwa Waziri

alitusaidia ile gari nayo imeshaanguka, imeshaanguka kwa sababu ya maporomoko, hii barabara inaenda kwenye bonde la ufa la Ziwa Tanganyika ndiyo maana ina changamoto nyingi. Kwa hiyo, inahitaji kuangaliwa kwa namna ya pekee zaidi, naomba barabara hizi tatu ziangaliwe kwa jicho la pekee, naliomba Bunge katika Bajeti hii Mheshimiwa Waziri Mkuu ututazame kwa jicho la huruma na hasa kwa vile unaifahamu vizuri barabara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo tunayo ni katika kilimo, wananchi wetu wa jimbo la Nkasi Kusini ni wakulima, sisi hatuombi chakula, sisi tunajitosheleza chakula na tunazalisha chakula cha kuwalisha Watanzania wengine, tuna changamoto za barabara za kuunganisha vijiji vilivyoko katika maeneo mazuri ya uzalishaji. Ipo barabara ya Kasu – Katani, Chonga - Charatila, ni changamoto kubwa inaunganisha vijiji vinavyolima sana mahindi, iko barabara ya kutoka Milundikwa kwenda Kisula, Milundikwa - Malongwe, kutoka Kalundi kwenda Sintali ni barabara ambazo zinahitaji msaada mkubwa wa kuzihudumia ili wakulima waweze kupunguza gharama katika kilimo chao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini changamoto nyingine katika kilimo haijaishia katika barabara, ni masoko ya mazao ya wakulima, masoko ya mahindi yanatutatiza, sisi kwetu sasa hivi tumeingiliwa kuna watu wanalangua wananchi kwanza hatujui bei gani wananchi watauza Serikalini, tungeomba hii bei tuitambue ili wananchi wajue kama leo hii wamelanguliwa au hawalanguliwi waamue wa *opt* wamuuzie nani kwa sababu ya soko huria. (*Makofi*)

Lakini masoko yaliyopo ya *NFRA* yamekuwa na changamoto nyingi, hayamjali mkulima mwenye magunia machache, magunia matano, mawili mangapi hawasaidiwi, wanawajali walaguzi hao hao wanaowalangua wakulima kwa bei ya chini ndiyo wanakuwa wa kwanza kuwauzia. Kwa hiyo, kuna kitu kama rushwa naweza nikasema, kama siyo rushwa basi ni changamoto ya wakala huyo wa ununuzi wa mazao ya akiba ya chakula kuwa na watumishi wachache na vilevile kuongeza vituo jimbo zima lina vituo viwili, kuna kituo kimoja kiko Ntaramila, kiko kimoja tu katika jimbo zima kwa hiyo, ningeomba kama vituo vingeweza kuongeza pengine kimoja pale Sitali, kimoja kingine kiwe pale Kasu, kingine kiwe Nkundi, Challa, vingeweza kusaidia sana katika kuhakikisha kwamba wakulima wanapata tija katika mazao ambayo wanazalisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni uvuvi, wananchi wa mwambao wa Ziwa Tanganyika wamekabiliwa na changamoto kubwa na hawajatizamwa kama hivi tulivyoweza kuwatizama wakulima pengine wanetazamiwa kama wakulima wa mahindi. Huku tumeweka ruzuku kwenye pembejeo, tumeweka *power tillers*, tukaleta asilimia 80 ya Serikali na wao walipie asilimia 20 peke yake kwenye uvuvi hili hatujalifanya na wavuvi hawa ni maskini sana kule, wanahitaji tu msaada wa Serikali, naomba Wizara inayohusika iangalie hawa wavuvi, kwa namna ya pekee ile asilimia inayokuwepo kwenye *power tillers*, basi na sisi tuwapeleke kwenye zana zao za uvuvi, tuwatambue ndiyo namna wanavyoweza kuishi kujikimu na maisha yao. Hawawezi kuhukumiwa na jiografia, maskini watu wale wametengwa barabara ndiyo hizo mbovu

nazisema, lakini mbaya zaidi hawawezi kuishi kutumia mazao yanayotokana na bahari wakiwa wanatumia zana duni kabisa kwa hiyo, ni changamoto hii inatakiwa itazamwe kwa namna ya pekee kuwasaidia kwa mfumo huu huu tunaofanya kwenye kilimo, nina imani tunaweza tukawasukuma, mikopo tuwape, wakati tunazungumza huku mikopo ya *power tiller* basi kule tuzungumze mikopo ya zana za uvuvi (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine muhimu katika mwambao ule changamoto nyingine ni mtandao wa simu, kata zangu tatu katika jimbo la Nkasi Kusini halina mawasiliano na Watanzania wengine, watabadilikaje watu hawa? Mama mjamzito akizidiwa hapa hakuna namna ya kumnusuru kwa namna yoyote hata ya kuhitaji msaada kutoka mbali. Namna gani tutapiga hatua kwa namna hiyo, naomba kata ya Kalla, Kata ya Ninde, kata ya Wapembe, zipate kwa haraka mawasiliano ya simu za mkono. Nimeshakuja kwa Waziri mara kadhaa na kuna wakati nimeahidiwa, nina imani kwa heshima ya Chama cha Mapinduzi na uongozi wa Chama cha Mapinduzi, imani ile niliyojenga juu yao na nikawaambia wananchi itatekelezwa. Kwa hiyo, nawaomba sana Serikali iyaone mambo hayo kwa uangalifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ndugu zangu, jambo la mwisho umeme, umeme umeshakuja kwa dalili ninazoziona, lakini ungesogea mpaka Ziwa Tanganyika kwa njia yoyote basi tungeweza kunusuru sana wananchi wa kule, kwa sababu wananchi wale sasa wanaiza samaki wabichi Zambia kinyume na taratibu za sheria inavyoagiza na Serikali inasimamia, inachukua ushuru pale Kasanga, ni mambo ya aibu. Kwa sababu tunachukua ushuru wa samaki wabichi wasiochakatwa huku Sheria ya mwaka 2003 ikiwa tayari inapiga vita kwamba samaki hawawezi kutoka nje bila kuchakatwa, sasa imewanyima wananchi huduma muhimu, akinamama wale waliokuwa wanapata ajira ndogo ndogo hawawezi kupata tena, bado Halmashauri haiwezi kupata ushuru yote haya ni changamoto ziko kwenye jimbo langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo ni ya muhimu sana kwa sababu zipo nyingi ni katika huduma za afya, huduma za afya hazitoshi, vituo vya afya kipo kimoja tu cha Wapembe na bado hakina hata watumishi. Zipo kata tisa hazina vituo vya afya, ni sera ya Chama cha Mapinduzi na tumeitangaza juzi kwa hiyo, katika mwanzo huu tuanze vizuri tukielekeza katika utekelezaji wa sera kama tulivyokuwa tunawatangazia wananchi. Hakuna watumishi wa kutosha, lakini bado hata wale watumishi wachache ambao wanajinusuru kusoma hawapandishiwi maslahi yao naomba nayo hii muione kama ni changamoto kubwa ambayo inahitaji kushughulikiwa. Vilevile walimu, ziko shule za sekondari zangu za Nkana, Milundikwa, Challa, Ninde, hazina walimu, Wapembe, King'ombe zote hazina walimu kabisa kuna walimu wawili, watatu, utegemee mafanikio gani hayo ya kimapinduzi ya kisasa hivi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba Wizara inayohusika iangalie kwa makini tunapozungumzia ubora wa elimu basi tusipuuze mambo ambayo ni changamoto katika kuhakikisha kwamba elimu inakwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na la mwisho ni hizi lugha za kubezana Bungeni, wananchi hawakututuma tuje tubezane, tuwe wakubwa hebu tukue jamani,

wanatushangaa tuseme matatizo yao, mtu mmoja alikuwa amenunua beberu, anaenda kuchinja kwa ajili ya sikuu, vijana wahuni wakapanga njiani wa kwanza akasema tumbabaishe mzee huyu ili tuchukue hii mbuzi imenona, akambabaisha akasema wewe shehe, unaburuza mbwa, akasema wewe mtoto una wazimu, huyu ni mbuzi naenda kumla, akamkuta wa pili, akasema unaburuza mbwa, akakuta wa tatu akasema unaburuza mbwa, shehe yule akafanya nini akakimbia na kumuacha na huyo mbuzi, wale vijana wakachukua kile kitoweo. Sasa hiki ndicho kilichoipanga kwa watu wengine, Tanzania inafanya vizuri kwa mambo mengi, tunahesabiwa vizuri kwa kila takwimu hapa elimu tuko juu, uchumi unakua na nani asiyejua Tanzania ni nchi katika nchi zilizo na uchumi wa nyuma? Unataka matarajio ya haraka ya ajabu ya kiasi gani ambayo uyatarajie kwa wakati mmoja, tunafanya vizuri viongozi msibabaike, Mawaziri mnafanya vizuri mrekebishe hayo tunayoyasema hao lazima watupe changamoto, lakini siyo kwamba wananchi hawana imani na sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi, vilevile nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kwela, kwa imani yao kubwa walihonipa ya kuniwezesha kuingia katika jengo hili, nafasi ambayo nimeitafuta kwa muda mrefu toka mwaka 2000. Naomba wananchi wawe na imani, sitawaangusha, nitawawakilisha vizuri naomba wanipe ushirikiano. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nimshukuru Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa matumaini katika nchi yetu ya Tanzania. Vilevile nitoe shukrani kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa huruma iliyonayo kwa umakini wa kufikiria kutoa chakula kwa watu ambao wana matatizo ya chakula, hiyo ni huruma pekee lazima tuipongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tuwapongeze wakulima ambao wanalima chakula hicho kutoka mikoa ambayo inazalisha chakula kwa wingi na haikupata tatizo la mvua ina maana wakulima hao ni hodari wamelima kimepatikana chakula cha ziada ndiyo ambacho kimetumika katika kupeleka maeneo mengine ambayo hayana chakula nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waswahili wanasema mti wenyе matunda hauachi kutupiwa mawe, kwa hiyo, lazima tukubali Serikali iliyopo madarakani, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo Serikali pekee inayoweza kuleta matumaini na maendeleo kwa Watanzania. Kwa hiyo, changamoto zote zilizopo tuzipokee, cha msingi ni kuzichuja zile zinazowezekana tuzipokee na kuzifanyia kazi na hakuna sababu ya kuchukia ndiyo hali halisi kwa sababu ndiyo mti wenyе matunda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzungumza nataka nizungumzie katika suala la kilimo, tunapozungumza suala la kilimo kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa hatuwafundishi kulima, wananchi wa Mkoa wa Rukwa kilimo ni jadi yao isipokuwa

kinachotakiwa ni Serikali kuziona zile changamoto zinazowakabili zinazowazuia wasiweze kulima, kupanua mashamba yao ndiyo Serikali inatakiwa iziangalie changamoto na changamoto zipo wazi. (*Makofi*)

Kwanza ni uwezesho, wapewe mikopo ili waweze kupanua mashamba yao, wazalishe kwa wingi zaidi na katika kupewa mikopo lazima tuangalie wananchi hawa wa chini bila kurasimisha ardhi, hakuna njia nyingine ya kuwasaidia lazima mashamba yao yarasimishwe, wapate hatimiliki ya mashamba yao ili mabenki yaweze kuwakopesha. (*Makofi*)

Sasa cha kushangaza suala hili limezungumzwa katika Ilani iliyopo sasa hivi lakini ukiuliza mkoa wa Rukwa hata kijiji kimoja ambacho kimeshafanyiwa kazi hiyo ya kurasimishwa ardhi, pamoja na umaarufu wa wakulima, pamoja na sifa kubwa hata kijiji kimoja ambacho zoezi hilo limekamilika hakuna. Kwa hiyo, inakuwa ni maneno matupu, tufike mahali jamani tutende zaidi kuliko kusema zaidi, kwa hiyo, natoa changamoto ili kupanua kilimo kwa wakulima hawa wa chini lazima turasimishe ardhi walijonayo ili waweze kukopesheka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni masoko, mkulima ukitaka kumhimiza alime, ni kumhakikishia soko, baada ya kulima atauza wapi na kwa bei gani ambayo inaweza ikakidhi gharama za uzalishaji. Wakati nakuja Bungeni mimi nimepitia pale kwenye maghala yetu Sumbawanga, maghala yote yamejaa chakula, mazao mengine yapo nje. Sasa wananchi wanasema kama maghala haya yamejaa chakula na sisi hatuna mahali pengine pa kuuza mazao, mazao yetu tutauzaje?

Kwa hiyo, wananchi wa Mkoa wa Rukwa mpaka sasa hivi wana mashaka makubwa, tunaomba Serikali ilijue hilo iwaondoe hofu iwape tumaini ili waweze kuzalisha vizuri kwa mwaka unaokuja maana watakata tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile Serikali lazima iangalie makundi ya wakulima, wapo wakulima wakubwa, wapo wakulima wa kati na wapo wakulima wadogo ambao wengine wana mashamba tu lakini hawana mitaji. Kama Serikali inaweza ikafanya jambo zuri la kuwapelekea chakula ndugu zetu wengine ambao hawana chakula ili waweze kunusuru maisha yao kwa sababu kosa lile siyo la kwao, ni amri ya Mwenyezi Mungu hawakupata mvua. Sasa Serikali inashindwaje kumsadia huyu mkulima ambaye ana ardhi, impe mkopo, imkopeshe alime na baadaye atalipa, maana bila kufanya hivyo tutakuwa tunamgandamiza na maana ile ya kusema kwamba tunataka kuondoa umaskini itakuwa haina maana, ukiangalia mbolea inayotolewa sasa hivi zile *package* tatu, ukiondoa pamoja na ruzuku lakini mwananchi wa kawaida anakaribia ili azipate zile *package* tatu awe na laki moja, sasa wananchi wetu hawana hiyo. Kwa nini Serikali isiwapo bure au iwakopeshe? Nyie si ni kuzalisha, uwezo wa wakulima wanao, mashamba wanayo, kwa hiyo, sioni sababu ya kuwa na mashaka katika jambo hilo, kama tunataka kweli kuwakomboa wakulima wetu tuangalie kwa makundi kwa jinsi walivyo na tuwasidie kulingana na uwezo walio nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kuzungumzia ni kuhusu baadhi ya maeneo, baadhi ya vijiji kuwa na uhaba wa ardhi ya kulima kwa sababu wawekezaji wameingia mpaka katikati ya kijiji yapo maeneo ambayo wakulima wanailalamikia Serikali, wanajenga hasira kwa Serikali kwa wawekezaji wameingia mpaka karibu katikati ya vijiji. Mifano ya vijiji hivyo ninavyo, kijiji cha Sikaungu kata ya Msanda Muungano, kijiji cha Songambele Azimio na Kijiji cha Msanda Muungano chenyewe ukienda ndiyo malalamiko ya wananchi, Serikali ijaribu kuangalia vitu nya namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunasema mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe sasa atakaa na nguvu zake bila kuzipeleka shambani wakati hana mahali pa kulima? Natoa wito kwa Serikali iangalie maeneo haya muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ninachotaka kuzungumzia ni kilimo cha umwagiliaji. Hakika tukitaka kulikomboa Taifa hili lazima tujiwekeze zaidi katika kilimo cha umwagiliaji kwani kilimo cha umwagiliaji ni kilimo chenyeye uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nashangaa hivi karibuni wakati tunasomewa mpango wa miaka mitano, yalitajwa baadhi ya maeneo ambayo ni maarufu kwa kuzalisha zao la mpunga. Nasikitika kuona bonde la Rukwa ukanda wa Ziwa Rukwa halikutamkwa wakati bonde hilo ni maarufu. Ni bonde kubwa lenye mito zaidi ya kumi ambayo haikauki muda wote, ni bonde lenye rutuba, ni bonde ambalo halitumii hata mbolea kwa sasa na pia ni *Eden*. Wananchi wa maeneo yale wanazalisha mpunga tena mpunga mzuri bila kutumia mbolea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aliangalie lile bonde kwani linazalisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija Tunduma maghala yamejaa mpunga unaotoka ukanda wa bonde la Ziwa Rukwa. Ukija Mloo ule mpunga unatoka ukanda wa bonde la Ziwa Rukwa, ukija Mbeya Uyole utakuta akina mama wanauza mchele watakuambia ni wa Sakalilo ambao unatoka bonde la Ziwa Rukwa. Sasa nashangaa Serikali haijaelekeza nguvu katika maeneo haya. Jamani, tutende haki, tutende haki katika maeneo yote mnataka nani aje aseme? Watusemee akina nani? Na sisi wenyewe ndiyo tunatoka katika meneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ukanda wa bonde la Ziwa Rukwa utambulike kwa uzalishaji mkubwa wa mpunga. Mimi ninazo takwimu si chini ya tani 100,000 ambazo huzalishwa kila mwaka kutoka bonde la Ziwa Rukwa lakini nashangaa halipo kwenye takwimu. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Mabaraza ya Ardhi. Mabaraza ya Ardhi yamekuwa ni msaada mkubwa sana kwa utatuvi wa migogoro ya ardhi kisheria. Tatizo mabaraza haya yamekosa uwezo kwani hayana magari, watumishi ni wachache na yapo mikoani. Kwa hiyo, natoa wito mabaraza haya ya ardhi yaende *at least* kila Wilaya kwa sababu umekuwa ni msaada mkubwa sana katika utatuvi wa kisheria kwa upande wa ardhi. Kwa hiyo, naomba Serikali ilione hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Suala hili limekuwa likijirudiarudia na Serikali isipolitambua hili huko mbele linaweza likavunja amani na utulivu tulionao katika nchi yetu. Suala ni Serikali kutolitilia maanani na kulipangia utaratibu wa kulimaliza. Upo ugomvi mkubwa kati ya wakulima na wafugaji wanagombana hatimaye viongozi wanaokwenda kule akipokea rushwa, akipendelea upande mmoja wananchi wanachukia wanaamua kuchukua sheria mkononi na kuua mtu, sasa hii yote ni lazima Serikali iangalie. Juzi tu askari mmoja ameuawa kule Muze, amepigwa mshale na mfugaji mmoja kwa sababu ya hasira. Hakuna chombo ambacho kimekaa makini katika kusimamia utatuzi wa migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma Mkoa wa Rukwa tulikuwa na kitu kinachoitwa Azimio la Mto Wisa, hili lilitusaidia sana katika kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji na hali ilitulia. Sasa azimio hilo lilishazikwa baada ya Mheshimiwa Jaka Mwambi kuondoka na azimio likamfuata. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni miundombinu. Kwanza niishukuru Serikali kwa jitihada inazozifanya na hasa kwa barabara hii ya kutoka Tunduma, Sumbawanga mpaka Mpanda. Tunashukuru kwa jitihada hizo. Lakini lazima tuangalie vilevile na barabara za vijiji kwa sababu ndiko kunakotoka mazao. Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ina kilomita 1004 ambazo ni barabara zinazotegemewa na wananchi, lakini ukiangalia katika mgawo wa fedha za kutengeneza barabara hizo haujapata kuzidi zaidi ya shilingi milioni 450. Sasa shilingi milioni 450 unazigawanyaje kwa kilomita 1004? Matokeo yake ni kulaumu Halmashauri na Madiwani kwamba hawasimamii vizuri lakini kumbe zile fedha ni kidogo. Nichukue mfano kuna barabara moja ambayo ni kero na majuzi nimeomba Serikali iichukue ya kutoka Kalambazite – Illemba. Barabara moja tu inaweza ikachukua karibu shilingi bilioni 1.9 lakini ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzugumzaji*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, tunakushuru sana.

MHE. IGNAS A MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia hotuba ya Waziri Mkuu nilipigiwa Kanuni moja na kwa utamaduni na utaratibu wa Bunge hili ningetegemea kengele ya pili ingefuata baadaye. Kunikata huko kulisababisha sikuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nitumie fursa hii kusema naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITU: Ulikuwa umenogewa na mazungumzao mazuri lakini kengele ya mwanzo ilipigwa kuku-*alert* kwamba muda wako unakaribia kuisha.

Sasa nimuite mse maji wa mwisho kwa leo ambaye ni Mheshimiwa Khalfan Hilaly Aeshi.

MHE. KHALIFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuongea kwa mara ya kwanza ndani ya Bunge lako Tukufu. Lakini la pili, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa afya bora kwa kusimama mbele yenu na kuweza kuwahutubia wananchi wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa tena kwa mara ya pili na naamini atatufikisha pale alipokuwa ametuahidi. Lakini pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuchaguliwa tena kwa mara ya pili na tatu nimpongeze mama yangu mpenzi Mheshimiwa Anne Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mwisho naomba niwashukuru wapiga kura wangu kwa kuniamini na leo niko mbele yako naomba niwaahidi kwamba nitawatumikia kwa moyo wangu wote na kwa upendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwa mambo machache japokuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele yako, tulikuwa tunajifunza mambo mengi lakini sasa hivi ninaamini tunaweza kupata ujasiri wa kuweza kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kwa kuujali Mkoa wa Rukwa hususani Jimbo la Sumbawanga Mjini kwa awamu ya nne kutupatia barabara ya lami kutoka Sumbawanga kwenda Tunduma na kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda na kutoka Sumbawanga kwenda Kasanga. Naomba niishukuru sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiusie Serikali ijtihadi kuweka kipaumbele sana kati ya barabara ya Sumbawanga kwenda Mpanda na kwani naona inasuasua sana. Naomba niiombe Serikali iweze kutoa kipaumbele hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kidogo kilimo lakini wenzangu Waheshimiwa Wabunge waliotangulia wameliongelea hilo, lakini Mkoa wa Rukwa umekuwa ni Mkoa mzuri na wenye ardhi bora na wenye hali ya hewa nzuri. Kwa hiyo, upatikanaji wa mazao kwetu ni mzuri ila tatizo letu kubwa ni masoko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tumelima mahindi mengi sana, tumelima mpunga mwingi lakini tumeweza kuiuza Serikali lakini mazao bado yamebaki mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ninavyokuambia *godown* zote zimejaa na mahindi yale tumeyaweka nje. Sasa namuomba Waziri anayehusika aweze katuondolea yale mahindi tuweze kuyahamisha ili mwaka huu tuweze kununua mahindi mengi tena ya kujaza zile *godown*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana Sumbawanga wana wasiwasi, tumejaza mahindi *godown* na mpaka sasa hivi hatuna taarifa yoyote kama mahindi tunaweza kuyanunua tena na wana wasiwasi kwamba tukiyانunu tutayaweka wapi? Naomba mtuwezeshe kuyasafirisha mapema ili tuweze kuyaondoa pale na kuyapeleka sehemu nyininge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niipongeze Serikali kwa kutuvekeea ruzuku kwenye pembejeo. Serikali ina lengo zuri na wananchi wake lakini tatizo kubwa tumemlenga mkulima lakini si kusudio letu. Wanaonufaika si wakulima bali ni watu wachache amba ni mawakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima hana uwezo wa kununua ile *package* ya vitu vitatu yaani *DAP, Urea* na mbegu, kwa sababu hana uwezo, yule wakala anamdaganya mkulima kuwa saini vocha hii mimi nitakupa mfuko mmoja wa mbegu matokeo yake anapoteza vitu viwili. Sasa kama kusudio letu ni kumsaidia mkulima basi ifike wakati sasa huyu mkulima apewe ruzuku ya moja kwa moja au akopeshwe ile *package* ya pembejeo. Naamini wakulima wa Rukwa hususani wa Jimbo la Sumbawanga Mjini ni waaminifu, wanaweza wakafanya kazi hiyo na wakalima wakalipa deni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona hapa ni kwamba tunamnufaisha wakala wa mbolea na hatumnufaishi mkulima na lengo letu ni kumsaidia mkulima mimi nakuomba na namuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu hili analifahamu vizuri sana tuweze kuwanufaisha wakulima moja kwa moja badala ya kuwanufaisha watu wachache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala lingine la uwanja wa ndege. Ni aibu kubwa sana ndani ya *Mkoa wa Rukwa*. Hapa tulipo hatuna uwanja kabisa wa ndege. Ni aibu kubwa kwani hata uwanja mdogo wa ndege hatuna kwa sababu hata Rais akienda leo hii atashukia Mbeya ndiyo aende Sumbawanga, akienda Waziri Mkuu atashukia Mbeya ndiyo aende Sumbawanga, ni aibu kubwa sana. Nakuomba na ninamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tulipe kipaumbele sana suala la uwanja wa ndege kwani uwanja wa ndege huu ndiyo utaweza kutuletea maendeleo ndani ya *Mkoa wa Rukwa*. Tuna vivutio vingi kama *Lake Tanganyika, Kalambo Falls, Katavi National Park*, Msitu wa Mbizi amba una nyani wekundu peke yake dunia nzima lakini hatuoni watalii kwa sababu watalii wanafisri kwa ndege. Watalii kila wanapouliza tutafika vipi tunawaambia kuna magari wakifkiria magari hawawezi kuja, naomba safari hii uwanja huu upewe kipaumbele zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sumbawanga kuna wawekezaji wamewekeza viwanda vikubwa vya unga, lakini wanapata vikwazo vingi vya kutoweza kuruhusiwa kwenda kuuza unga wanaou-*pack* kwenda kuuza nje ya nchi. Ifike wakati sasa hivi mkulima wa Rukwa naye awe na thamani, ifike wakati mkulima wa Sumbawanga naye ajitambue kama na yeye ni mkulima, analima mahindi lakini bei anapangiwa.

Wakati huo huo jirani zetu wa Rwanda, Congo, Burundi na kadhalika wana njaa, wanatuhitaji sana, wana Sumbawanga na wakulima wa Sumbawanga Mjini. Viwanda vile vimejengwa kwa thamani kubwa wapo *Energy Milling, Great Lake* na hata *Fantashiru*, lakini vilevile havifanyi kazi ni hasara kubwa sana wanaipata. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba uwaruhusu watu hawa waweze kuuza mahindi yao sehemu yoyote watakayokuwa wamepata soko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kuhusu ardhi. Suala la ardhi ni kubwa sana ndani ya mji wetu wa Sumbawanga Mjini. Utakuta mkulima ana eneo kubwa, ila kutanuka kwa mjini inabidi anyang'anywe eneo lake, lile eneo likishapimwa anapewa shilingi 200,000/= halafu vilevile anaambiwa anunue kiwanja kwa shilingi 1,000,000/=, hili linaumiza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike wakati sasa vile viwanja vikipimwa basi yule mtu mwenye kiwanja apewe hata viwanja vitatu yaani cha kwake ye, cha mke wake na watoto, vizuri na wala si ustaarabu sana kama utamnyang'anya mtu eneo lake halafu utampa shilingi 200,000/= na baadaye umuuzie kiwanja kwa shilingi 1,000,000/= mimi nafikiri hili tuliangalie upya. Kwa kweli wana Sumbawanga wanaumia sana na wamenyang'anywa maeneo mengi na makubwa kwa sababu ni mji mkubwa unaotanuka na unaokua kwa kasi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawaongelea Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Tumewaacha sana, tumewasahau lakini hawa ndio watendaji wakubwa, muda wote na wakati wote wapo na wananchi wetu. Sisi tupo Bungeni lakini wenyeewe ndio wanaohangaika. Wakati umefika sasa kama ni sheria ibadilishwe, kama ni Katiba ibadilishwe ili hawa watu waweze kupata mishahara na waweze kunufaika na Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipunguza 12% kwenye Matumizi ya Kawaida ya Bajeti, naamini inatosha kuwapa mishahara Madiwani wote na Wenyeviti wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati ya Nishati na Madini. Mimi nikiwa kama Mjumbe naombwa niwapongeze wote kwa sababu tumekuwa tukishirikiana bega kwa bega na matokeo yake tumeweza kupata jenereta kubwa nne ndani ya Mkoa wa Rukwa hususani Sumbawanga Mjini. (*Makofi*)

Naomba nimpongeze Waziri wa Nishati na Madini, naomba nimpongeze Mwenyekiti wangu Mheshimiwa January Makamba kwa juhudi kubwa wanazozifanya na matokeo yake leo tumeweza kupata umeme Sumbawanga Mjini na unaelekea

Namanyere. Ombi kwa Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa William Ngeleja, naomba umeme ufile Namanyere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutoka Namanyere kwenda Kirando ni kilomita 60, Kirando kule ni sehemu kubwa sana na ina watu wengi sana na tuna *Lake Tanganyika* kule. Nakuomba Mheshimiwa Waziri nikiwa kama Mjumbe wako wa Kamati ya Nishati na Madini nipelekewe umeme huko kwani naamini wananchi wa Kiwando watafurahi sana wakishapata umeme huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nampongeza Waziri Mkuu na napenda kumwambia kuwa wananchi wanakutegemea sana, wewe ni mزالendo na unaipenda nchi yako. Naomba uendelee na uzalendo huo na uendelee na imani yako kwa kupenda wananchi wako, tupo pamoja na tutakuunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nawashukuru na napenda kuwashukuru kwa ushirikiano wenu toka asubuhi mpaka sasa hivi.

Lakini nina matangazo machache kabla ya kuahirisha kikao hiki. Kwanza napenda kuwatangazia wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Bunge kuwa kesho tarehe 25 Juni saa 3.30 asubuhi kutakuwa na kikao katika ukumbi wa Spika. Ni muhimu kufika kwa wakati.

Pia napenda kuwatangazia matangazo yafuatayo, kesho tarehe 25 Juni, siku ya Jumamosi kutakuwa na semina ya masuala ya uongozi itakayotolewa na *Uongozi Institute* katika ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa nne asubuhi, ni muhimu kufika. (*Makofi*)

Pia siku ya Jumapili tarehe 26 Juni, kutakuwa na semina kuhusu sekta za nishati na madini katika ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa 4.30 asubuhi. Mnaombwa mfike bila kukosa. (*Makofi*)

Pia napenda kuwatangazia Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote waliopo ukumbini na Makatibu Tawala kwamba tumealikwa kushiriki katika tafrija ya Ubalozi wa Canada katika hoteli ya VETA saa mbili kasoro robo. Tafadhalii tufike kwa wakati na Waheshimiwa Wabunge wote mmepewa kadi nawatangazia na kuwaomba mhudhurie bila kukosa.

Baada ya matangazo hayo naahirisha kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

(*Saa 1.48 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 27 Juni, 2011 saa tatu asubuhi*)

